# Nipashe

Jumatano Julai 31, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581754

www.ippmedia.com **MWANGA WA JAMII**

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US


**Meya** Jacob, Malisa wakana kukamatwa na polisi



UKURASA 2

**Wahalifu** wa unyanyasaji kijinsia, ukatili watoto kutengwa

UKURASA 4

**Wafanyabiashara** maduka wagomea kodi ya pango

UKURASA 4



Ukurasa 12

Ni wakati 'wanasheria wasomi' wanapoanza kufanya jambo lao

Ukurasa 13

ACT-Wazalendo na harakati mikoani kusaka wanachama wapya 'chapchapu'

siasa

JUMATANO JULAI 31, 2024 Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU

Ukurasa 14

KUJIUZULU KINANA

Kunavyoakisi ukomavu wa demokrasia ndani ya chama

Wanawake wapiganaji wanavyosimamia mageuzi kiutendaji tasnia ya habari

Na Jenifer Gilla

UKURASA 11

# Maporomoko ya Hanang' yachochea ukuaji tatizo afya ya akili

UKURASA 2






Baadhi ya wanafunzi wa darasa la pili katika Shule ya Msingi Lituhi, Wilaya ya Nyasa mkoani Ruvuma, wakiwa darasani wamekaa chini hivi karibuni kutokana na uhaba wa madawati shuleni hapo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

RIPOTI MAALUM

## Uhaba wa walimu, uchakavu wa majengo janga sugu kwa taifa

UK. 5

UKURASA WA 7

## WANACHAMA 200 ACT-WAZALENDO WATIMKIA CCM

WANACHAMA zaidi ya 200 wa Chama cha ACT- Wazalendo wakiongozwa na Mwenyekiti wao Mkoa wa Lindi, Hamidu Bobali, wamejiunga na Chama Cha ...

## Vurugu zaibuka ugawaji vizimba soko la Tandale

UKURASA 3

**MICHEZO** GAMONDI ASHIKILIA NAMBA ZA MASTAA UK.24

**MAONI,** UK.6



Aliyekuwa Meya wa Manispaa ya Ubungo, Boniphace Jacob (kulia) akijadiliana jambo na mawakili wake, Dickson Matata (kushoto) na Peter Kibatala katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu Dar es Salaam jana, kabla ya kuanza kusikiliza kesi inayomkabili ya kuchapisha taarifa za uongo katika mitandao ya jamii, ambapo walisomewa maelezo ya awali. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Maporomoko Hanang' yachochea ongezeko tatizo la afya ya akili

**Na Christina Mwakangale**

UTAFITI uliofanywa na Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe (MNMH), umebaini kiwango cha kesi zilizohusu afya ya akili wilayani Hanang' mkoani Manyara, ziliongezeka hasa baada ya maporomoko ya tope eneo hilo mwaka jana.

Waliopatiwa huduma ya afya ya akili katika Hospitali ya Wilaya ya Hanang' Desemba, mwaka jana, walifikia 25 kutoka kesi tatu Septemba; Oktoba zikiwa mbili wakati Novemba hakukuwa na kesi yoyote.

Katika kesi zilizoripotiwa Desemba, mwaka jana, wanane walikuwa wagonjwa wenye matatizo ya akili waliolazwa katika Hospitali ya Wilaya ya Hanang', watoto wawili, akiwamo aliyejeruhiwa sehemu ya ubongo katika tukio la maporomoko hayo.

Bingwa wa Magonjwa na Afya ya Akili kutoka MNMH, Dk. Sadiki Mandari, alisema hayo hivi karibuni kwenye wasilisho mtandaoni kuhusu 'Afya ya Akili na Majanga ya Asili' ulioandaliwa na Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) kupitia Jumuiya ya Afya ya Akili Tanzania (TMHCoP).

Alisema miongoni mwa walioathiriwa na janga hilo ni waliopata matatizo ya akili, wakiwamo waliokumbwa na kiwewe, msongo wa mawazo na mfadhaiko huku baadhi wakipanga kujitoa uhai.

"Wagonjwa wanane walibainika. Mtoto wa miaka 15 alijeruhiwa ubongo na akawa katika hali ya uangalizi maalumu. Mtoto wa miaka 13 pia alikuwa na msongo wa mawazo," alibainisha bingwa huyo.

Dk. Mandari alisema kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), maafa ni jambo la ghafla la kiikolojia lenye ukubwa wa kutosha kuhitaji msaada wa dharura na kwamba mradi huo kwa wiki tatu uliwafikia watu 3,380 waliopatiwa elimu ya kisaikolojia na tiba ya akili.

"Maafa ni ya aina mbili hasa; asili na yale ya kusababishwa na mwanadamu. Majanga ya asili ni matokeo ya sababu za asili, kwa mfano mafuriko, matetemeko ya ardhi, tsunami na vimbunga vya kitropiki.

"Maafa yanayosababishwa na binadamu yanaletwa na matendo ya binadamu, ikiwa ni pamoja na migogoro ya kijeshi, ugaidi, machafuko ya kisiasa na ajali za viwandani," alisema.

Alisema baada ya tukio la maafa ya janga, athari hutokea kwa binadamu hasa katika akili, huku afya ikiathiriwa kutokana na mtu kushuhudia tatizo ambalo mtu hakulitarajia, ikiwamo kupoteza mali kama vile makazi na jamaa.

"Mradi uliwakusanya baadhi ya walionusurika, kuwapa elimu ya kisaikolojia na tiba kwa waliopata changamoto ya akili na kupatiwa makazi ya kambi za muda. Mradi ukiwalenga walishuhudia tukio, walipoteza wapendwa wao na waokoaji," alisema Dk. Mandari.

**TUKIO HALISI**

Mtoto wa kiume mwenye umri wa miaka 15, mwanafunzi wa shule ya sekondari, mzaliwa wa pili kati ya watoto wanne, ana ndugu wawili ambao wako hai na wanaendelea vizuri.

Alipoteza mdogo wake na mama yake katika tukio la maporomoko ya ardhi (03/12/2023). Baba yake yuko hai na ni mkulima. Mtoto huyo alipata jeraha la kichwa kutokana na tukio hilo la maporomoko ya ardhi.

Alilazwa na kusimamiwa katika hospitali ya Wilaya ya Hanan'g, alikaa hospitalini bila fahamu kwa siku 10. Baada ya kupata fahamu, alipata matibabu zaidi kwa siku tatu kisha kuruhusiwa nyumbani.

Ingawa siku tatu baada ya kutoka, alianza kupata dalili za (kiwewe) zilizozidi kuwa mbaya. Alirudishwa tena katika hospitali ya Hanan'g, na alipatikana na ugonjwa wa 'Bipolar/manic episode kutokana na TBI (traumatic brain injury).

Alitumia carbamazepine na haloperidol. Uchunguzi wa CT wa ubongo ulipata mshtuko. Alipewa rufani ya kwenda hospitali ya kiwango cha juu (Brain MRI ilithibitisha matokeo ya CT Scan.

# Jacob, Malisa wakataa kukamatwa na polisi

**Na Grace Gurisha**

ALIYEKUWA Meya wa Manispaa ya Ubungo, Boniface Jacob (42) na mwenzake Godlisten Malisa (38), wamekataa mbele ya mahakama kuwa hawakukamatwa na Jeshi la Polisi wala hawakupekuliwa katika Kituo Kikuu cha Polisi.

Jacob na Malisa, ambaye ni Ofisa Afya na Mkazi Moshi mkoani Kilimanjaro, walikataa hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Ushindi Swalo, baada ya kusomewa maelezo ya awali na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Job Mrema, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam.

Washtakiwa hao katika kesi ya kuchapisha taarifa za uongo katika mtandao wa kijamii wa X, walikubali taarifa zao binafsi lakini maelezo mengine ya kukamatwa, kufanyiwa mahojiano, kufikishwa mahakamani na kukutwa na vifaa kama simu, walikataa.

Akisoma maelezo hayo, Mrema alidai kuwa Jacob ambaye ni mshtakiwa wa kwanza, baada ya kupekuliwa na askari polisi alikutwa na simu tatu, laini tatu za simu aina mbalimbali na kompyuta mpakato (laptop) moja.

Alidai kuwa Malisa ambaye ni mshtakiwa namba mbili, baada ya kupekuliwa alikutwa na simu mbili na laini moja ya simu.

Ilidaiwa kuwa, Machi 19, 2024 Jacob akiwa ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alichapisha taarifa ya uongo katika mtandao wa kijamii wa X wenye jina la Boniface Jacob @ExmayorUbungo wenye kichwa kilichosomeka 'Mauaji Arusha', kupitia kompyuta mpakato.

Ilidaiwa kwamba taarifa hiyo ilisomeka 'Mwananchi mwenzetu na aliyekuwa dereva wa magari ya watalii Omary Msamo ameuawa na Askari wa Jeshi la Polisi Wilaya ya Karatu mkoani wa Arusha'.

"Omary Msamo ameuawa baada ya kusimamishwa na kushushiwa kipigo kizito kilichosababisha kutoa uhai wake na polisi wa usalama barabarani baada ya kutuhumiwa kuendesha gari akiwa ametumia kilevi," alisema.

Pia Mrema alidai kuwa Aprili 22, 2024 Jacob akiwa ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alichapisha taarifa katika mtandao wa kijamii wa X kuwa 'Wenye leseni ya kuua wameua tena'.

Alidai kuwa maneno aliyoyaandika ni kwamba 'Kijana wetu Rajabu Mlanga Mushi maarufu kama Babu G, amekutwa Hospitali ya Kilwa Road akiwa ameuawa. "'Imagine' (fikiri) tumetoa taarifa Jeshi la Polisi la kupotelewa kwa kijana wetu, cha ajabu Jeshi la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam likawa linatusaidia kumtafuta pia.

"Kila siku Jeshi la Polisi linasema halijapata taarifa wala fununu zozote za kijana wetu na kwamba tuwe wavumilivu wanapambana kuendelea kumtafuta. Jana machale yakawacheza ndugu wa kijana baada ya msiri mmoja kuwatonya ndugu 'nendeni hospitali ya Polisi Kilwa Road mkachungulie vyumba vya kuhifadhia maiti".

Ilidaiwa kuwa Aprili 22, 2024 Malisa akiwa ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alichapisha taarifa za uongo katika mtandao wake wa kijamii Instagram ya jina la Malisagj.

Baadhi ya maneno anayotuhumiwa kuyachapisha ni kwamba 'Aprili 13 Meya mstaafu wa Manispaa ya Ubungo @exmayor_bonifacejacob alitoa taarifa ya kupotelewa na ndugu yake, Robert Mushi maarufu kama Babu G, ambaye alipotea mapema mwezi Aprili 2024.

'Inadaiwa alikamatwa na watu waliojitambulisha kuwa polisi maeneo ya Kariakoo na baada ya hapo hakuonekana tena,' ilisema taarifa hiyo ya Malisa.

Pia Mrema alidai kuwa upelelezi ulifanyika na kuonyesha kwamba washtakiwa wametenda makosa hayo yaliyotajwa kwenye hati ya mashtaka na kusababisha kufunguliwa kwa kesi.

Baada ya washtakiwa kusomewa maelezo hayo, walikubali kuwa taarifa zao binafsi na kukataa maelezo mengine. Kabla ya kusomewa maelezo hayo, upande wa mashtaka uliomba kuwabadilishia washtakiwa hati ya mashtaka ambayo ilisomwa na Wakili wa Serikali, Neema Mushi.

Kesi imeahirishwa hadi Agosti 29, 2024 kwa ajili ya kuanza kusikilizwa kwa mashahidi wa upande wa mashtaka. Washtakiwa wanawakilishwa na mawakili Peter Kibatala, Dickson Mataka na Josephat Msanga.

HABARI KITAIFA

# Vurugu zazuka ugawaji vizimba sokoni Tandale

**Na Jenifer Gilla**

SIKU chache baada ya wafanyabiashara wa Soko la Kariakoo kugomea utaratibu wa kuingia eneo hilo, mgogoro kama huo umeibuka tena katika soko la Tandale, Manispaa ya Kinondoni.

Wafanyabiashara wa soko hilo jana walifanya vurugu katika viunga vya soko jipya wakipinga uamuzi wa viongozi wa soko na Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni kuwabadilishia maeneo ya kuuza bidhaa zao huku wakiwashutumu kuingiza watu wapya.

Aidha, wafanyabiashara hao wamewataka viongozi wa soko hilo wa sasa kuitisha uchaguzi ili wachaguliwe viongozi wa awamu nyingine kwa kuwa muda wao ulishakwisha tangu mwaka 2022.

Wakizungumza na mwandishi wa gazeti hili jana wafanyabishara hao walisema wanashangazwa na taarifa kutoka kwa viongozi wa soko kuwa wamewabadilishia maeneo ya kuuza bidhaa zao kutoka 'ground floor' (sakafu ya ardhini) hadi shimoni tofauti na makubaliano yaliyokuwapo wakati wanapisha ujenzi wa soko hilo.

Mmoja wa wafanyabishara, Pius Paul, alisema walihamia sokoni hapo mwaka 1986 kutoka pembezoni mwa barabara, ndipo mwaka 2019 waliambiwa wapishe ujenzi wa soko la kisasa na kuwekeana maazimio.

Kwa mujibu wa Paul, maazimio hayo ni kuwa jengo jipya likikamilika shimoni yatakaa magari yenye mizigo pamoja na mizigo mizito, ghorofa inayofuata watakaa wafanyabiashara wa nafaka na matunda.

"Hapo meza tisa wakawa wametengewa watu wa vizimba kama wale wa dagaa na vitu vidogo dogo na ghorofa ya kwanza ikatengwa eneo la mama lishe, vibanda vya biashara na ofisi za soko lakini kadiri siku zinavyoendelea kukawa na utata," alisema.

Paul ambaye pia ni Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Shina la Wakereketwa katika soko hilo, alisema walikubaliana na uamuzi huo na kwenda nje ya soko huku wakiendelea kulipa kodi zote wakati wanasubiri likamilike.

Alisema wanashangaa baada ya kusubiri kwa muda mrefu juzi, Mwenyekiti Msaidizi ambaye muda wake umeshakwisha anawapa taarifa ya mabadiliko ya maeneo watakayouza, wakiwapangia wauza matunda kwenda kukaa shimoni ambapo magari ya jumla yanashusha mizigo.

Paul alisema hawaoni sababu ya wao kuhamishiwa shimoni na kuwapisha wauza nafaka kwa sababu kundi hilo halizidi watu 100 wakati eneo hilo ni kubwa, hivyo wanahisi kuwa viongozi hao wanataka kuwapanga wafanyabiashara kutoka masoko mengine.



Alisema kuwa uamuzi huo si sahihi kwao kwa sababu eneo hilo la shimoni lina joto hivyo bidhaa zao zitaharibika mapema, lakini pia wakiwa kama wauzaji wa rejareja kwenda kukaa shimoni kulikojificha kutadhorotesha biashara zao.

Kiongozi wa Ulinzi na Usalama, Kambi Ramadhani, alisema juzi walitembelewa na Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Saad Mtambule, akazungumza na baadhi ya viongozi hao na wafanyabiashara ambao si sehemu ya eneo hilo kwa lengo la kuwapa vizimba katika eneo walilotakiwa kukaa wao, jambo ambalo wanaona si sawa.

"Mkuu wa wilaya kuja kimya kimya na kuzungumza na viongozi ambao muda wao umeshakwisha pamoja na watu ambao si sehemu ya eneo hili bila kutushirikisha si sawa," alisema.

Alisema jana asubuhi alikwenda kwa mkuu wa wilaya kumweleza kero hiyo na akawajibu kuwa wampe siku tatu ashughulikie kero hiyo. Katibu Msaidizi wa Soko, Michael Kidakule, alithibitisha kuwa ni kweli muda wao wa uongozi ulishakwisha na anaungana na wenzake kuwa kuna haja ya kufanya uchaguzi ili wapatikane viongozi wapya.

Alisema anashangazwa na kitendo cha mwenyekiti msaidizi kuwahamisha kundi hilo kwa madai kuwa wanataka wakae wauza nafaka pekee, kwani kufanya hivyo itakuwa ni matumizi mabaya ya soko lililojengwa kwa kodi za wananchi wakiwamo wafanyabiashara hao.

Mfanyabiashara wa viazi, Lucy Jeremia, alisema wakiwa kama wafanyabiashara wakongwe katika eneo hilo hawatokubali kuondolewa katika eneo hilo, ili awekwe mfanyabiashara ambaye hahusiki na soko hilo.

Alisema kuwa vurugu zilizofanywa jana ni sehemu ya kuomba msaada ngazi za juu kwa kuwa hawana imani na mkuu wa wilaya hiyo wakimtuhumu kushirikiana na baadhi ya waliokuwa viongozi wa soko kuwahujumu na kuleta watu wapya.

Mwenyekiti msaidizi wa soko hilo, Juma Kibwe alisema taarifa walizotoa wafanyabiashara hao sio za kweli kwani utaratibu wanaoupinga ndio uliokuwapo tangu awali.

"Kwa asilimia 100 hakuna mfanyabiashara mpya yoyote kutoka masoko ya nje aliyepewa nafasi pale, awamu ya kwanza tumeingiza wale ambao walipisha ujenzi na awamu ya pili ni wale walioomba nafasi," alisema.

Nipashe ilimtafuta Mkuu wa wilaya hiyo, Mtambule ambaye simu yake iliita bila kupokelewa, lakini alipatikana Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Manispaa ya Kinondoni, Aquilinus Shinduki ambaye aliahidi kutolea ufafanuzi wa jambo hilo leo.


## Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya epaper.ippmedia.com utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza "subscribe"
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa kadi ya benki malipo kwa mtandao wa simu unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa namba ya simu unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala.
Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. Kwa benki unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

6. Unafungua website yako ya www.ippmedia.com upande wa kulia utaona "E-Paper" utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

halotel

**TAARIFA KWA UMMA**

Viettel Tanzania PLC (Halotel) ni kampuni ya mawasiliano inayoendelea kuboresha huduma na kuvunja mipaka ya mawasiliano kwa wateja wetu kwa kutoa gharama nafuu kwenye SMS, Huduma za kupiga simu na Intaneti.

Tunapenda kuwatangazia wateja wetu na umma kwa ujumla juu ya gharama zetu za makato pindi mteja atakapokuwa hajajiunga kwenye kifurushi.

**GHARAMA ZA NDANI YA NCHI**

| Kipengele | Gharama |
|---|---|
| Kupiga Halotel kwenda Halotel | 10 Tsh/Dk |
| Kupiga Halotel kwenda mitandao mingine | 20 Tsh/Dk |
| Kutuma SMS | 5 Tsh/SMS |
| Data (MB) | 9.35 Tsh/MB |

**GHARAMA ZA NJE YA NCHI**

GHARAMA ZA KUPIGA SIMU NJE YA NCHI

| Kanda | Gharama (Tsh/Dk) |
|---|---|
| **Ukanda 1:** USA, UK, India, China, Canada, Australia, Japan, South Korea, Vietnam, Laos, Cambodia | 450 |
| **Ukanda 2:** Nchi nyingine za ULAYA, Kenya | 750 |
| **Ukanda 3:** Rwanda, Afrika Kusini, Zambia, UAE, Oman,Haiti, Peru | 840 |
| **Ukanda 4:** Cameroon, Zimbabwe, Malawi, Uganda, Congo DRC, Mozambique | 1,000 |
| **Ukanda 5:** Burundi | 1,350 |
| **Ukanda 6:** Sehemu nyingine duniani | 2,700 |
| **Ukanda 7:** Mitandao ya satelite | 13,800 |

GHARAMA ZA KUTUMA SMS NJE YA NCHI

| SMS | Gharama |
|---|---|
| SMS kwenda nje ya nchi | 95 Tsh/SMS |

| Aina ya kifurushi | Muda | Gharama (Tsh) | Mitadao Yote (Dk) | Halotel-Halotel (Dk) | SMS | Data (MB) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| VIFURUSHI VYA SAUTI | | | | | | |
| Dakika & SMS | Siku | 350 | 25 | | | |
| Dakika & SMS | Siku | 500 | | 110 | | |
| Dakika & SMS | Siku | 500 | 60 | | 60 | |
| Dakika & SMS | Siku | 1,000 | 180 | | 60 | |
| Dakika & SMS | Siku 2 | 1,000 | 160 | | 25 | |
| Dakika & SMS | Siku | 700 | 10 | Kila Dk 5 za mwanzo bure | | |
| Dakika & SMS | Wiki | 1,500 | 180 | | 150 | |
| Dakika & SMS | Wiki | 2,500 | 350 | 50 | 150 | |
| Dakika & SMS | Wiki | 3,000 | 450 | | 150 | |
| Dakika & SMS | Mwezi | 4,000 | 400 | 50 | 50 | |
| Dakika & SMS | Mwezi | 5,000 | 550 | 650 | 100 | |
| Dakika & SMS | Mwezi | 10,000 | 1,600 | 1,600 | 150 | |
| Dakika & SMS | Bila Kikomo | 500 | 20 | | | |
| VIFURUSHI VYA SMS | | | | | | |
| SMS | Siku | 100 | | | 200 | |
| SMS | Wiki | 500 | | | 2000 | |
| SMS | Mwezi | 1,000 | | | 10,000 | |
| VIFURUSHI VYA INTANETI | | | | | | |
| Intaneti | Siku | 350 | | | | 170 |
| Intaneti | Siku | 500 | | | | 246 |
| Intaneti | Siku | 1,000 | | | | 492 |
| Intaneti | Siku | 2,000 | | | | 985 |
| Intaneti | Siku 10 | 2,100 | | | | 1,024 |
| Intaneti | Wiki | 1,000 | | | | 492 |
| Intaneti | Wiki | 2,000 | | | | 985 |
| Intaneti | Wiki | 3,000 | | | | 1,475 |
| Intaneti | Wiki | 5,000 | | | | 2,460 |
| Intaneti | Wiki | 10,000 | | | | 4,925 |
| Intaneti | Mwezi | 10,000 | | | | 4,920 |
| Intaneti | Mwezi | 20,000 | | | | 9,850 |
| Intaneti | Mwezi | 30,000 | | | | 14,780 |
| Intaneti | Miezi 2 | 50,000 | | | | 24,600 |
| Intaneti | Bila Kikomo | 500 | | | | 200 |
| VIFURUSHI VYA COMBO | | | | | | |
| Combo | Siku | 500 | 15 | 10 | 5 | 200 |
| Combo | Siku | 1,000 | 60 | | 60 | 246 |
| Combo | Wiki | 2,000 | 55 | | 20 | 850 |
| Combo | Wiki | 2,500 | 20 | | 20 | 1,150 |
| Combo | Wiki | 3,000 | 100 | | 30 | 1,250 |
| Combo | Siku 10 | 3,100 | 150 | 20 | 300 | 1,024 |
| Combo | Mwezi | 10,000 | 280 | | 50 | 4,000 |
| Combo | Mwezi | 20,000 | 400 | | 100 | 8,500 |
| Combo | Mwezi | 50,000 | 600 | | 200 | 22,000 |


# Wafanyabiashara maduka wagomea kodi ya pango

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WAFANYABIASHARA wa maduka katika kituo kikuu cha mabasi ya mikoani mjini Moshi, mkoani Kilimanjaro, jana walifunga maduka kwa zaidi ya saa nne, wakishinikiza Halmashauri ya Manispaa kushusha kodi ya pango kama walivyoahidiwa hapo awali.

Mmoja wa wafanyabiashara hao Seif Rashid akizungumza na Nipashe alisema, awali walikubaliana kupunguziwa kodi kwa Sh. 50,000 katika bajeti ya 2024/25.

Filimoni Mallya alisema wamelazimika kufunga maduka kutokana na Manispaa ya Moshi kukiuka makubaliano ya kushusha kodi katika vibanda vya stendi kama walivyokubaliana awali.

"Licha ya kuahidiwa kupunguziwa kodi katika mwaka wa fedha wa 2024/25, hakuna jitihada zozote zilizofanywa na uongozi wa manispaa mpaka sasa. Wanachokifanya kwa sasa ni kutufungia vibanda vyetu, "alisema Zuena Yusuf

Wakati huo huo, wafanyabiashara hao walilalamikia juu ya uwepo wa machinga pembezoni mwa maduka yao wanaouza bidhaa kama zao kwa bei rahisi.

Mfanyabiashara Ester Mchau alisema: "Tunaiomba serikali kuwapanga machinga maeneo wanayopaswa kufanya biashara zao maana kwa sasa wanazidi kutuharibia biashara zetu kwa kuuza bidhaa zilizofana na zetu hii inazidi kudidimiza uchumi wetu."

Mwenyekiti wa wafanyabiashara hao, Frederick Makundi, alisema mgomo wa wafanyabiashara umesitishwa baada ya Manispaa ya Moshi kuahidi kusitisha oparesheni ya kufunga vibanda hivyo.

Baada ya mgomo huo, Mkuu wa Wilaya Moshi, Zephania Sumaye, alifika na kufanya kikao na wafanyabiashara hao.

Alisema wafanyabiashara hao walifunga maduka yao kwa takribani saa mbili wakishiniza kupunguziwa kodi ambayo kwa sasa ni 450,000 hadi 400,000.

"Nimefika hapa na kuzungumza na wafanyabiashara, tatizo lao lilikuwa ni dogo tu, ongezeko la kodi ambayo waliahidiwa itapungunzwa kwa mwaka wa fedha 2024/25.

"Sisi kama serikali tumeongea nao tumelichukua na tutalifanyia kazi pia tutaangalia kama kuna sababu ya kupunguza kutokana na 'Market price' na pia suala la kisheria,"alisema na kubainisha kuwa yako maeneo mengine ambayo vibanda kama hivyo hulipa 700,000 hadi 1,000,000.

Akizungumzia suala la uwepo wa wafanyabiashara wadogowadogo nje ya maduka ya wafanyabiashara Sumaye alisema kwa sasa hawezi kuwaondoa wafanyabiashara hao.

# Wahalifu ukatili wa watoto kutengwa

**Na Jenifer Gilla**

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Pindi Chana, amesema serikali inaweka utaratibu maalum wa kuwatambua wahalifu wa makosa ya unyanyasaji wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto ili watengwe wasiendelee kuleta madhara kwa kundi hilo.

Aliyasema hayo jana katika hafla ya uzinduzi wa Kituo cha Kutoa Huduma Jumuishi kwa manusura wa ukatili wa kijinsia na watoto katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Mwananyamala, Wilaya ya Kinondoni jijini Dar es Salaam.

Alisema watakitumia kituo hicho kuwatambua wahalifu wa unyanyasaji wa kijinsia, licha ya kuwachukulia hatua za kisheria hawataruhusiwa kutoa huduma katika maeneo kama vile katika shule za msingi na sekondari.

"Na wale wote ambao tunatambua kwamba ni wahalifu wa makosa ya kijinsia marufuku kupata huduma katika maeneo ya shule kuangalia watoto wetu na tutakwenda kuweka mikakati ya kuendelea kuwatambua," alisema.

Aliagiza elimu iendelee kutolewa kwa jamii ili isiwasamehe wala kusuluhisha migogoro inayotokana na makosa hayo, kwa kuwa ni lazima mkosaji achukuliwe hatua stahiki za kisheria ili kukomesha vitendo hivyo katika jamii.

Alisema maeneo mengi nchini watoto ni waathirika wa matukio ya kijinsia na wanaishia kupata huduma za hospitalini pekee, lakini kupitia kituo hicho watapata huduma za kisheria bure.

"Vituo hivi vina umuhimu na mchango mkubwa sana katika kuhakikisha waathirika wa vitendo vya ukatili wa kijinsia wanapata haki kwa wakati na kwa ufanisi mkubwa," alisema.

Alisema serikali inafanya mchakato wa kuongeza huduma ya kisheria katika vituo vingine kama hivyo kwenye mikoa na wilaya zote ili waathirika wasio na uwezo wa kulipia huduma ya sheria wapate msaada bure. Vitendo hivyo alisema ni janga linatokana na mila na desturi zilizopitwa na wakati na vimekuwa vikifanywa na watu katika ngazi za familia, majumbani, shuleni na kunahitajika nguvu ya pamoja ya wadau kukabiliana nayo.

Serikali inatambua waathirika wa mambo hayo kukabiliana na vizuizi vikubwa katika kupata haki ikiwamo ya kisheria, kijamii, kiuchumi kwa hiyo kituo hicho kitakuwa suluhisho la changamoto hiyo. Aliagiza kamati za ulinzi wa watoto katika ngazi ya vijiji vikutane na kujadili ajenda ya ulinzi wa watoto na wanawake na kutoa elimu kwa jamii namna ya kuwalinda.

Pia jamii iendelee kutoa taarifa ya vitendo vya ukatili ili kuvidhibiti na kuwakumbusha wanafamilia kutoficha vitendo vya unyanyasaji vinavyofanyika katika nyumba zao.

Balozi wa Ujerumani nchini, Thomas Terstegen, alisema anafurahi kuwa sehemu ya uanzishwaji kituo hicho ili kurahisisha kutoa za msingi kwa manusura wa unyanyasaji wa kijinsia na watoto.

Pia aliishukuru Wizara ya Katiba na Kisheria kwa kuonesha ushirikiano mzuri katika programu zao za upatikanaji wa haki, pamoja na ushirikiano kati ya Wizara ya Afya, Wizara ya Maendeleo, Jinsia, Wanawake, Makundi Maalum, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, na Jeshi la Polisi la Tanzania, na mamlaka za mikoa kwa kujitolea kupambana na ukatili wa kijinsia.

Mganga Mfawidhi hospitali hiyo, Saveli Benela, alisema kituo tangu kituo hicho kianzishwe mwaka 2019 idadi ya wanaonusurika imeongezeka kutoka 350 hadi 1,400 mwaka 2023.

RIPOTI MAALUM

# Uhaba wa walimu janga sugu la taifa

## • Uchakavu miundombinu ya shule za msingi bado tishio...



Shule ya Msingi Lituhi, Nyasa



Adolf Mkenda

**Na Halfani Chusi**

LICHA ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kutoa angalizo miaka saba iliyopita kuhusu hali ya rasilimali watu na miundombinu ya shule za msingi nchini, changamoto hiyo haijatatuliwa na serikali.

Kwa mujibu wa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohammed Mchengerwa, hivi sasa kuna uhaba wa walimu 271,028 kuanzia ngazi ya awali, msingi na sekondari.

Shule ya Msingi Lituhi, wilayani Nyasa, mkoani Ruvuma ina changamoto ambazo si tu zinakinzana na kanuni za afya, bali pia ni ukiukwaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014.

Shule hiyo ya Nyanda za Juu Kusini inayomilikiwa na serikali, hivi sasa ina jumla ya wanafunzi 888 wanaofundishwa na walimu saba walioajiriwa na serikali. Idadi hiyo ni sawa na uwiano wa mwalimu mmoja kwa wanafunzi 127.

Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2024 inaelekeza uwiano wa 1:45 (mwalimu mmoja kwa wanafunzi), hivyo Shule ya Msingi Lituhi yenye wanafunzi 888 inapaswa kuwa na walimu 20, hivyo kuwapo uhaba wa walimu 13 shuleni huko.

Kukiwa na shida hiyo, mwandishi wa habari hii aliyefunga safari ya Km 730 kutoka jijini Dar es Salaam hadi wilayani Nyasa, amebaini shule hiyo ina matundu 12 ya choo; sita ya wasichana na mengine ya idadi hiyo kwa ajili ya kaka zao. Kwa mujibu wa Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Nicolous Mahundi, wanafunzi wa kike shuleni kwake hivi sasa wako 468 na wa kiume ni 420.

Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 inaelekeza kila shule iwe na vyoo kwa ajili ya wanafunzi kwa uwiano wa tundu moja kwa wavulana 25 na tundu moja kwa wasichana 20, pia kuwe na vyoo kwa ajili ya walimu wao.

Hivyo, Shule ya Msingi Lituhi inapaswa kuwa na matundu 17 kwa ajili ya wavulana 420 na mengine 23 kwa ajili ya dada zao, yakifanya jumla ya mahitaji ya matundu ya vyoo shuleni huko kuwa 40. Kuna uhaba wa matundu 28.

Kukabiliana na uhaba wa walimu uliopo, Mwalimu Mkuu Mahundi anasema kuwa hivi sasa wanao walimu watatu wanaojitolea kwa miaka mitatu sasa, akiwataja ni Zawadi Hyera, Mikaela Mpangara, Efrem Chale.

Katika mazungumzo na mwandishi shuleni huko, mwalimu wa kujitolea Zawadi anasema, "Tunaiomba serikali itupe kipaumbele cha ajira kwa sababu tayari tumeshazoea mazingira na tupo tayari kufanya kazi hapa."

Mwalimu Mkuu Mahundi anasema kuwa mbali na uhaba wa matundu ya vyoo na walimu, shule hiyo pia inakabiliwa na upungufu wa madawati 90 na nyumba za walimu. Shule hiyo ina nyumba moja tu kwa ajili ya walimu.

Anasema changamoto hizo ni kikwazo kikubwa kwa ustawi wa taaluma shuleni huko, akiwa na ufafanuzi kwamba wanashindwa kutekeleza majukumu ya kitaaluma kwa ufanisi.

Mwalimu Mkuu huyo anasema uhaba wa walimu unasababishwa na mazingira ya kazi kutokuwa rafiki; walimu wakiripoti kituoni kwake huko, hawakai muda mrefu, wanaomba kuhama.

Akiwa kijijini Lituhi, iliko shule hiyo, mwandishi aliambiwa na wenyeji kuwa hawana huduma za kibenki; wanakijiji (wakiwamo walimu) wakihitaji fedha, hulazimika kusafiri umbali wa takriban Km 85 kwenda Mbamba Bay kupata huduma hizo, wakipita barabara ya vumbi.

Mwalimu Mkuu Mahundi anasema: "Kutokana na ubovu wa barabara, usafiri wa basi uliopo, gari likitoka hapa leo, linalala hukohuko mjini, linarejea kesho. Hii inaongeza gharama ya kulala katika nyumba za wageni kusubiri siku ya pili gari linaporejea. Huduma za mawasiliano ya simu nazo ni za kusuasua, hivyo walimu kufuata mshahara Mbamba Bay hakukwepeki.

"Nyumba ya walimu ipo moja tu, ninaitumia na familia yangu, walimu wengine wamepanga kijijini huko. Tuna changamoto mwalimu akistaafu, hatuletewi haraka wa kuziba pengo lake.

"Kwa miaka mitatu mfululizo wamestaafu walimu watatu kuanzia mwaka 2021 hadi 2023 bila kuwapo mbadala wao," anafafanua zaidi Mwalimu Mahundi na kubainisha kuwa changamoto hiyo inafahamika hadi kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ambaye amekuwa anazuru shuleni huko, akiahidi kuendelea kuisukuma serikali kuwapatia walimu wa kutosha.

> **"Kwa sasa tunakarabati yale (madawati) ya zamani lakini ni kweli kwamba kwa sasa wanafunzi wanabanana sana kwenye dawati, anasema ofisa huyo na kuthibitisha kuwapo uhaba mkubwa wa nyumba za walimu shuleni Lituhi kutokana na shule hiyo kutopangiwa bajeti ya ujenzi wa miundombinu hiyo.**

Hata alipotafutwa na mwandishi wa habari hizi, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa, Khalid Khalif kuzungumzia changamoto zinazokabili shule hiyo, alithibitisha kuwa na taarifa hizo, akiekeleza ufafanuzi zaidi utolewe na Ofisa Elimu wa Halmashauri.

Ofisa Elimu wa Awali na Msingi Halmashauri ya Nyasa, Benjamini Kusaga anasema wanaendelea na mipango ya kuboresha ujifunzaji na ufundishaji katika shule hiyo.

"Utaratibu wa ajira serikalini hivi sasa ni tofauti na wa zamani. Sasa unaletewa walimu wameshapangiwa vituo vya kazi tofauti na zamani ambapo mwalimu alikuwa anaambiwa aripoti kwa mkurugenzi, kisha kupangiwa kituo kulingana na mahitaji ya shule.

"Tumeshapeleka taarifa serikalini kuhusu uhaba wa walimu katika shule zetu, ikiwamo hiyo ya Lituhi, ninaamini tutaongezwa walimu wengine," anasema Ofisa Elimu Kusaga.

Kuhusu changamoto ya uhamisho wa mara kwa mara wa walimu wanaopangwa wilayani Nyasa, Ofisa Elimu huyo anasema: "Ni kweli hali ya mazingira ilivyo; ukosefu wa huduma za msingi, walimu wengi wamehama, wengine waliugua maradhi ambayo si rahisi kubaki huku. Inapofikia hatua hiyo, lazima ahamishwe."

Ofisa Elimu huyo pia anasema wanaendelea na ukarabati wa madawati yaliyoharibika na kutengeneza mengine mapya, akibainisha kuwa uhaba wa samani shuleni umesababishwa na mwitikio mkubwa wa wazazi na walezi kupeleka watoto shuleni kutokana na serikali kuondoa ada.

"Kwa sasa tunakarabati yale (madawati) ya zamani lakini ni kweli kwamba kwa sasa wanafunzi wanabanana sana kwenye dawati, anasema ofisa huyo na kuthibitisha kuwapo uhaba mkubwa wa nyumba za walimu shuleni Lituhi kutokana na shule hiyo kutopangiwa bajeti ya ujenzi wa miundombinu hiyo.

Ofisa Elimu Kusaga anasema changamoto hizo ni kikwazo kikubwa kwa ustawi wa elimu, akinyooshea kidole wanafunzi kupoteza vipindi vya masomo kutokana na kukosa walimu na hata wakati mwingine wanafunzi kulazimika kwenda shuleni mwishoni mwa wiki kufidia vipindi walivyokosa.

Si hayo tu. Kusaga ambaye kitaaluma ni mwalimu, anasema dosari hizo zimesababisha ufaulu wa shule hiyo kuwa chini, akitolea mfano darasa la saba mwaka jana, walitakiwa kufikia ufaulu wao ulikuwa wa wastani wa 78, ukiwa chini ya lengo la kitaifa la asilimia 85.

Kuhusu kutowaajiri walimu wanaojitolea shuleni Lituhi, Ofisa Elimu Kusaga anasema Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Nyasa ana taarifa za walimu hao na amekuwa anapendekeza waajiriwe.

**ITAENDELEA KESHO**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mazingira bora ndiyo njia pekee ya kuwezesha ustawi wa biashara

**RAIS** Samia Suluhu Hassan, juzi aliongoza Mkutano wa Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) jijini Dar es Salaam uliojumuisha sekta ya umma na binafsi ambao pamoja na mambo mengine, huangazia namna bora ya ufanyaji biashara kwa maendeleo ya nchi.

Mkutano huo kama ilivyo ada, wafanyabiashara hutoa dukuduku lao, vikiwamo vikwazo vinavyokwamisha ufanyaji biashara. Wafanyabiashara ndio walipaji wakubwa wa kodi ambazo ni chachu kubwa katika utekelezaji wa mipango ya serikali katika masuala ya maendeleo kwenye sekta mbalimbali kama vile afya, elimu, kilimo na maji.

Katika kuhakikisha hilo linafanikiwa katika mazingira ya sasa ya uchumi wa soko, sekta binafsi ndio mhimili mkubwa wa ukuaji wa uchumi, hivyo haina budi kupewa kipaumbele. Licha ya kwamba ni injini katika uchumi, kuwapo kwa ustawi katika sekta binafsi pia kunasaidia kwa kiwango kikubwa katika kupunguza tatizo la ajira hususani kwa vijana.

Akifungua mkutano huo pamoja na mambo mengine, Rais Samia alisema serikali imesikia kilio cha wafanyabiashara kuhusu kodi na katika kuhakikisha suala hilo linapatiwa ufumbuzi. Aidha, serikali itaunda kamati itakayopitia mifumo ya kodi ili kushughulikia malalamiko hayo. Rais alisema lengo ni kuwawekea wafanyabiashara mazingira mazuri katika ufanyaji wa shughuli zao na hatimaye kuchangia pato la taifa.

Wafanyabiashara nchini wamekuwa wakieleza vikwazo mbalimbali wanavyokutana navyo vikiwamo kubambikiwa kodi au mazingira yasiyo rafiki katika ulipaji wa kodi kutokana na mifumo iliyopo. Hatua hiyo imekuwa ikisababisha baadhi yao kufungiwa akaunti zao na kuchukuliwa fedha zao kwenye akaunti kwa sababu ya kutokulipa kodi na wengine kuamua kukwepa kodi.

Kwa kutambua vikwazo hivyo, Rais alikutana na kufanya kikao na baadhi yao ili kusikiliza changamoto zao, ambazo pamoja na mambo mengine, suala la kodi lilijitokeza kuwa ni tatizo kubwa kwao. Alisema hali hiyo imesababisha serikali kuunda kamati itakayopitia mfumo mzima wa ulipaji kodi ikiwamo utekelezwaji wa sera na sheria ili kuweka mazingira wezeshi kwa wafanyabiashara na hatimaye kunufaika na kufurahia shughuli wanazofanya.

Rais alionyesha bayana kwamba suala hilo ni kero ikiwamo katika utekelezaji wa falsafa ya 4R ili kufikia maendeleo ya kweli na ustawi wa taifa kwa kuwa

aliweka bayana kwamba baadhi ya changamoto zinatokana na baadhi ya watendaji wa serikali kutoelewa dhamira ya kuwezesha biashara na uwekezaji, stempu za kodi, na ucheleweshaji wa vibali.

Ni dhahiri kwamba ili taifa liendelee kustawi na kukua kiuchumi, sekta binafsi haiwezi kupuuzwa. Serikali inachopaswa kufanya ni kuweka mazingira bora ya ufanyaji biashara na kutoa miongozo, sheria na kanuni ili kufanikisha azma hiyo badala ya kuwa kikwazo.

Kuna msemo kwamba ili kumwezesha ng'ombe kutoa maziwa mfugaji hana budi kumwezesha kwa kumpa mashudu ya kutosha badala ya kumwadhibu kwa kumpiga mijeledi na kumnyima chakula. Ndivyo ilivyo kwa wafanyabiashara kwa kuwa ili walipe kodi ambazo ni tegemeo kubwa kwa serikali katika kuendesha shughuli zake, haina budi kuweka mazingira bora na rafiki kwa wafanyabiashara kufanya shughuli zao.

Katika falsafa ya 4R moja ya mambo yanayosisitizwa ni maridhiano, ili kuwawezesha wafanyabiashara kulipa kodi kwa mujibu wa sheria. Kama kuna jambo ambalo linasababisha kikwazo katika suala la kodi, ni vyema mamlaka zinazosimamia masuala ya mapato au kodi zikakaa na mfanyabiashara au mhusika na kukubaliana ikiwamo kupeana muda maalumu wa kulipa badala ya kuwapo mazingira yasiyo rafiki ya kufanya biashara.

Lengo la serikali na wafanyabiashara ni kufika kilele cha safari ya maendeleo, hivyo hakuna kuwekeana vikwazo kwa kuwa pande zote zina shabaha moja. Maridhiano pekee ndiyo njia bora ya kufanikisha azma ya serikali katika kuweka mazingira bora ya kufanya biashara na si kuwekeana chuki, vinyongo na kukomoana.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Mwandishi Wetu

# Vijana ni bomu hatari zaidi ya tabianchi

**TATIZO** la vijana kukosa ajira na wengi kushindwa kumudu maisha yao ni kitisho kipya Tanzania na barani Afrika.

Licha ya kuwapo na shida nyingine kubwa ambayo ni janga la mabadiliko ya tabianchi na uharibifu wa mazingira, kwa hakika, ikiwa vijana hawataweza kupata kazi na kufanikisha kujiajiri au kuajiriwa ni dhahiri kuwa yajayo ni mashaka matupu.

Kundi hilo lina hatari kubwa ya kuwa chanzo cha ukosefu wa amani, utulivu na maendeleo ya katika jamii nyingi.

Kwa mfano ukingalia mabadiliko ya tabianchi tayari imekuwa shida kubwa, lakini huwezi kuidhibiti kama vijana hawana chakula wala fedha mifukoni.

Ni vigumu kuwaambia wasiingie msituni kukata miti, kuuza mbao, mkaa, kuni au kutumia rasilimali hiyo kwa namna yoyote kama hawana mbadala wa kupata fedha wala chakula.

Ikumbukwe ni vigumu kuzungumzia ulinzi wa rasilimali kama vyanzo vya maji na mito kwa kukataza kuchimba mchanga na kulima kando ya mito kama vijana hao hawana cha kuwashughulisha.

Kwa upande wa samaki ndani ya mito na maziwa ni vigumu kulindwa kama vijana wataachwa kuishi na msongo wa mawazo kuwa kesho yao itakuwaje.

Kwa kifupi taifa litakuwa kwenye wasiwasi kama vijana ambao ni zaidi ya nusu ya raia wake watabakia hohehahe, ambao wanaweza kushiriki kila aina ya uhalifu.

Wanaleta hofu ya kuwa majambazi, wauaji, washiriki wa ngono za jinsia moja, magaidi, wabakaji, watumia dawa za kulevya, bangi, waporaji magari na abiria na kwa ujumla vijana wenye matatizo ya akili na wasio na utimamu kiafya.

Ni wakati wa kukabili janga hilo. Kwanza tatizo la ajira ni kubwa na serikali na sekta binafsi zichukue hatua ya kuwapatia vijana fursa zaidi za kupata kazi.

Wanapaswa kuwekeza katika programu za kuanzisha ajira lakini pia kutoa elimu na mafunzo yanayowapa vijana ujuzi unaohitajika kuingia katika soko la ajira au kujiajiri.

Serikali pia itoe fedha, vivutio, misamaha ya kodi kwa kampuni ili kuanzisha viwanda, kampuni na biashara ndogo na kubwa ambazo zitatoa nafasi mpya za kazi.

Lakini ijenge miundombinu kama maji, umeme vitolewe bure na barabara ili vitumike kwa wawekezaji wanaoweza kuzalisha ajira na kuendesha shughuli katika mazingira magumu.

Ufahamu hatari za matumizi mabaya ya dawa za kulevya ili kuzuia matumizi yake miongoni mwa vijana ni muhimu.

Ni lazima shule na vyuo vifanye programu za kuhamasisha kuelimisha vijana kuhusu madhara ya dawa za kulevya.

Wazazi wanapaswa pia kuzuia kikamilifu matumizi ya dawa za kulevya kwa kufuatilia shughuli na tabia za watoto wao.

Na serikali pia kusaidia na kufadhili mashirika yanayotoa huduma za ushauri nasaha na kurekebisha waathirika wa dawa za kulevya.

Ushauri na ukaribu kwa vijana zama hizi ni muhimu na kila mara ukaribu ulenge kuwaambia vijana kuwa serikali inawakumbuka na iko karibu nao.

Ikumbukwe kuwa kijana ni wakati wa kusisimua, kujaribu na kujiamini kupita kiasi. Ni vyema kuwa na mabaraza ya vijana ngazi ya vijijini na mijini kwa lengo la kukabiliana na hali hiyo.

Mabaraza haya yalelewe na wakuu wa wilaya, wa mikoa, viongozi wa dola kama wakuu wa polisi, magereza, mahakimu na hata viongozi wa vyama mbalimbali wakati huu.

Hatua hiyo itawaweka vijana karibu, kuwachunguza na kuwafuatilia ili wakuwa na kujifunza. Ikumbukwe ni rahisi kupotea katika ujana wenye changamoto nyingi unaowafanya wafikie utu uzima wa mapema kutokana na shida hasa umaskini na maradhi.

Katika mikutano ya ukaribu kwanza, vijana wafunzwe kuweka kipaumbele cha maisha na afya yao ya mwili na akili, ikimaanisha kuwa wajijali wenyewe kimwili, kihisia, na kiakili.

Wakumbushwe kufanya kazi halai ili wapate chakula wale vizuri, na wajifunze kutosheka na kutafuta zaidi mafanikio halali na si ya kiuhalifu.

Kadhalika, wasiogope kuzungumza na watu wazima wanaowaamini kuhusu masuala yoyote ambayo huenda yakakabili na kukwamisha maisha yao.

Viongozi wa dini wana nafasi muhimu kuzungumzia mambo ya imani, hofu na uaminifu kwa Mungu na kwa jamii inayowazunguka.

## Wanachama 200 ACT-Wazalendo watimkia CCM

**Na Gwamaka Alipipi,** LINDI

WANACHAMA zaidi ya 200 wa Chama cha ACT- Wazalendo wakiongozwa na Mwenyekiti wao Mkoa wa Lindi, Hamidu Bobali, wamejiunga na Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Wanachama hao walipokewa jana na Katibu Mkuu wa CCM, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, wakati akihutubia wanachama wa CCM na wananchi katika Uwanja wa Mpilipiki, mkoani Lindi.

Akizungumza katika mkutano huo kwa niaba ya wanachama hao, Bobali alisema sababu iliyowasukuma kuhamia CCM ni kazi nzuri iliyofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan katika uongozi wake, mkoani Lindi.

Alisema tangu alipohamia ACT- Wazalendo akitoka Chama cha Wananchi (CUF) amekuwa haoni maendeleo yoyote ndani ya chama hicho.

"Kwa miaka mitatu Rais Samia ameibadilisha Lindi, ameleta maendeleo katika sekta ya maji, kilimo, elimu pamoja na miundombinu. Sasa leo mimi na kundi langu tumeamua kumfuata (Samia), ili kumsaidia kuisukuma Lindi iwe na maendeleo," alisema Bobali.

Akizungumza katika mkutano huo baada ya kuwapokea wanachama hao, Balozi Dk. Nchimbi alisema kwa miaka mitatu ya uongozi wa Rais Samia, Lindi imefanikiwa kujenga hospitali nne, vituo vya afya 18 pamoja na zahanati 41.

Alisema katika sekta ya elimu serikali katika miaka mitatu imefanikiwa kujenga shule 54 za serikali na binafsi pamoja na kufanikisha kuandikisha idadi kubwa ya wanafunzi pamoja na kuongeza ufaulu.

Dk. Nchimbi alisema serikali itaendelea kutatua matatizo yanayowasibu wakazi wa Lindi, ikiwamo kulipa fidia kwa wakati wananchi wanaoathiriwa na wanyama hususani tembo.

Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM, Amos Makalla, aliwataka wananchi wa Lindi kutofanya makosa ya kuchagua viongozi wa upinzani kama walivyofanya katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2010 na 2015.

Alisema Jimbo la Lindi limekuwa likileta shida wakati wa uchaguzi kwa vyama vya upinzani kushinda kuanzia ngazi ya kata hadi jimbo.

Makalla alisema: "Katika uchaguzi wa mwaka 2010 kuna mtu aliongoza hapa Lindi anaitwa Baruani. Nikadhani CCM tumejisahau kidogo, lakini tulipofanya uchaguzi wa mwaka 2015 hali ikawa mbaya zaidi katika majimbo manane tulipoteza majimbo manne. Majimbo tuliyopoteza ni Kilwa yote Kusini na Kaskazini, tukapoteza Liwale pamoja na Mchinga."

Makalla alisema chama kilichokuwa kinashinda katika Jimbo la Lindi ni Chama cha Wananchi CUF, aliwataka wananchi wa Lindi kutorudia makosa waliyokuwa wanayafanya katika chaguzi zilizopita.

Kadhalika, aliwaagiza viongozi wa CCM mkoani Lindi kuhakikisha katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vitongoji na Kata, CCM inaibuka mshindi kwa kishindo.

Mbunge wa Lindi Mjini, Hamida Abdallah alimwomba Dk. Nchimbi kusaidia ujenzi wa Shule ya Sekondari Lindi iliyoungua moto miaka mitano iliyopita.

Alisema ameshawasiliana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), lakini bado hajapata majibu ya uhakika hivyo kupitia kwa Dk. Nchimbi anaamini jambo hilo linakwenda kutekelezwa kwa uharaka.

Katibu wa NEC, Idara ya Mambo ya Ndani ya Siasa na Uhusiano wa Kimataifa (SUKI), Rabia Abdallah Hamid, alisema Rais Samia amefanya mambo makubwa katika uongozi wake wa miaka mitatu.

Alisema Samia amefanikisha kupanda bei ya zao la ufuta pamoja na mbaazi, kwamba zao la korosho serikali imeshaweka mikakati kuhakikisha nalo linakuwa na bei nzuri kwa wakulima.




Mkurugenzi Mtendaji wa Watumishi Housing Investment (WHI), Dk. Fred Msemwa (kulia) na Mkurugenzi Mkuu wa Shandong H-Speed Dejian Group, Li Manchao wakionyesha mikataba baada ya kutiliana saini, jijini Dar es Salaam jana, makubaliano ya ujenzi wa mradi wa nyumba 101 za mkopo kwa watumishi wa umma zitakazojengwa katika eneo la Mikocheni. **PICHA: BEATRICE MOSES**

# Utafiti: Watoa huduma wa afya hukumbwa msongo wa mawazo

**Na Christina Mwakangale**

WATOA huduma za afya ngazi ya jamii (CHWs), wamebainika wengi wao hukumbwa na tatizo la afya ya akili ikiwamo msongo wa mawazo, wasiwasi na mfadhaiko, kutokana na changamoto wanazopitia wakati wakitoa huduma. Utafiti umebaini.

Vilevile madaktari, wauguzi na wafamasia hupitia changamoto kama hiyo, wakikosa huduma za kisaikolojia kwa dhana walinayo kwamba, wako salama na mganga hajigangi.

Prof. Tumbwene Mwansisya kutoka Chuo Kikuu Aga Khan, alisema hayo jana akiwasilisha matokeo ya utafiti uliowahusisha watu 1,700 wa sekta hiyo, uliofanywa mwaka huu katika mikoa sita, uliohusu 'Prevalence and Predictors of anxiety, depression and PTSD (Post traumatic stress disorder) among healthcare workers in Tanzania.'

Mdahalo ya kiafya kiutafiti hufanyika mara moja kwa mwezi, likiwa ni jukwaa linalokutanisha wataalamu tofauti wa afya ya akili ambao huzungumzia utafiti linaloandaliwa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) kupitia Jumuiya ya Afya ya Akili Tanzania 'Tanzania Mental Health Community of Practice (TMH-CoP)'.

Alisema kuna haja ya kuwa na mpango maalumu wa ushauri wa kisaikolojia kwa watoa huduma za afya katika sekta ya afya ili kuwapunguzia athari ambazo ni pamoja na kutoa huduma isivyo sahihi kwenye jamii na kuwa na lugha zisizofaa.

Alisema wafanyakazi wa afya huchukuliwa kama mti ambao huota na kuwa wa kijani unaovutia msimu na muda wote, ni kundi ambalo halitakiwi kuugua na hilo huwaathiri zaidi wafanyakazi hao.

Alisema CHWs ni ambao hufanya kazi kwa kujitolea na mara kadhaa huwa changamoto za ujira huku wakiwa miongoni mwa wanajamii wanaoishi mitaani na kushiriki matatizo yote, tofauti na daktari au muuguzi ambaye yupo eneo rasmi la kazi.

"CHWs anapokea lawama nyingi, akimfikisha mgonjwa hospitalini anaambiwa umemchelewesha, lakini pengine si wao. Ikumbukwe hawa wanajitolea, hawana mshahara wanasubiri ufadhili, wanakumbwa na hali ngumu mgonjwa wake aliyempambania kafariki, na yeye huyo huyo anashiriki mazishi. Ana mzigo mkubwa kichwani ni msongo.

"Mara nyingi huwa tunadhani tumei-control (dhibiti) afya kwa sababu tumo ndani ku-practice afya. Afya ya akili ni muhimu kwa sababu kinyume chake mtoa huduma anaweza kuwa na mawasiliano mabovu kwa wagonjwa na wenzake; kutoa dawa visivyo na kupoteza kujali.

"Utafiti mwingi unaonesha duniani wafanyakazi katika afya wapo kwenye tatizo la kisaikolojia kupata msongo na mengine ya afya ya akili. Lakini walio wengi hawajitafutii huduma za kiafya wao wenyewe. Mganga hajigangi.

"Na ngumu sana kutafuta msaada wanapopata changamoto hiyo, kwa sababu anaona yupo ndani ya sekta anakabiliana na tatizo. Utafiti tuliofanya tulimuweka katika hatua tatu."

Alisema utafiti huo ulifanyika mkoani Dar es Salaam na 'pilot' ikafanyika Mkoa wa Pwani na zoezi mkoani Dodoma, Tabora, Arusha na Mbeya, mikoa hiyo iliwakilisha kanda muhimu, huku washiriki wengi walikuwa ni wanawake na wastani umri miaka 39 wenye hatua ya elimu ya diploma, waliopo katika ndoa na asilimia 58 walikuwa wauguzi.

Prof. Mwansisya alisema washiriki hao walibainika kuwa na msongo wa mawazo, wasiwasi, mfadhaiko kutokana na kufanya kazi za kushtua, kuogofya. Wengi wa washiriki hufanya kazi zaidi ya saa nane na walitokea vituo vya umma na asilimia 73 walikuwa na bima za afya.

"Kundi la watoa huduma za afya ngazi ya jamii (CHWs), wamebainika ndio zaidi huwa tatizo la afya ya akili, wakiwa na msongo wa mawazo, ikilinganishwa na kundi lingine la watoa huduma katika sekta hii.

"Kundi linalofuata ni madaktari, wafamasia na watoa huduma za maabara, kisha wauguzi. Viwango vya utafiti vilipima maeneo tofauti kama vile, kiwango cha hali ya maisha, elimu, uzoefu kazini na kuwana uhakika wa kupata msaada huchangia kuongeza au kupunguza uwezekano wa kupata tatizo.

"Wafanyakazi wa afya ni asilimia 26 yaani asilimia tano zaidi ya takwimu za dunia katika msongo, wasiwasi. Hii husababisha kiwango cha tatizo la afya ya akili na kuchangia mawasiliano mabovu na kuleta kiwango duni cha kazi.

"Lakini kukosa tiba kisaikolojia inawasababishia zaidi watoa huduma hao katika sekta ya afya, kushindwa kutafuta msaada pale wanapokumbwa na tatizo kiafya wakiamini wao wako salama.

Watoa huduma za afya kuliko kundi lingine kwenye jamii kidunia na nchini, wanaathiriwa na tatizo hili, kutokana na kupitia magumu hususan hapa nchini CHWs kipindi cha Uviko-19 walikuwa na msongo mkubwa. Waliwachukua wagonjwa kwenye jamii na baadaye kuambiwa mgonjwa amefariki," alibainisha.

Prof. Mwansisya alisema kutokuwapo kwa mfumo rasmi wa kisaikolojia kutokana na kupitia changamoto kila siku katika matukio tofauti, ni tatizo.

"Mtu kuona mfanyakazi wa afya anapitia mengi kuona magumu na vifo, jamii inaona ni sehemu yako ya kazi wamezoea. Hii si kweli na haimaanishi kwamba wao hawapati tatizo kisaikolojia."

Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Wataalamu wa Afya ya Akili (MEHATA), Bingwa Mwandamizi wa Afya na Magonjwa ya Akili kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. Saidi Kuganda, akichangia mada alisema tatizo lililopo kwa wataalamu wa sekta hiyo, ni unyanyapaa miongoni mwao kwamba wao hawapatiti magumu yanayohitaji tiba kisaikolojia.

HABARI KITAIFA



Wafanyabishara wadogo maarufu machinga wakiwahudumia wateja wao huku wakiwa wamepanga bidhaa zao barabarani katika eneo la Manzese, Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Uchakavu wa majengo tishio kwa wanafunzi

**Na Godfrey Mushi,** HAI

UCHAKAVU wa majengo katika Shule ya Msingi Narumu Tela iliyoko Hai mkoani Kilimanjaro, unatishia usalama wa wanafunzi 250 wanaotumia majengo hayo huku darasa moja likianguka.

Wakati majengo yakiwa chakavu, walimu hawana vyoo, hivyo kulazimika kutumia nyumba za jirani na shule hiyo, jambo ambalo linalowafedhehesha.

Diwani wa Machame Narumu, John Lengai, aliyabainisha hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu hali ya shule hiyo na kutaka hatua za haraka kuchukuliwa kabla madhara hayajatokea.

"Kwanza hilo darasa lililoanguka ni miongoni mwa madarasa ambayo yalikuwa yamefungwa na Mhandisi wa Wilaya kutokana na ubovu wake. Kwa hiyo, kwa muda mrefu sasa tukawa tunafuatilia halmashauri kwa ajili ya kupambana na hilo tatizo.

"Hata hivyo, imekuja kuonekana kwamba pia kuanguka kwa hilo darasa kulitokana na kupita kwa tetemeko la ardhi Julai 22, mwaka huu. Basi mamlaka zinazohusika kwa maana ya Mhandisi wa Wilaya, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Hai na Ofisa Elimu Msingi tuliwafahamisha," alisema.

Alipotafutwa kuzungumzia hali hiyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Shule hiyo, Felician Kweka, alithibitisha kuwapo uchakavu wa majengo ya shule hiyo unaotishia usalama wa wanafunzi na walimu, huku akiiomba serikali kuharakisha ukarabati wa shule hiyo.

"Kutokana na hatari iliyopo kwa wanafunzi na walimu, ya baadhi ya madarasa kukatika nyufa na jingine kuanguka, tunaomba serikali itufikirie ili kupunguza hofu iliyopo," alibainisha mwenyekiti huyo.

Ofisa Elimu Msingi wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai, Husein Kitingi, alipoulizwa kuhusu taarifa ya kuanguka kwa darasa hilo kutokana na uchakavu wa miundombinu, alithibitisha huku akieleza kuwa mchakato wa ujenzi wake utafuata taratibu za serikali.

Kwa mujibu wa Kitingi, shule hiyo ni miongoni mwa shule 53 za wilaya hiyo zenye uchakavu wa miundombinu na kuhitaji hatua za haraka.

Mkazi wa Kijiji cha Narumu Tela, Isdori Mallya, aliiomba Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), kuangalia uwezekano wa kuijenga upya shule hiyo kutokana na madarasa yake yaliyobaki kuwa na nyufa.


**BODI YA KOROSHO TANZANIA**

**TANGAZO LA MKUTANO MKUU WA WADAU WA TASNIA YA KOROSHO MWAKA 2024**

Bodi ya Korosho Tanzania inapenda kuwaarifu Wadau wote wa Tasnia ya korosho nchini kuwa mkutano mkuu wa Wadau wa tasnia ya korosho utafanyika tarehe 22 na 23 Agosti mwaka 2024 kuanzia saa 2 kamili asubuhi katika ukumbi wa PSSSF Makole jijini Dodoma.

Mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Hussein M. Bashe (MB). Mada mbalimbali zinazohusu maendeleo ya tasnia ya korosho nchini zitawasilishwa na kujadiliwa.

Barua za mwaliko zimetumwa kwa Waalikwa wote. Waalikwa wanaombwa kujigharamia kuhudhuria mkutano huo kwa usafiri, malazi na gharama zingine. Bodi ya korosho itagharamia chakula na viburudisho wakati wa Mkutano.

Aidha, mkutano huu ni kwa wadau waliopata barua za mwaliko pekee. Kila mshiriki afike na barua yake ya mwaliko. Asiye na barua ya mwaliko hataruhusiwa kushiriki mkutano huo.

**Tangazo hili limetolewa na:**
**MKURUGENZI MKUU**
**BODI YA KOROSHO TANZANIA**
**S. L. P. BOX 533.**
**MTWARA**


# Bil. 613/- kunufaisha wakulima, wafugaji

**Na Maulid Mmbaga**

SERIKALI imeipatia Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) Sh. bilioni 613 kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wakulima, wafugaji na wavuvi wenye kipato cha chini ili waweze kulima kwa tija na kibiashara.

Hayo yalibainishwa jana mkoani Dar es Salaam na Mkurugenzi wa TADB, Frank Nyabundege, wakati akitoa taarifa ya mafanikio ya benki hiyo kwa miezi sita ya mwaka huu.

Alisema fedha hizo zimesaidia kupungua kwa riba ya mikopo ya kilimo katika taasisi zingine za kifedha kutoka asilimia 36 hadi 14, na kwamba hiyo imetokana na kuwa na kiongozi mwenye utashi wa kisiasa anayehakikisha Watanzania wanapata maendeleo.

Alisema wakati Rais Samia Suluhu Hassan anaingia madarakani mikopo chechefu ilikuwa zaidi ya asilimia saba na sasa imeshuka hadi tano.

Aidha, alieleza kuwa kupitia fedha hizo ulianzisha mfuko wa dhamana kwa wakulima wadogo ambao umewafikia wakulima, wavuvi na wafugaji takribani 23,659.

"Pia kuna vyama vya ushirika 475 ambavyo ndani yake vina wanufaika 772,104 idadi hiyo ukijumuishwa na wale wakulima waliopata mikopo mmoja mmoja mfuko unakuwa umewafikia wanufaika 795,763, kati yao asilimia 22.4 ni wanawake.

"Wanawake wamependelewa kwa sababu kwa miaka mingi wamekuwa hawanufaiki sana katika kuendeleza uchumi wa nchi yetu, lakini ukiangalia ndani katika familia tunazoishi ndio wamekuwa wakisimamia na kuhakikisha familia zinakuwa imara," alisema Nyabundege.

Aidha, alitoa wito kwa vijana kuhakikisha wanachangamkia fursa hiyo kwani asilimia 19 ya mikopo inayotolewa inaenda kwao, na kwamba kupitia mfuko huo wengi wamesaidika na kuinuka kimaisha.

"Nataka niwaombe Watanzania nendeni kwenye taasisi za kifedha, unataka kulima, kuvua na kufuga pata mtaji wakikuuliza dhamana waambie Rais Samia tayari ametoa, nendeni TADB mtazipata," alisema Nyabundege.

Aidha, alieleza kuwa Sh. bilioni 25 ambayo ni sehemu ya bilioni 613, zilielekezwa kwa wavuvi na kusaidia utoaji mikopo bila riba, ikiwamo ununuzi wa boti za kisasa 156, ambazo zimenufaisha watu 3213 kati ya hao 1,099 ni wanawake.

Alisema pia kuna utengenezaji wa vizimba na tayari 117 vimeshatolewa kwa wanufaika 674 kati yao 161 wakiwa wanawake, na kwamba fedha hizo zimewafikia na wakulima wa mwani na jongoo bahari ambao wanapatiwa mikopo kwa riba ya asilimia 0.00.

Hata hivyo, alieleza kuwa wamekuwa wakitoa fedha pia katika sekta ya kahawa na kwa sasa hakuna mkulima anayekopwa zao hilo tofauti na awali na kwamba eneo lingine ni zao la pamba ambako wamewasaidia wakulima kulima kisasa na kuinua ubora wa bidhaa hiyo kimataifa.

TANGAZO

# VISIONFUND TANZANIA MICROFINANCE BANK LTD

VisionFund TANZANIA MICROFINANCE BANK LTD

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

### Imetolewa chini ya kanuni ya 7 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

### WARAKA WA MIZANIA KWA TAREHE 30 JUNI 2024
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka ya sasa Tarehe 30/06/2024 | Robo ya Mwaka iliyopita Tarehe 31/03/2024 |
|---|---|---|---|
| | | TZS | TZS |
| **A.** | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 99 | 82 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | - | - |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | - | - |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 9,778 | 11,897 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushungulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima ya Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa Kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | | - | - |
| | Mikopo Halisi Iliyopo | 45,517 | 43,372 |
| 12 | Mali Nyingine | 3,180 | 2,729 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika ,Mitambo na Vifaa | 2,516 | 2,575 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **61,090** | **60,656** |
| | | - | - |
| **B.** | **DHIMA** | - | - |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | - | - |
| 18 | Amana za Wateja | 5,882 | 4,842 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | 2,459 | 3,257 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 10 | 12 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine | 77 | 77 |
| 27 | Zitakazolipwa Baadae | 3,875 | 4,941 |
| 28 | Dhima Nyingine | 22,508 | 22,508 |
| **29** | **Madeni** | **34,811** | **35,636** |
| | **JUMLA YA DHIMA** | - | - |
| **30** | **MALI/(DHIMA)HALISI (16 kutoka 29)** | **26,280** | **25,020** |
| | | - | - |
| **C.** | **FEDHA ZA WANAHISA** | - | - |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 21,200 | 21,200 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 2,737 | 1,824 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (2,119) | (2,119) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 863 | 525 |
| 35 | Akauti Nyingine za Mtaji | 3,599 | 3,589 |
| 36 | **Stahiki ya Wenyehisa Chache** | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISANI** | **26,280** | **25,020** |
| | | - | - |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | - | - |
| 39 | Mikopo Chechefu | **1,475** | **1,097** |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | **1,005** | **773** |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| | | - | - |
| **D.** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | - | - |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | **43%** | **41%** |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | **3.2%** | **2.5%** |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | **555%** | **541%** |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Hali na Mali | **76%** | **72%** |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | **84%** | **83%** |
| (vi) | Ongezeko la Amana | **3.0%** | **7.9%** |
| (vii) | Ongezeko la Mali | **0.7%** | **3.4%** |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 30 JUNI 2024
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa 30/06/2024 | Robo ya Mwaka Linganishi 30/06/2023 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30/06/2024 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 30/06/2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| | | TZS | TZS | TZS | TZS |
| 1 | Mapato ya Riba | 5,423 | 4,092 | 10,722 | 7,867 |
| 2 | Gharama za Riba | 1,097 | 356 | 2,134 | 625 |
| 3 | **Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2 )** | **4,326** | **3,737** | **8,588** | **7,242** |
| | | - | - | - | - |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (253) | **(131)** | (303) | **(307)** |
| | | - | - | - | - |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **1,562** | **1,046** | **3,119** | **1,984** |
| | | - | - | - | - |
| | 6.1 Faida/(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 73 | 164 | 146 | 205 |
| | 6.2 Ada za Kamisheni | 1,093 | 681 | 2,224 | 1,390 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 396 | 202 | 749 | 388 |
| | | - | - | - | - |
| 7 | **Gharama Zisizo na Riba :** | **5,297** | **3,921** | **10,541** | **7,923** |
| | | - | - | - | - |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 2,544 | 2,091 | 5,072 | 4,120 |
| | 7.2 Gharama Nyingine | 2,753 | 1,831 | 5,469 | 3,803 |
| | 7.3 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| | | - | - | - | - |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **337** | **730** | **863** | **996** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | - | - | - | - |
| 10 | **Faida /(Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **337** | **730** | **863** | **996** |
| | | 0 | - | - | - |
| 11 | Idadi ya Waajiriwa | **456** | **402** | **456** | **402** |
| 12 | Mapato kwa Hisa | 15,919 | 34,445 | 40,703 | 46,991 |
| 13 | Kipato kwa Hisa | 15,919 | 34,445 | 40,703 | 46,991 |
| 14 | Idadi ya Matawi | 1 | 1 | 1 | 1 |
| 15 | Vituo Vya Biashara | 35 | 35 | 35 | 35 |
| 16 | Vituo Vidogo | 12 | 12 | 12 | 12 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | - | - | - | - |
| (i) | Uwiano wa Mapato na Wastani wa Mali | 0.6% | 1.8% | 1.4% | 2.4% |
| (ii) | Uwiano wa Mapato na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 1.3% | 3.1% | 3.4% | 4.3% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 90% | 82% | 90% | 86% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani Wa Mali Zinazozalisha | **17%** | **21%** | **34%** | **41%** |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 30 JUNI 2024
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa Tarehe 30/06/2024 | Robo ya Mwaka iliyopita Tarehe 31/03/2024 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30/06/2024 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 30/06/2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| | | TZS | TZS | TZS | TZS |
| **I:** | **MTIRIRIKO WA FEDHA KUTOKANA NA SHUGHULI ZA UENDESHAJI** | | | | |
| | Mapato/(Hasara)Hakisi | **337** | **525** | **863** | **996** |
| | | - | - | - | - |
| | **Marekebisho kwa Ajili ya:** | - | - | - | - |
| | Hasara Katika Mali | 125 | 161 | 286 | 255 |
| | Badiliko Halisi Katika Mikopo | (2,145) | (2,505) | (4,650) | (5,060) |
| | Faida/Hasira Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana | 243 | 593 | 836 | 287 |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (451) | 439 | (11) | (421) |
| | Kodi Iliyolipwa | - | - | - | - |
| | Mengineyo | (1,067) | 1,025 | (43) | (1,078) |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | - | - | - | - |
| | **kwa shughuli za uendeshaji** | **(2,958)** | **238** | **(2,720)** | **(5,021)** |
| | | - | - | - | - |
| **II:** | **MTIRIRIKO WA FEDHA KUTIKANA NA SHUGHULI ZA UWEKEZAJI** | - | - | - | - |
| | Gawio Lililopokelewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (66) | (728) | (794) | (570) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika)** | - | - | - | - |
| | **kwa Shughuli za uekezaji** | **(66)** | (728) | (794) | (570) |
| | | - | - | - | - |
| **III:** | **MTIRIRIKO WA FEDHA KUTOKANA NA SHUGHULIZA KIFEDHA** | - | - | - | - |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | (17) | (17) | 4,632 |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | 913 | 287 | 1,199 | 1,146 |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| | Mengineyo | 9 | (422) | (413) | 351 |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika)** | - | - | - | - |
| | **kwa Shughuli za Kifedha** | **922** | **(153)** | **770** | **6,129** |
| | | - | - | - | - |
| **IV:** | **FEDHA TASLIMU NA MALI ZAINAZOFANANA NA FEDHA TASLIMU** | - | - | - | - |
| | Onzezeko/Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofana na Fedha Tastimu | (2,102) | (642) | (2,744) | 539 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 11,980 | 12,622 | 12,622 | 5,569 |
| | | - | - | - | - |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu /** | - | - | - | - |
| | **Mwishoni mwa Robo Mwaka** | **9,878** | **11,980** | **9,878** | **6,108** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA TAREHE 30 JUNI 2024
(Kiasi cha shilingi milioni)

| | Mtaji wa hisa | Mapato yaliyobakizwa | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| **Salio la mwanzo wa Mwaka (2024)** | **21,200** | **(1,646)** | **0** | **5,076** | **24,630** |
| Faida /(Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | **863** | - | - | **863** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | **2,737** | **(473)** | - | **(1,477)** | **787** |
| **Salio la mwisho wa Robo ya mwaka wa sasa** | **23,937** | **(1,256)** | **0** | **3,598** | **26,280** |
| | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwanzo wa Mwaka Uliopita ( 2023)** | **21,200** | **(2,418)** | **0** | **2,292** | **21,074** |
| Faida /(Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | **755** | - | - | **755** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | **17** | - | **2,784** | **2,801** |
| **Salio la mwisho wa mwaka Uliopita** | **21,200** | **(1,646)** | **0** | **5,076** | **24,630** |

### BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 30 JUNI 2024

Katika kuaandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zile zile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita.

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Chilala Hakooma(Ofisa Mtendaji Mkuu) | | 15 Julai 2024 |
| Rogathe Godson (Mkuu wa Fedha) | | 15 Julai 2024 |
| Albert Chikira (Mkaguzi mkuu wa Ndani) | | 15 Julai 2024 |

Sisi,tuliotajwa hapo chini,wajumbe wa bodi ya wakurugenzi,tunathibitisha usahihi wa taarifaza zahapo juu,Tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi,na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Athanasia Soka ( Mwenyekiti ya Bodi) | | 15 Julai 2024 |
| Jeff Mckrae (Mwendeshaji) | | 15 Julai 2024 |

### ADA NA GHARAMA ZA HUDUMA

| | Huduma za Kibenki | | Gharama-(Pamoja na VAT) |
|---|---|---|---|
| 1 | Kuangalia Salio-Dirishani & ATM | | 554 |
| 2 | Kuhamisha fedha | Ndani ya VFT hadi TZS1,000,000 | 944 |
| | | Ndani ya VFT zaidi ya TZS1,000,000 | 1,180 |
| | | Kwenda Benki nyingine hadi TZS10,000,000 | 3,554 |
| | | Kwenda Benki Nyingine zaidi ya TZS10,000,000 | 11,800 |
| 3 | Kutoa disrishani hadi/Kwakila TZS 5,000,000 | | 1,770 |
| 4 | Kutoa ATM | | 1,500 |
| 5 | Kadi ya ATM (Mpya au Kubadili) | | 5,000 |
| 6 | Gharama za mwezi (Monthly Acc maintanance fees) | Akiba Akaunti | 885 |
| | | Akaunti ya Biashara | 1,770 |
| 7 | Kufunga Akaunti | Akaunti ya Akiba, Watoto & Dunduliza | 2,360 |
| | | Akaunti ya Vikundi na Biashara | 5,900 |
| 8 | Taarifa ya Akaunti | Taarifa Fupi ATM | 720 |
| | | Miezi 0-1 | Bure |
| | | Miezi 1-3 | 1,180 |
| | | Miezi 3-12 | 3,540 |
| | | Miezi 12-24 | 11,800 |
| | | Miezi 24-48 | 29,500 |
| | | Miaka 3-6 | 41,300 |
| | | Zaidi ya miaka 6 | 55,400 |

| | Huduma Za Simu (Mobile banking) | Gharama-(Pamoja na VAT) |
|---|---|---|
| 9 | Kujua Salio-Simu | 118 |
| 10 | Kutoa-Simu | Bure |
| 11 | Kuhamisha Fedha-Simu | 118 |
| 12 | Taarifa Fupi-Simu | 354 |
| 13 | Kubadili Number ya Siri | 236 |

Akaunti

| s/n | Huduma | Kiwango cha chini | Riba Kwa mwaka * |
|---|---|---|---|
| 1 | Akiba Akaunti | 5,000 | 3% |
| 2 | Salary Akaunti | 5,000 | 3% |
| 3 | Kikundi Akaunti | 20,000 | 4% |
| 4 | Watoto Akaunti | 10,000 | 4% |
| 5 | Biashara Akaunti | 100,000 | 3% |
| 6 | Fixed Deposit Accounts | N/A | Kulingana na muda na Kiasi |
| 7 | Dunduliza Akaunti | 10,000 | 4% |

** Riba kwa akaunti za aina zote itajilimbikiza kwa kila la siku kwa kiasi cha akiba cha TZS100,000 na kuendelea na kulipwa kila Mwezi.*

Mikopo ya Vikundi

| | Aina ya Mkopo | Riba Kwa Mwezi (Kiima punguza) | Riba Kwa mwaka (Kiima punguza) | Gharama ya mkopo | Ada ya usimamizi wa Majanga |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mikopo ya Vikundi -Biashara group Loan | 5% | 60% | 3% | 1% |
| 2 | Mikopo ya Vikundi/Savings Group Loan | 5% | 60% | 2.5% | 0% |
| 3 | Mikopo ya Vikundi -Jiendeleze Group Loan | 4% | 48% | 3.1% | 1% |

Mikopo Binafsi

| | Aina ya Mkopo | Riba Kwa Mwezi (Kiima punguza) | Riba Kwa mwaka (Kiima punguza) | Gharama ya mkopo | Ada ya usimamizi wa Majanga |
|---|---|---|---|---|---|
| 4 | Mkopo Binafsi Na shule- hadi TZS10M | 4% | 48% | 2.5% | 1% |
| 5 | Mkopo Binafsi na shule inayozidi TZS10M Hadi TZS 20M | 3.50% | 42% | 2.5% | 1% |
| 6 | Mikopo Binafsi na shuke inayozidi TZS20M | 2.50% | 30% | 2.5% | 1% |
| 7 | Elimisha | 4% | 48% | 3.5% | 1% |

Mikopo ya Kilimo

| | Aina ya Mkopo | Riba Kwa Mwezi (Kiima punguza) | Riba Kwa mwaka (Kiima punguza) | Gharama ya mkopo | Ada ya usimamizi wa Majanga |
|---|---|---|---|---|---|
| 9 | Mikopo Binafsi -Jikomboe Loan | 4% | 48% | 4.0% | 1% |
| 10 | Mikopo ya kikundi -Jitume | 5% | 60% | 4.0% | 1% |
| 11 | Mikopo ya Kikundi -Mkombozi Loan | 5% | 60% | 4.0% | 1% |
| 12 | Patnerships | 3% | 36% | 3% | 1% |

| Name and Title | Signature | Date |
|---|---|---|
| Chilala Hakooma ( Chief Executive Officer) | Signed | 15-Jul-24 |
| Rogathe Godson (Chief Finance Officer) | Signed | 15-Jul-24 |
| Albert Chikira ( Internal Audit Manager) | Signed | 15-Jul-24 |



HABARI KANDA YA ZIWA

# Wadau wajenga nyumba kuwarahisishia kazi walimu

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WALIMU wa Shule ya Msingi Nyangaka, Kata ya Bugarama Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga, wameondokana na adha ya kutembea umbali wa kilometa 14 kwenda na kurudi shuleni, baada ya kujengewa nyumba ya kisasa na mdau wa maendeleo.

Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 katika suala namba 3(2)12 imebainisha katika elimu ya msingi kuwapo kwa upungufu wa asilimia 79 wa nyumba za walimu huku sekondari, kukiwa na upungufu wa asilimia 77 wa nyumba za walimu.

Sera hiyo katika kifungu namba 3(7)3 imeeleza jukumu la serikali kuimarisha ubia baina ya sekta ya umma na binafsi katika upatikanaji wa miundombinu ya kisasa na huduma mbalimbali katika ngazi zote za elimu na mafunzo.

Pia kuhakikisha kuna maabara za sayansi, karakana, madarasa, mabweni na nyumba za walimu pamoja na miundombinu mingine muhimu ya ustawi wa wanafunzi na walimu katika shule na vyuo.

Katika utekelezaji wa sera hiyo pamoja na kanuni ya uwajibikaji kwa jamii Kampuni ya Swala Solution inayofanyakazi katika Mgodi wa Barrick Bulyanhulu, imetekeleza mradi huo ili kukabiliana na adha wanapokumbana nazo walimu hao.

Akizungumza mwishoni mwa wiki wakati akikabidhiwa nyumba hiyo, Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Msalala, Najuka Sumeye alisema kupatikana kwa nyumba hiyo kutawasogeza walimu karibu na shule na kufundisha mpaka muda wa ziada ili kuongeza ufaulu.

"Shule hii ilikuwa na walimu saba na sasa wamebaki walimu wanne tu na wengi wameyakimbia mazingira ya kutembea umbali mrefu kuja hapa kufundisha," alisema Sumeye.

Mwakilishi wa kampuni hiyo, Raymond Warioba, alisema wamekuwa wakishirikiana na serikali katika kuboresha sekta ya afya na elimu kwa kuweka miondombinu rafiki kwa walimu na wanafunzi na lengo likiwa ni kuona mtoto anatimiza ndoto yake ya kielimu.

Akizungumza kwa niaba ya Meneja Mahusiano ya Jamii Mgodi wa Barrick Bulyanhulu, Marry Lupamba, alisema mgodi unaomkakati wa kushirikiana na kampuni yote yanayofanya kazi ndani ya mgodi kutekeleza miradi mbalimbali ya kijamii kwa ajili ya wananchi hasa wale wanaotoka vijiji 14 vinavyozunguka mgodi huo.

# Wahitimu wa chuo kikuu waanika ndoto kuwa na kampuni kubwa

**Na Vitus Audax,** MARA

VIJANA watano wahitimu wa chuo kikuu wanaounda kikundi cha vijana cha Eden Group katika Kijiji cha Muriba, Kata ya Muriba Halmashauri ya Wilaya ya Tarime wameeleza kuwa na ndoto ya kutoka kuwa kikundi na kumiliki kampuni kubwa ya uuzaji na usambazaji wa vifaa vya umeme wilayani hapa.

Katibu wa Eden Group, Amos Lameck, alieleza ndoto yao hiyo juzi wakati Mwenge wa Uhuru ulipokagua mradi wa kikundi hicho kilichokopeshwa Sh. milioni sita kupitia fedha za asilimia 10 za halmashauri mwaka 2023 baada ya kukamilisha taratibu zote za usajili 2022 na kurejesha zote kwa wakati.

Lameck alisema kikundi hicho chenye wanachama watano na kati yao wanne wakiume na mmoja wakike kinajishughulisha na biashara ya vifaa vya umeme wa majumbani na viwandani na mpaka sasa biashara yao ina mtaji wa Sh.milioni 7.2.

"Kwa sasa tayari tumefungua duka lingine katika Kijiji cha Gibaso, tumetoa ufadhili wa elimu kwa kijana mmoja kusomea Chuo cha Lubondo Biharamulo. Lengo kuu ni kuwa na kampuni kubwa ya uuzaji na usambazaji wa vifaa vya umeme wilayani hapa," alisema Lameck.

Akizungumza baada ya kukagua mradi wa vijana hao Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru, Godfrey Mzava aliwataka vijana kuachana na mambo yasiyo na tija na kujiunga na vikundi vya uzalishaji mali, ili viwasaidie kupata mikopo inayotolewa na serikali kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa itakayowasaidia kujiinua kiuchumi.

Aidha, Mzava aliwataka wakurugenzi wa halmashauri zote nchini kutoa kipaumbele cha mikopo kwa vikundi vinavyowahi kurejesha mikopo ya makundi ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu, ili waweze kuendelea kufanya shughuli za uzalishaji mali na kupunguza tatizo la ajira katika jamii.


twiga cement
Heidelberg Materials

**TANZANIA PORTLAND CEMENT PUBLIC LIMITED COMPANY**
**UNAUDITED RESULTS FOR THE PERIOD ENDED 30 JUNE 2024**

**CHAIRMAN'S STATEMENT**

The first half of the year presented a challenging market environment characterized by adverse weather conditions and projects on hold due to lack of funding. This translated into a market shrinkage compared to the previous year.

Overall, the company's revenue declined by 18% year-on-year. However, we have made substantial strides in operational efficiency, achieving positive outcomes in clinker incorporation, alternative fuel utilization, CO2 emissions and maintenance costs, among other areas.

Efficiency and process optimization played a vital role in efforts to optimize the costs to offset the decline in revenue. Our strong commitment to customer satisfaction and sustainability remains at the core of our business strategy.

**Prospects**

We are optimistic about market recovery in the coming months, weather conditions have softened, and projects should restart soon. Cost control will remain a priority in the coming months.

**Appreciation**

The Board would like to thank all its stakeholders for their support. We have every confidence that TPCPLC will continue to deliver value for the shareholders and community.

BY ORDER OF THE BOARD

Hakan Gurdal
**Chairman of the Board**

**STATEMENT OF PROFIT OR LOSS AND OTHER COMPREHENSIVE INCOME FOR THE PERIOD ENDED 30 JUNE 2024**

| | 2024 | 2023 |
|---|---|---|
| | TZS '000 | TZS '000 |
| Revenue from contracts with customers | 201,575,441 | 246,284,758 |
| Cost of sales | (152,530,052) | (166,235,904) |
| **Gross profit** | **49,045,389** | **80,048,854** |
| Other operating income | 428,958 | 295,793 |
| Selling and marketing costs | (1,701,687) | (1,468,800) |
| Administrative costs | (11,821,322) | (12,026,402) |
| Other operating expenses | (417,018) | (745,615) |
| Net gain on foreign currency translation | 7,253,225 | 4,752,475 |
| **Operating Profit** | **42,787,545** | **70,856,305** |
| Finance income | 1,458,743 | 1,481,873 |
| Finance costs | (436,623) | (308,890) |
| Finance income - net | **1,022,120** | **1,172,983** |
| **Profit before tax** | **43,809,665** | **72,029,288** |
| Income tax expense | (12,891,824) | (22,026,418) |
| **Profit for the year** | **30,917,841** | **50,002,870** |

**STATEMENT OF FINANCIAL POSITION AS AT 30 JUNE 2024**

| | 2024 | 2023 |
|---|---|---|
| | TZS '000 | TZS '000 |
| **ASSETS** | | |
| **Non-current assets** | | |
| Property, plant and equipment | 136,575,513 | 136,081,672 |
| Intangible assets | 842,665 | 797,217 |
| Leasehold land | 939,163 | 967,009 |
| Right of use assets | 171,005 | 2,669,129 |
| Other non-current financial assets | 649,000 | 728,000 |
| | **139,177,346** | **141,243,027** |
| **Current assets** | | |
| Inventories | 84,798,541 | 103,507,384 |
| Trade receivables | 62,031,569 | 60,698,079 |
| Other short-term operating receivables | 28,469,631 | 14,650,144 |
| Current income tax recoverable | 9,197,950 | 324,060 |
| Other current financial assets | - | 300,000 |
| Cash and bank balances | 96,861,416 | 72,379,452 |
| | **281,359,107** | **251,859,119** |
| **TOTAL ASSETS** | **420,536,453** | **393,102,146** |
| **EQUITY AND LIABILITIES** | | |
| **Equity** | | |
| Share capital | 3,598,462 | 3,598,462 |
| Retained earnings | 285,707,120 | 275,973,475 |
| | **289,305,582** | **279,571,937** |
| **Non-current liabilities** | | |
| Lease liabilities | 202,013 | 202,595 |
| Employment benefit obligations | 5,590,521 | 5,308,978 |
| Provision for quarry site restoration | 4,637,226 | 4,440,123 |
| Deferred income tax liability | 8,052,392 | 8,624,404 |
| | **18,482,152** | **18,576,100** |
| **Current liabilities** | | |
| Lease liabilities | 583 | 2,769,285 |
| Employment benefit obligations | 562,206 | 401,627 |
| Provision for quarry site restoration | 425,377 | 281,626 |
| Current income tax payable | - | - |
| Trade and other payables | 88,736,221 | 75,557,506 |
| Provisions | 10,583,245 | 13,049,775 |
| Dividend payable | 12,441,088 | 2,894,291 |
| | **112,748,719** | **94,954,110** |
| **TOTAL EQUITY AND LIABILITIES** | **420,536,453** | **393,102,146** |




Ukurasa 12

**Ni wakati 'wanasheria wasomi' wanapoanza kufanya jambo lao**



Ukurasa 13

ACT-Wazalendo na harakati mikoani kusaka wanachama wapya 'chapchapu'



Ukurasa 14

**KUJIUZULU KINANA**

**Kunavyoakisi ukomavu wa demokrasia ndani ya chama**

siasa
JUMATANO JULAI 31, 2024
Nipashe
HABARI BORA NA KAMILIFU

# Wanawake wapiganaji wanavyosimamia mageuzi kiutendaji tasnia ya habari

**Na Jenifer Gilla**

MIAKA ya 1980 vyombo vya habari nchini viliongozwa na wanaume. Hali hiyo iliathiri utendaji kazi wa wanawake ndani ya taasisi hizo na pia maudhui yaliyochapishwa yalikuwa ya kisiasa, uchumi na burudani.

Aidha, ilisababisha masuala ya kijamii, taarifa za wanawake, mgawanyo wa majukumu, haki, usawa na haki za binadamu na wanawake kutopewa kipaumbele katika vyombo vya habari.

Upungufu huo ukawa mwanzo wa vuguvugu la kukemea udhalilishaji wanawake na watoto wa kike, harakati za kutaka wanawake wapate nafasi za juu za uongozi.Taasisi mbalimbali kama Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) na Wan-Infra Women In News zikaanza harakati za ukombozi.

Utafiti unaofanywa na Baraza la Habari Tanzania (MCT) kuchunguza usawa wa jinsia kwenye vyombo vya habari nchini mwaka 2019 ulionesha kuwa wanawake walikuwa asilimia 21 ya nafasi za juu za uongozi na asilimia 20 katika nafasi za kati.

Mwandishi wa habari mkongwe na mwasisi TAMWA, Pili Mtambalike, anazungumzia hali ya wanawake na changamoto za miaka ya 1980.

Anasema alipokuwa kazini miaka ya 1980 kulikuwa na idadi ndogo wa wanawake hasa kwenye magazeti, tatizo likianzia vyuoni.

"Sisi tuliosoma Chuo cha Uandishi wa Habari Tanzania (TSJ), kwenye darasa la wanafunzi 30 wanawake tulikuwa watano. Huo ulikuwa tayari ni upungufu, kwa maana kuwa waliokwenda kwenye vyombo vya habari ni wachache pia," anaongeza.

Alipotoka chuoni na kujiunga na Shirika la Habari Tanzania SHIHATA, Dar es Salaam, kati ya



Mshindi wa Tuzo ya Mwanamke Kiongozi katika Chombo cha Habari 2024, Mhariri Mtendaji wa Nipashe Beatrice Bandawe (katikati), akipongezwa na wadau wa habari baada ya ushindi. Kulia ni Mwenyekiti wa TAMWA, Joyce Shebe na mwandishi mbobezi, Dk. Joyce Bazira. **PICHA: MWANDISHI WETU**

waandishi 40 waliokuwapo, wanawake hawakuzidi 10.

Anasema kuwapo wa wanaume wengi kwenye vyombo vya habari kuliongeza ugumu kwani iliwabidi wafanye kazi mara 10 zaidi ili wapangiwe majukumu kulingana na uwezo wao, kinyume na hapo walipangiwa kazi tofauti mfano kupokea simu za waandishi wanaotuma habari kutoka mikoani.

Hali hiyo ilichangia wanawake kupitia unyanyasaji wa kijinsia kwa sababu viongozi walikuwa wanatumia udhaifu huo kama fimbo kuwachapa ikiwamo kuomba rushwa ya ngono.

Pili anasema changamoto hiyo pia ilisababisha habari zinazohusu wanawake, watoto na makundi maalum kuwa chache hali iliyowasukuma kuanzisha TAMWA ili kuongeza wigo wa kuandika taarifa hizo, jambo lililochukua muda mrefu kufanikiwa.

"Lakini tunashukuru, tuliwapa mbinu za kupambana na mfumo dume na kuchukua nafasi za juu za uongozi, ikiwamo kutoa mikopo ya kujiendeleza kielimu ili kuondoa vikwazo vya kufikia nafasi hizo na sasa tunaona kuna viongozi wanawake katika nafasi hizo kwenye tasnia ya habari," anasema Pili.

Kuanzia 2010 waandishi habari wanawake walianza kujitokeza kwa wingi kuwania nafasi za juu za uongozi katika vyombo hivyo, na wale waliofanikiwa kushika nyadhifa hizo walifanya mapinduzi na kuleta mabadiliko chanya.

## SAFARI NGUMU

Safari za wanawake kufikia nafasi za uongozi haikuwa rahisi, Mhariri Mtendaji wa Nipashe, Beatrice Bandawe, anakumbusha.

Anaeleza kuwa alipoanza kuandika habari mwaka 1989, kazi zilipangwa kwa kupendelea wanaume.

Anaeleza kuwa alikabiliana na hali hiyo kwa kuingia mtaani na kutafuta habari badala ya kusubiri kutumwa au kupangiwa.

Beatrice anasema alijituma kuandika habari zenye ubora kuliko hata zile walizotumwa na wahariri, hali iliyomfanya kuaminika na kupewa majukumu sawa na wanaume.

Baadaye alipewa kazi ya kupitia habari za waandishi wengine kisha uhariri wa habari mwaka 2008 na baadaye uhariri wa kijarida cha habari za mikoani.

"Wanaume wanapangiwa kuripoti habari kubwa na ngumu kama za siasa, za uchunguzi, bunge, lakini wanawake tunapangiwa kuandika habari nyepesi zinazohusu masuala ya afya na wanawake.

"Lakini mimi nilikuwa naingia mtaani natafuta wanasiasa nawahoji naandika habari nzuri na zikawa zinapendwa," anaongeza.

Anaeleza kuwa baada ya kupandishwa cheo alipitia vita ya kudharaulika kutoka kwa waandishi aliowasimamia, lakini alisimama kama kiongozi bila kutetereka mpaka walipozoea na kukubali kuwepo kwake katika nafasi hiyo.

Ili kuongeza ufanisi katika majukumu yake, Beatrice alijiendeleza kielimu kwa kusoma kozi mbalimbali ikiwamo ya uongozi inayotolewa na Shirika la Women in News ambazo zilimwongezea ari ya utendaji wa kazi na kujiamini.

Kutokana na jitihada katika kazi, mwaka 2018 aliteuliwa kuwa Mhariri Mtendaji wa Nipashe na anakiri kuwa mambo yalikuwa magumu zaidi kwani kipindi hicho hali ya uandishi ilikuwa ngumu kutokana na vyombo vya habari kutokuwa na uhuru wa kuandika taarifa za uchunguzi hasa zinazogusa serikali.

"Nilipopewa barua ya kuwa mhariri mtendaji nilijiuliza, nitaweza kweli kumudu hii nafasi? Kuna vyeo vingine unapopewa unafurahia, lakini hiki sikuwa na furaha.

"Ni kwasababu nilijua niko katika wakati mgumu na ninaweza kupoteza kazi wakati wowote kama nisipokuwa makini. Lakini ilikuwa tofauti, nilipata ushirikiano mzuri kwa timu yangu na kufanya kazi kuwa rahisi," anasema.

INAENDELEA UK. 13

UCHAGUZI RAIS TLS

# Ni wakati 'wanasheria wasomi' wanapoanza kufanya jambo lao



BONIFACE A.K. MWABUKUSI | EMMANUEL AUGUSTINO MUGA | CAPT. IBRAHIM MBIU BENDERA | PAUL REVOCATUS KAUNDA | REVOCATUS LUBIGILI KIBWE KUULI | SWEETBERT NKUBA

**Na Elizabeth Zaya**

UNAWEZA kusema ile siku imewadia. Ni mwaka mwingine wa uchaguzi ndani ya taasisi kongwe ya Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), kilichoanzishwa mwaka 1954.

Kwa miaka kadhaa sasa uchaguzi ndani ya chama hicho umekuwa wa kiushindani kutokana na kushirikisha magwiji wa taaluma ya sheria wa nchi hii.

Na kuanzia kesho hadi Jumamosi jijini Dodoma, kura ya ndani ya boksi itaamua nani awe rais mpya wa TLS, atakayemrithi Harold Sungusia.

Pamoja na kwamba uchaguzi huo unafanyika katika nafasi mbalimbali, lakini ngazi ya urais ndiyo yenye ushindani mkubwa kuliko nyingine.

Imekuwa ikishuhudiwa 'vitimbwi vya hapa na pale inapofika uchaguzi huo ambao hufanyika kila mwaka licha ya kwamba katiba ya chama hicho inaruhusu mgombea katika nafasi mbalimbali ndani ya chama hicho kugombea mara tatu mfululizo yaani miaka mitatu na akibahatika kushinda zote anaongoza kwa miaka hiyo yote mitatu.

Lakini, baadhi ya wagombea au viongozi waliowahi kushika nafasi hususani ya urais baada ya kushinda na kuongoza kwa mwaka mmoja hawatamani tena kugombea ili wapewe ridhaa ya kuendelea tena. Baadhi yao ni Harold Sungusia, Fatma Karume, pamoja na Dk.Edward Hosea ambao baada ya kuitumikia TLS kwa mwaka mmoja hawakutaka tena kurejea ofisini kwa mara nyingine.

Baadhi ya wanataaluma ambao ni wanachama wa TLS wanasema kuongoza wabobezi hao wa tasnia ya sheria kwa zaidi ya mwaka mmoja ni lazima uwe 'mwamba'.

Kama ilivyokuwa kwa miaka mingine iliyopita, uchaguzi wa mwaka huu nao umekuwa na 'purukushani' za hapa na pale ikiwamo mmoja wa wagombea wa urais Boniface Mwabukusi kuenguliwa na baadaye kurejeshwa na mahakama.

"Baadhi ya wanataaluma ambao ni wanachama wa TLS wanasema kuongoza wabobezi hao wa tasnia ya sheria kwa zaidi ya mwaka mmoja ni lazima uwe 'mwamba'.

Mbali na Mwabukusi, wagombea wengine katika kinyang'anyiro hicho ni Sweetbert Nkuba, Revocatus Kuuli, Paul Kaunda, Emmanuel Muga na Kapteni Ibrahim Bendera.

### WANAYOSEMA WAGOMBEA

Baadhi ya wagombea hao wanazungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam, kueleza misimamo yao, Emmanuel Muga, akifungua pazia.

Muga mbali na taaluma ya sheria ni mwandishi wa habari ambaye amefanya kazi kwenye tasnia hiyo kwa zaidi ya miaka 10 kwenye vyombo tofauti vya habari vya ndani na nje ya nchi wakati kazi ya uwakili nayo mpaka sasa amefanya kwa zaidi ya muongo mmoja tangu mwaka 2012. Muga anasema aliwahi kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mawakili TLS Mkoa wa Dar es Salaam mwaka 2019 hadi 2021.

Anaeleza kuwa anagombea nafasi hiyo akiamini anatosha na akiahidi kusimamia malengo maalumu kuleta maendeleo ndani ya chama hicho ikiwamo kuisaidia serikali, mahakama, wananchi na wanachama wa TLS.

Mgombea mwingine ni Sweetbert Nkuba, ambaye anasema anakwenda kuleta mabadiliko ndani ya chama hicho na moja ya mipango yake ni kuboresha miundombinu ya TLS, kuimarisha sheria na kutumia teknolojia.

Anaeleza kuwa analenga kuwezesha huduma bora kwa wanachama na jamii hususani kuongeza uwekezaji katika mifumo ya kidijitali ili kurahisisha kupatikana taarifa na huduma za kisheria na kuboresha ofisi za TLS katika mikoa mbalimbali kwa vifaa vya kisasa na miundombinu bora.

Jambo jingine anasema ni kusisitiza mafunzo endelevu kwa wanachama wa TLS ili wawe na ujuzi wa kisasa na uwezo wa kushindana kimataifa.

Aidha, hilo linajumuisha kuanzisha programu za mafunzo ya mara kwa mara kuhusu sheria mpya na mabadiliko ya sheria pamoja na kushirikiana na taasisi za kimataifa kwa mafunzo na kubadilishana uzoefu.

Anaahidi kuwa ataifanya TLS iwe na sauti yenye nguvu katika masuala ya kitaifa na kimataifa yanayohusu sheria na haki ikiwamo kuanzisha mikakati ya ushawishi kwa serikali na bunge ili kuboresha mfumo wa sheria na kutoa msaada wa kisheria kwa jamii, hususani makundi yenye uhitaji maalum.

Jambo jingine analosema ni kusimamia kwa uwazi na uwajibikaji shughuli za TLS ili kujenga imani kwa wanachama na wadau wengine ikiwamo kuboresha mifumo ya ukaguzi wa ndani na nje ili kuhakikisha matumizi sahihi ya rasilimali zake. Anasema pia ataanzisha utaratibu wa kutoa taarifa za mara kwa mara kwa wanachama kuhusu shughuli na matumizi ya fedha za taasisi hiyo.

Kadhalika, atajenga na kuimarisha uhusiano na wadau mbalimbali, hasa serikali, mashirika ya kiraia na taasisi za kimataifa pamoja na kuanzisha na kudumisha ushirikiano na mashirika ya kimataifa ya kisheria kwa manufaa ya wanachama wa TLS.

Anaahidi pia kushirikiana na vyuo vikuu na taasisi za elimu ya juu katika kutoa elimu ya sheria na mafunzo ya vitendo kwa wanataaluma.

Kadhalika, Nkuba anasema akichaguliwa kuwa rais wa TLS, ataanzisha mfuko wa malipo ya ada ya mwaka kwa unafuu na kusimamia vituo vya malezi kwa mawakili wapya, pamoja na upatikanaji wa bima ya afya kwa utaratibu wa kulipa kidogo kidogo.

Mgombea mwingine Paul Kaunda, anayejinadi kuwa si mgeni kwenye uongozi kwani amefanyakazi kwa miaka 10 katika maeneo mbalimbali ya sheria hasa sheria za jinai na madai na ni mdau mkubwa wa matumizi ya teknolojia ya akili bandia (AI).

Anasema pia si mgeni wa kuongoza taasisi kama TLS kwani 2019 hadi 2020 alikuwa mjumbe wa Baraza la Uongozi na wa Kamati ya Sheria na Katiba ya TLS kwa miaka mitano.

Kapteni Ibrahim Bendera anasema anajinadi akisema amekuwa wakili kwa miaka 18 Bara na 19 Zanzibar hivyo amejipima na kuona anatosha kuongoza chama hicho hasa wakati huu ambapo rais wa chama hicho ataongoza kwa miaka mitatu badala ya mwaka mmoja.

Aanasema kwa mwaka TLS yenye wanachama 12,000 inapata wastani wa bilioni 1.2 na inalipa mishahara inayofikia Sh.milioni 80 kwa mwezi hivyo akichaguliwa atapunguza gharama za matumizi na kuwawekea mazingira mazuri mawakili vijana waweze kupata uzoefu. Revocatus Kuuli, anasema amekuwa wakili kwa miaka 13 Tanzania Bara na Zanzibar kwa miaka minne na kwamba katika mawakili 13 waliosajiliwa na Mahakama ya Afrika iliyoko Arusha ni miongoni mwao.

Boniface Mwabukuzi anajinadi akisema anataka nafasi hiyo ili kuleta mageuzi ambayo kwa muda mrefu yameshindikana ikiwamo kupambana na mafisadi ndani na nje ya TLS.

Kwa muda mrefu TLS imeshindwa kutimiza wajibu wake wa kusaidia wanachama kutokana na watu wanaochaguliwa kuiogopa serikali hali ambayo iliwafanya washindwe kusimamia misingi ya kuanzishwa kwake, anasema.

# ACT-Wazalendo na harakati mikoani kusaka wanachama wapya 'chapchapu'

**Na Sabato Kasika**



Kiongozi wa Chama cha ACT-Wazalendo, Dorothy Semu, akihutubia moja ya mikutano yake inayoendelea mikoani. **NA MPIGAPICHA WETU**

VIONGOZI wakuu wa Chama cha ACT- Wazalendo, wameanza kupiga baragumu (tarumbeta) nchi nzima, kukusanya wanachama wapya milioni 10 kwa miezi michache kabla ya uchaguzi mkuu mwakani.

Wanajinasibu kuwa mkakati wa kuzunguka mikoa mbalimbali kusaka wanachama ndani ya miezi 10, ni mtaji utakaowafanikisha kupata ushindi kwenye uchaguzi mkuu wa 2025.

Kiongozi Mkuu wa chama hicho, Dorothy Semu, anaiambia Nipashe kuwa wanachama hao milioni 10 wanaosakwa kwa kipindi hicho, ni silaha ya ushindi ya ACT-Wazalendo katika kujiimarisha na kujijenga kisiasa.

Akizungumza na gazeti hili kutoka mkoani Singida, Dorothy anasema, chama kimeanza awamu ya kwanza ya kampeni ya kusajili wanachama milioni 10 katika kipindi cha miezi 10.

Anafafanua kuwa kipindi hicho kimeanza Julai, na kwamba kitaendelea hadi Aprili mwaka 2025 wakiwa wamefikia mikoa 22 yenye majimbo 125 kati ya majimbo 214 ya Tanzania Bara.

"Chama chetu kimeamua kufanya kampeni ya kusajili wanachama katika mfumo wa kisasa tunauita 'ACT Kiganjani', lengo ni kushiriki uchaguzi wa serikali za mitaa na kushinda," anasema Dorothy.

Kiongozi huyo anafafanua kuwa ushindi huo ndio ambao utakiwezesha chama hicho kuendelea kupata ushindi wa kishindo katika uchaguzi mkuu wa 2025, kwa kuwa kitakuwa na mtaji wa kutosha.

"Tumejipangia kwamba Septemba tuanze awamu ya pili ya kampeni ambayo itafikia majimbo 89 yaliyobakia ili kabla ya uchaguzi wa serikali za mitaa tuwe tumefikia majimbo yote 214 ya Tanzania Bara," anasema.

Anasema, wanachama wa chama cha siasa ndio mtaji wa kwanza wa chama, na kwamba kama chama hakina wanachama kinakuwa mfu, na kuongeza kuwa ACT-Wazalendo hakitaki kuwa chama mfu.

"Watanzania wanataka mabadiliko ya uongozi, wamekuwa wakiumizwa na gharama kubwa za maisha na umaskini, ukosefu wa ajira, fursa na huduma mbovu za jamii. Ninaamini watatuunga mkono," anasema.

## WAKITINGA MIKOANI

Naibu Katibu wa Habari, Uenezi na Uhusiano wa Umma wa chama hicho, Shangwe Ayo, anafafanua kuwa, Kiongozi Mkuu wa chama hicho, Dorothy na kundi lake yupo katika majimbo 30 kwenye mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Dodoma, Singida na Manyara.

"Makamu Mwenyekiti Bara, Isihaka Mchinjita, ana ziara katika mjimbo 28 kwenye mikoa ya Ruvuma, Mkoa wa Kichama wa Selous, Mtwara, Lindi, Pwani na Tanga," anasema Shangwe.

Shangwe anasema, Katibu Mkuu Ado Shaibu anazungukia majimbo 21 katika mikoa ya Mwanza, Simiyu, Mara, Geita na Kagera, akiendelea na 'msako' wa wanachama wapya milioni 10.

Naibu Katibu wa Habari, Uenezi na Mahusiano na Umma anaeleza, Kiongozi Mkuu mstaafu Zitto Kabwe ana ziara kwenye majimbo 36 katika mikoa ya Kigoma, Rukwa, Katavi, Tabora, mkoa wa Kichama Kahama mkoani Shinyanga.

"Kwa ujumla ni kwamba, viongozi wetu watawahamasisha Watanzania kujiandikisha katika daftari la kudumu la wapigakura, lakini kuwahamasisha kushiriki uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi Mkuu 2025 ili wakipe chama chetu ushindi," anasema.

Anaongeza kuwa, viongozi hao pia wanasikiliza kero mbalimbali za wananchi za kiuchumi, kijamii na kisiasa, kuzipazia sauti na kuendelea kuinadi ahadi ya chama ya kujenga taifa la wote kwa maslahi ya wote.

"Kimsingi, wananchi wanataka kuona wanamudu maisha yao kwa kuweza kugharamia mahitaji yao ya msingi, kupata fursa ya ajira, kazi na kufanya shughuli za kujipatia kipato bila vikwazo," anasema.

## KUONDOA MATABAKA

Makamu Mwenyekiti ACT-Wazalendo Bara, Isihaka Mchinjita anasema, katika kampeni hiyo chama chao kinalenga kuunganisha Watanzania na kujenga taifa la wote kwa maslahi ya umma.

"Tunataka taifa ambalo serikali itahakikisha sera za uchumi zinapunguza gharama za maisha ya wananchi wote, ili mmoja aweze kumudu na kuendeleza naisha yake, hii ndio maana yetu ya kuunganisha Watanzania," anasema.

Anafafanua kuwa matabaka yaliyopo ya walionacho na wasiokuwa yanasababishwa na CCM, kwa maelezo kwamba inakumbatia rushwa na kusababisha umaskini kwa Watanzania wengi.

"Wananchi wanapaswa kujiunga na vuguvugu hili, kwa ajili ya kuikomboa nchi kutoka katika mikono ya chama tawala ambacho kinakumbatia watu wachache na kusababisha kuwapo kwa matabaka ya walionacho na walalahoi," anadai.

Anasema, ili wananchi waondokane na hali hiyo, hawana budi kuichagua Wazalendo kupitia kampeni inayoendelea katika mikoa mbalimbali ya kuingiza wanachama wapya.

Kiongozi huyo anaongeza kuwa nguvu ya wananchi kuiwajibisha serikali ya CCM ipo mikononi mwao, na kwamba hawana budi kuunga mkono kampeni zinazoendelea kwa kujisajili kuwa wanachama wa chama hicho.

"Tukiwa madarakani tutahakikisha uchumi unakua na kuzalisha ajira nyingi na kila Mtanzania anapata matibabu kwa kuunganishwa kwenye mfumo wa hifadhi ya Jamii (NSSF na PSSSF)," anasema Mchinjita.

Ili chama kiweze kufikia mafanikio hayo, ni muhimu wananchi kujisajili kuwa wanachama wa ACT-Wazalendo, uwe ni ujumbe kwa CCM kuwa umeikataa serikali ya chama hicho, ijiandae kuondoka madarakani kwenye uchaguzi ujao, anasema Mchinjita.

# Wanawake wapiganaji wanavyosimamia mageuzi kiutendaji tasnia ya habari

**INATOKA UK. 11**

Katika maeneo ya kazi unapopata cheo lazima kutakuwa na maneno, wengine watakupongeza na wengine watasema hakustahili, anaeleza Beatrice.

"Lakini nikasema hao wanaoona kuwa wanastahili cheo hiki kuliko mimi mbona hawajapewa? Kwa nini mimi? Hapo nikapata jibu kuwa nipo kwa sababu ninastahili na hivyo ninaweza, nikaachana na maneno yao nikatekeleza majukumu yangu kama inavyostahili."

Kutokana na utendaji kazi mahiri mwaka huu, Beatrice ametambuliwa na kupewa tuzo Mwanamke Kiongozi katika Chombo cha Habari (2024 Women In News Laureate Leadership Awards), iliyotolewa na Umoja wa Wachapishaji wa Magazeti Duniani (WAN-IFRA).

Mhariri Mkuu wa Clouds Media Group, Joyce Shebe, ameshika jukumu hilo tangu Novemba 2010, baada ya kuonyesha uwezo mkubwa na bidii ya kiutendaji katika majukumu ya chini ikiwamo uandishi na uhariri wa habari.

Kama ilivyokuwa kwa wengine haikuwa rahisi kwa Joyce pia, ni kutokana na changamoto ya kutokukubalika kwa baadhi ya wafanyakazi.

Anasema hasa wanaume walikuwa wengi katika chumba cha habari na baadhi yao walikuwa viongozi wake hapo awali.

Anasema alikabiliana na changamoto hiyo kwa kumchukulia hatua yeyote aliyempa majukumu na kukaidi na pale aliipoona upinzani unazidi kuongezeka alikwenda kutoa taarifa ngazi za juu.

Halikadhalika alipitia changamoto ya kushindwa kugawa muda wake ili aweze kuhudumia familia na kutimiza majukumu ya kazi, lakini baadaye alihudhuria mafunzo ya namna ya kugawa mujukumu yake na wale waliomzunguka ofisini.

"Nilipambana sana kuongeza maarifa kwa kuhudhuria mafunzo mbalimbali ya kiuandishi na uongozi ili niikuze taaluma yangu na niwe bora zaidi.

"Pia kujitofautisha na wengine na hili lilinisaidia kufika hapa nilipo. Mimi kwangu kujifunza ni sehemu ya maisha yangu," anasema Joyce, ambaye ni Mwenyekiti wa TAMWA.

Anasifu kuwa changamoto hizo zilimkuza na kumjengea ujasiri wa kuwania nafasi mbalimbali za uongozi katika tasnia hiyo ikiwamo ujumbe wa bodi katika Jukwaa la Habari Tanzania na kufanikiwa kuendeleza harakati za kutetea na kuendeleza maslahi bora ya wanawake.

**ITAENDELEA WIKI IJAYO**

JUKWAA LA VIONGOZI

KUJIUZULU KINANA

# Kunavyoakisi ukomavu wa demokrasia ndani ya chama

**Na Sabato Kasika**

MAKAMU Mwenyekiti wa CCM Bara, Abdulrahman Kinana, amejiweka pembeni, akijiuzulu nafasi hiyo na kuacha maswali mengi ndani na nje ya mipaka kwa wanaofuatilia siasa za Tanzania.

Wapo wanaosema kulikoni? Uamuzi huo kwa nini umekuwa ghafla kiasi hicho?...Wadau wa kisiasa na uongozi wanazungumza na Nipashe kuhusu uamuzi huo ulioridhiwa na Mwenyekiti wa CCM Taifa, Rais Samia Suluhu Hassan.

James Mbatia, anaanza kuelezea hatua hiyo kuwa ni vigumu kuitenganisha na suala la Mawaziri Nape Nnauye (Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari pamoja na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika, Mashariki January Makamba, waliotenguliwa.

Anafafanua kuwa wakati wa serikali ya awamu ya tano, Kinana akiwa Katibu Mkuu wa CCM, aliomba kustaafu, na kwamba wakati huu akiwa Makamu Mwenyekiti CCM Bara, anajiuzulu.

"Hivyo, kuna haja ya kutofautisha kati ya kujiuzulu na kuomba kustaafu, lakini ni haki ya kidemokrasia kufanya uamuzi huo, jambo la msingi ni kutofautisha maneno hayo mawili," anasema Mbatia.

Mchambuzi huyo anaongeza, " Suala la Kinana nalitazama kwa pande mbili, yaani hasi na chanya, kwani linaimarisha demokrasia lakini pia hofu kutokana na kauli zake alizowahi kutoa."

Anatolea mfano kuwa Kinana alishawahi kusema, yaliyojitokeza katika uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka 2019 hayatajirudia mwaka huu, na yaliyojitokeza uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 hayajirudii mwaka ujao.

"Hivyo, wakati mwingine kauli kama hizo zinaweza zikawa hasi kwa chama chake, lakini kwa taifa ni chanya, kwa maana kwamba zinasaidia kuimarisha 4R za Rais," anasema.

Falsafa ya R nne inaanza na ya kwanza ya maridhiano ili kujenga Tanzania bora, Rais Samia akitamani kujenga jamii yenye maridhiano na maelewano, umoja pasipo kujali tofauti za kisiasa, kidini na kikabila.

Ustahimilivu ni R ya pili ambayo Rais anamaanisha kuwa Tanzania haiwezi kusonga mbele kama wananchi na viongozi hawatakuwa pamoja.

Umoja ni nguvu na namna pekee ya kupambana na changamoto zote zinazoikumba dunia kwa sasa ni mshikamano.

R ya nne ni mabadiliko, Rais Samia amedhamiria kwamba serikali itafanya mabadiliko katika mifumo ya kisiasa, kiuchumi na katika sheria zetu za uchaguzi. Kwa lengo la kwenda na wakati kwa kila idara ikiwamo demokrasia.



Aliyekuwa Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara, Abdulrahman Kinana

> Hivyo, wakati mwingine kauli kama hizo zinaweza zikawa hasi kwa chama chake, lakini kwa taifa ni chanya, kwa maana kwamba zinasaidia kuimarisha 4R za Rais.

Kujenga Upya ni R nyingine ya nne ambayo ni kukuza uchumi wa Tanzania, unaoongeza ajira kwa vijana na utakaofungua fursa kwa makundi yote ya kijamii kuwa na maendeleo endelevu.

**WANASIASA SI WAKWELI**

Mkurugenzi Mtendaji mstaafu wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Dk. Hellen Kijo-Bisimba anadai, wanasiasa hawaaminiki na kwamba wanaojua kwa nini Kinana amejiuzulu.

Mwanaharakati huyo anasema, wanasiasa wanaweza kueleza jambo fulani kinyume ili kuwaaminisha wananchi, na kwamba yaliyotokea kwa Kinana, undani wake wanaujua wenyewe.

"Niliwahi kusikia kuwa alikubali kuwa Makamu Mwenyekiti kwa kipindi kifupi kisha apumzike, lakini swali ni kwamba kwa nini ajiuzulu wakati huu ambao kuna sakata la mawaziri vijana kutumbuliwa? Anahoji.

Mwanasheria huyo nguli, anaona kuwa inawezekana ni wakati huu ndio wasaa ambao alikuwa amepanga kuachia ngazi, na kwamba angetulia kwanza ili watu wasiunganishe tukio la kutumbuliwa kwa baadhi ya mawaziri.

"Lakini kama nilivyoeleza, wanasiasa hawaaminiki, zinaweza kuwa ni mbinu za kuwafanya Watanzania wafikirie kujiuzulu kwa Kinana na kuacha mambo ya msingi yanayohusu taifa lao," anasema Dk. Hellen.

**CHAKUJIFUNZA**

Mchambuzi wa siasa ambaye ni kada wa CCM, Abdulkarim Atiki anasema, Kinana ni mwanasiasa makini ambaye si king'ang'anizi wa madaraka, na kwamba ametoa somo kwa wingine.

Anasema, si mara ya kwanza mkongwe huyo wa siasa kuomba kuachia ngazi, na kwamba aliwahi kuachia ngazi akiwa mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM, kisha akaachia ngazi akiwa Katibu Mkuu wa chama.

"Sasa ameamua kuachia ngazi akiwa Makamu Mwenyekiti wa CCM Bara, hatua hizo zote zinaonyesha ni jinsi gani asivyo king'ang'anizi wa madaraka, anaheshimu mtindo wa kupokezana vijiti," anasema Atiki.

Atiki anasema, Kinana amekuwa katika madaraka baada ya kuombwa na kwamba hata hivyo nafasi ya Makamu Mwenyekiti aliombwa kurudi kwenye siasa ili asaidie kuimarisha chama.

"Cha ajabu ni kwamba, wapo watu ambao wameanza kuzusha kuwa amejiuzulu kutokana na Makamba na Nape kuachishwa kazi. Mimi siamini kama kuna uhusiano huo," anasema.

Anafafanua kuwa Kinana ni mwanasiasa msomi ana uzoefu mkubwa wa kiuongozi. Mwanajeshi aliyepanda ngazi hadi cheo cha Kanali, na kwamba alishakuwa mbunge na mjumbe wa baraza la mawaziri kwa vipindi tofauti na Spika wa kwanza wa Bunge la Afrika Mashariki.

Alishatumikia nchi na chama, tangu Umoja wa Vijana wa TANU (TANU Youth League), akawa mwalimu wa siasa jeshini na kwamba aliongoza kampeni za urais za Rais wa Tatu, Benjamin Mkapa na Kikwete.

"Kwa hiyo, Watanzania watakuwa wanakosea kumhusisha na masuala ya mawaziri hao vijana, bali ameamua kupumzika, kwa sababu si mara ya kwanza kuomba kuachia ngazi," anasema.

Mchambuzi huyo anasema, Kinana anaweza kuwa somo kwa ving'ag'anizi wa madaraka, wajifunze kwake ili wakati wao ikiisha wang'atuke badala ya kung'ang'ania madarakani.

**HALI SI SHWARI**

Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi (CUF) Bara, Magdalena Sakaya, anasema, hatua aliochukua Kinana, inaonyesha kuwa kuna baadhi ya mambo hayako shwari ndani ya CCM.

Magdalena anasema, haiwezekani wakati huu wa kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu bila kuwapo jambo, kiongozi huyo wa ngazi ya juu wa chama kuachia ngazi.

"Ninavyoona inawezekana kuna mambo ndani ya CCM hayajamfurahisha, huwezi kuwa vitani unajiandaa kusonga mbele, halafu mwingine anarudi nyuma, lazima kuna sababu," anasema Magdalena.

Anasema, lazima kuna sababu, wangekuwa wanasiasa vijana, wangetoka nje na kuanza kutangaza kwa nini wamejiuzulu na kwamba Kinana anaheshima kubwa ndani ya jamii hawezi kuropoka.

"Kinana ni mtu asiyependa watu washinde bila kupingwa katika uchaguzi na hilo amekuwa akilisema hadharani, hivyo, inawezekana msimamo wake huo usiwafurahishe wengine," anasema.

Mwanasiasa huyo anasema, ndio maana anaamini kuwa mambo hayako shwari ndani ya CCM, na kwamba mengine hayamfurahishi kama Makamu Mwenyekiti wa chama hadi akaamua kukaa pembeni.



## HABARI DODOMA

# Wachimbaji wadogo wapewa leseni upya

**Na Thobias Mwanakatwe,**
IRAMBA

WACHIMBAJI wadogo 100 wa madini katika Kijiji cha Nkonkilangi Kata ya Ntwike Tarafa ya Shelui wilayani Iramba mkoani Singida, wamepewa leseni za kuendelea na uchimbaji katika eneo ambalo waliondolewa na kupewa mwekezaji mkubwa.

Hatua hiyo, imetokana na agizo la Rais Samia Suluhu Hassan kuagiza wachimbaji wapewe leseni baada ya kutoa ombi kwake.

Wakizungumza na gazeti hili kwa nyakati tofauti wameishukumru serikali kwa kuwafungulia leseni za uchimbaji wa madini ambazo zilikuwa kifungoni kwa miaka mingi.

Wachimbaji hao wa Mgodi wa Sekenke One walisema wamesumbuka kwa muda mrefu kutafuta leseni hawakufanikiwa lakini hivi sasa wamefanikiwa.

Mmoja wa wachimbaji hao, Rashidi Mgendi alisema leseni ya mgodi huo inamilikiwa na watu wengi hivi sasa.

"Hakika imekuwa ni faida kubwa kwetu kwa sababu vipande zaidi ya 100 vinamilikiwa na wachimbaji wadogo," alisema.

Naye, Sudi Abasi alieleza mafanikio hayo ni baada ya kumuomba Rais Dk. Samia wakati alipofanya ziara wilayani humo kwa sababu kabla walikua wamekwishahangaika bila mafanikio.

Mchimbaji mwingine katika mgodi huo, Joseph Mnemba aliweka wazi changamoto ya kupata leseni iliyowakabili tangu mwaka 2012 .

Alibainisha watu wengi walitafuta leseni tangu mwaka huo lakini hawakufanikiwa.

"Tulipokua tunachimba bila leseni ukipata mwamba au sehemu ya kuchimba wanakuja watu ambao wanasema hapo ni sehemu ya leseni yao na wanakutoa katika eneo hilo," alisema na kuongeza kuwa;

"Tunamshukuru sana Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kutoa leseni ambazo zilikua kifungoni."

Aidha, serikali ilihamisha leseni iliyokua ikimilikiwa na mwekezaji mmoja na kuwapa wachimbaji wadogo kwa lengo la kuongeza ushiriki wao katika sekta ya madini.

Hatua ambayo itaendelea kuchochea ukuaji wa uchumi kwa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla,"alisema.

Aidha, aliendelea kusema kuwa, Rais Samia ameendelea kuwawezesha vijana na kwamba hadi kufikia Machi 2024 serikali ilitoa leseni 6,934 kwa wachimbaji hao ikilinganishwa na leseni 5,094 za mwaka 2018 hadi 2019, huku fedha za mikopo zikiongezeka kutoka Sh. billion 145 mwaka 2022 hadi Sh. bilioni 187 mwaka huu.

# Mwigulu atoa maagizo saba kwa watumishi wizarani

**Na Ibrahim Joseph,**
DODOMA

WAZIRI wa Fedha Dk. Mwigulu Nchemba, ametoa maagizo saba kwa watumishi wa wizara hiyo ikiwemo kuimarisha mfumo wa ukusanyaji mapato ili kutoa fedha kwa wakati kwenye miradi yote iliyoidhinishwa na Bunge.

Dk. Mwigulu alisema hayo juzi kupitia hotuba yake iliyosomwa kwa niaba yake na Naibu Waziri wake, Hamad Chande wakati wa ufunguzi wa kikao cha watumishi wa wizara ya fedha kilichofanyika jijini hapa.

Aliwataka wafanyakazi hao kuimarisha mfumo wa ukusanyaji mapato na kuratibu upatikanaji wa fedha ili kutoa fedha kwa wakati kwa miradi yote iliyoidhinishwa na Bunge.

Maagizo mengine ni kufanyia kazi kwa wakati mambo yatokanayo na mjadala wa bajeti ya serikali kwa mwaka 2024/25 na kufanya kazi kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo iliyopo ili kuimarisha mfumo wa utawala bora na unaozingatia sheria.

Alisema maagizo mengine ni kutumia taaluma zao katika kushauri na kufanya maamuzi kwa wakati na kwa maslahi mapana ya taifa.

Pia, aliwataka kuwa mfano katika kuzingatia miongozo ya usimamizi wa mali na fedha za umma, hususani kufungamanisha mahitaji na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge.

Aidha, aliagiza kuimarisha mfumo wa ushirikishaji, uratibu na kufanya kazi kwa karibu na wadau ili kuongeza ubora wa huduma kwa wateja wa ndani na nje.

Kadhalika, aliwataka wakuu wa taasisi za wizara hiyo waendelee kusimamia majukumu waliyopewa ili kuchangia fedha katika mfuko mkuu wa serikali.

Vilevile, aliwataka kusimamia mali na fedha za serikali kwa kuzingatia sheria na kanuni ili kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za umma katika ununuzi.

Pia, Dk. Mwigulu aliwataka wakatekeleze kwa ufanisi sheria ya ununuzi wa umma ya mwaka 2023 na kanuni zake pamoja na kutumia mfumo wa NeST, na watimize viapo na wajibu wao katika suala la usimamizi wa mali na fedha za umma.

Awali, Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Jenifa Omolo alisema lengo la kikao kazi hicho ni kuwajengea uwezo wafanyakazi.

Alisema katika kikao kazi hicho kutakuwa na mada mbalimbali zitakazotolewa na wabobezi katika mada hizo na wameshirikisha wadau wengine.




Baadhi ya wanafunzi wa shule mbalimbali za mkoa wa Dodoma, wakishiriki maandamano ya maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Kupinga Usafirishaji Haramu wa Binadamu yaliyofanyika kitaifa jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Vijana 500 kushiriki kongamano kujadili maeneo matano ya kimaendeleo

**Na Paul Mabeja,**
DODOMA

ZAIDI ya vijana 500 kutoka Mikoa mbalimbali nchini wanatarajiwa kushiriki kwenye kongamano la kujadili masuala yanayohusu uongozi, afya, uchumi, teknolojia ya kidijitali na mabadiliko ya tabianchi.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Vijana Tanzania (TYF), Rajabu Juma, alibainisha hayo jana jijini hapa, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kongamano hilo litakalofanyika kwa siku mbili (jana na leo).

"Tuna furaha kubwa kuwatangazia kongamano la vijana litakalofanyika kwa siku mbili jijini Dodoma kuanzia Julai 30 hadi 31, 2024 na kukutanisha zaidi ya vijana 500 kutoka maeneo mbalimbali nchini Tanzania Bara na Zanzibar,"alisema.

Aidha, alisema lengo la kongamano hilo ni kuimarisha ustawi na maendeleo ya vijana nchini.

"Kongamano hili muhimu limeandaliwa na Shirika la Vijana Mkoa wa Dodoma (DOYODO) kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi,Vijana na Wenye ulemavu pamoja na mashirika mbalimbali yasiyo ya kiserikali yasiyopungua 35,"alisema. Alisema kongamnao hilo litawaleta pamoja vijana kutoka sehemu mbalimbali za nchi, viongozi wa serikali, wadau wa maendeleo na wataalamu wa sekta mbalimbali ili kujadili masuala mbalimbali.

Aidha, alisema masuala hayo ni yale yanayohusu uongozi, afya, uchumi, teknolojia ya kidijitali na mabadiliko tabianchi lengo likiwa ni kusaidia kuboresha ustawi wa vijana na taifa kwa ujumla.

"Kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022, vijana wenye umri wa miaka 15 hadi 35 wanachangia asilimia 37 ya idadi ya watu nchini. Hivyo, kongamano hili lina umuhimu mkubwa kwa kuwa litasaidia kuweka mazingira wezeshi ya kuwainua vijana kiuchumi na kijamii,"alisema.

Kadhalika, alisema kongamano hilo ni fursa adimu kwa vijana kujifunza, kubadilishana mawazo na kuunda mitandao ya ushirikiano itakayosaidia kutatua changamoto wanazokutana nazo.

"Aidha, DOYODO itaendelea kushirikiana na serikali, vijana na wadau wengine kuhakikisha maazimio yote yatakayofikiwa yanatekelezwa ipasavyo kwa ajili ya maendeleo ya vijana nchini,"alisema.





# Polisi Njombe lawamani, wafanyabiashara kuvamiwa

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

SIKU chache baada ya mfanyabiashara Godfrey Ndambo Mkazi wa Mji wa Njombe kuvamiwa na kuuawa na majambazi kisha kumpora zaidi ya Sh. milioni 47, wafanyabiashara wa mkoani humo wamelijia juu Jeshi la Polisi wakidai limeshindwa kuwalinda.

Mfanyabiashara huyo aliuawa Julai 20, mwaka huu usiku, wakati akitoka kazini ambapo wahalifu walimpiga na kitu chenye ncha kali kichwani.

Wafanyabiashara hao wamesema vitendo vya uhalifu vimekithiri mkoani humo hasa mauaji ya watu na uporaji wa mali hali ambayo wanadai imeanza kuwakosesha amani wakati wanapotekeleza majukumu yao.

Walitoa malalamiko hayo jana na kwenye kikao cha wafanyabiashara wa huduma za fedha kilichofanyika mjini hapa, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Njombe pamoja na vyombo mbalimbali vya ulinzi na usalama.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Anna Mayemba alisema wamekua wakiripoti matukio ya kuibiwa na kutoa vielelezo, lakini watuhumiwa hawakamatwi badala yake wapelelezi wamekuwa wakiwazungusha.

"Mimi ni miongoni mwa waathirika kwani niliripoti tukio la kuibiwa na nikawasilisha vielelezo vyangu vyote na nikapewa mpelelezi wangu aanze kufuatilia mwenendo wa kesi yangu, kama huna pesa ya kumpa chochote mpelelezi kesi yako haiwezi kufika popote," alisema Mayemba. Alisema aliibiwa Sh. milioni 23 na kwamba aliomba kiasi cha fedha ambacho hakutaja na mpelelezi wa kesi yake na kwamba alimwambia fedha zilizopotea zikipatikana atamlipa tena Sh. milioni 10 na kwamba mpaka sasa fedha zake hazijapatikana na hakuna kinachoendelea.

Mwenyekiti wa Mawakala wa Mkoa wa Njombe, Erasto Mbembati, alisema matukio ya wafanyabiashara kuvamiwa yamekuwa yakifanyika wanapotoka kwenye maeneo ya biashara wakielekea nyumbani na hivyo akaomba jeshi hilo kuimarisha doria.

Alisema kutokana na hofu waliyonayo ya kuvamiwa na wahalifu, wameamua kuanza kufunga biashara zao saa 12 jioni badala ya kufanya kazi mpaka usiku hali ambayo alisema itasababisha uchumi kuyumba.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Kamishna Msaidizi Mahamoud Banga, alisema amepokea malalamiko hayo na kwamba atayafanyia kazi ikiwamo kuchukua hatua kali kwa askari polisi wanaosababisha kukwamisha upelelezi kwa kuomba fedha kwa waathirika wa matukio ya wizi.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, aliliagiza Jeshi la Polisi kufanya kazi kwa kuzingatia miiko ya kazi yao, huku akiwataka wafanyabiashara wasifunge biashara saa 12 jioni kama walivyoamua kwa sasa kwani polisi wako kazini watawalinda.

Aidha, alisema Jeshi la polisi litafanya kazi ya kuwalinda muda wote na wahalifu lazima watakamatwa na kuchukuliwa hatua kali ili kukomesha vitendo hivyo.

Mtaka aliwataka wafanyabiashara hao kubadilika na kufanya kazi kidigitali kwa kufunga Kamera za ulinzi (CCTV Camera), kuhakikisha zinafanyakazi muda wote ili kupunguza matatizo ya kiusalama.



Wanachama wa kikundi cha vijana na wanawake kinachojihusisha na uhamasishaji wa kuchangamkia fursa za kiuchumi cha TK Movement mkoani Mbeya, wakifuatilia hotuba za viongozi mbalimbali wa serikali, wakati wa uzinduzi wa kikundi hicho, jijini Mbeya jana. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# CCM Mbeya yaahidi kumlinda Spika Tulia

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, kimesema kitahakikisha kinamlinda Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson kwa gharama yoyote na kuhakikisha anaendelea kubaki madarakani kikidai kuwa ameupatia heshima mkoa huo.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama hicho taifa (NEC) anayewakilisha Mkoa wa Mbeya, Ndele Mwaselela aliyasema hayo juzi kwenye mkutano wa hadhara wa chama hicho uliofanyika katika Kata ya Isyesye jijini Mbeya.

Alisema kabla Dk. Tulia hajawa Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini mwaka 2020 chama hicho kilikuwa hakina muunganiko mzuri akidai kilikuwa kimegawanyika kwenye makundi mbalimbali ambayo yalikuwa yanasigana.

Aidha, alisema baada ya Dk. Tulia kuwa mbunge aliyaunganisha makundi yote na kukifanya chama hicho kiwe na nguvu kubwa ambayo inakifanya kiwe na uhakika wa kuendelea kuongoza jimbo hilo la Mbeya Mjini.

Alisema kiongozi huyo amekuwa akiwasaidia mitaji wajasiriamali wakiwamo waendesha pikipiki na kuwajengea nyumba wananchi wasiojiweza.

Akizungumza kwenye mkutano huo, Dk. Tulia alisema serikali imewekeza fedha nyingi katika Jiji hilo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo ya sekta ya afya, elimu na miundombinu ya barabara.

Alisema kwa sasa katika Jiji hilo serikali inaendelea na ujenzi wa barabara ya njia nne yenye urefu wa km. 29 kutoka Nsalaga mpaka Ifisi katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi pamoja na ujenzi wa barabara za mitaa.

Vilevile, alisema serikali imejenga vituo vya afya katika kata mbalimbali za jiji hilo ambazo awali zilikuwa hazina, ujenzi wa zahanati kwenye mitaa ambayo ilikuwa haina.

Aidha, alisema serikali imejenga vyumba vya madarasa kwenye shule mbalimbali za sekondari na msingi pamoja na kujenga shule mpya ili kupungua msongamano wa wanafunzi kwenye vyumba vya madarasa.

# Mbegu za alizeti tani 40 kusambazwa kwa wakulima

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

ZAIDI ya tani 40 za mbegu bora za alizeti zinatarajiwa kusambazwa kwa wakulima katika maeneo mbalimbali nchini ili kuongeza uzalishaji wa zao hilo na kupunguza tatizo la uhaba wa mafuta ya kupikia ambalo limekuwa likilikumba taifa.

Inaelezwa kuwa, Tanzania ni moja kati ya mataifa duniani yanayotumia fedha nyingi kuagiza mafuta ya kupikia kutoka nje kutokana na uzalishaji wa bidhaa hiyo kuwa mdogo.

Taasisisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI), Kituo cha Uyole jijini Mbeya ndicho kilichoandaa mbegu hizo na zinatarajiwa kusambazwa kwa wakulima katika msimu ujao wa kilimo.

Mtafiti wa alizeti wa kituo hicho, Beatha Paulo, alisema uzalishaji wa mbegu hizo ni sehemu ya mikakati iliyowekwa na serikali katika kukabiliana na upungufu wa malighafi za kuzalishia bidhaa hiyo nchini.

Alisema baada ya kukamilisha uzalishaji wa mbegu hizo wamezikabidhi kwa Wakala wa Taifa wa Uzalishaji na Uendelezaji wa Mbegu za Kilimo (ASA), ambao ndio wenye mamlaka ya kuzisambaza kwa wakulima.

"Mbegu hizi ambazo ni za msingi, tumesaidiwa na serikali pamoja na wadau mbalimbali katika kuziandaa, na tunashukuru sana kwa kutuwezesha kufanikisha uzalishaji huu na hizi mbegu uzaaji wake ni mkubwa sana ikilinganishwa na zile za asili," alisema Beatha.

Aidha, aliwataka wakulima kuchangamkia mbegu hizo kwa maelezo kuwa zina tija kubwa kuliko zile za asili ambazo wamekuwa wakizitumia na kwamba wakulima wanatakiwa kuacha kilimo cha mazoea.

Mwakilishi wa Idara ya Uhawilishaji wa Teknolojia na Uhusiano wa (TARI), Rehema Chiumbe, alisema mbegu hizo zina uwezo mkubwa wa kukabiliana na hali mbaya ya hewa ikiwamo kuvumilia ukame na mvua nyingi.

Alisema mbegu hiyo aina ya 'Record' inavumilia magonjwa na hivyo akawataka wakulima kuchangamkia kutokana na kwamba watatumia gharama ndogo kuzalisha na kupata tija ambayo itawaongezea kipato.

Alisema wameshaifanyia mbegu hiyo majaribio katika maeneo mbalimbali na kubaini kuwa inafaa na kwamba ndiyo maana wameamua kuisambaza ili iendelee kulimwa.

"Serikali imetoa fedha nyingi sana kwa ajili ya utafiti huu, sasa ili faida yake ionekane wakulima wanatakiwa waipate mbegu hii haraka na ndio maana tumeanza mapema kabla msimu haujaanza ili wazinunue na kuzihifadhi wakisubiri msimu ufike," alisema Rehema.

Alisema mbali na kuzifanyia majaribio mbegu hizo, pia wamewafundisha wakulima mbinu bora za uzalishaji wa zao hilo na kwamba wanaendelea kupitia mashamba darasa yaliyoko katika maeneo mbalimbali.

Baadhi ya wakulima ambao mbegu hiyo ilifanyiwa majaribio kwenye mashamba yao msimu uliopita, walisema mbegu hiyo imefanya vizuri zaidi kuliko za asili ambazo walikuwa wanazitumia.

Mmoja wa wakulima hao, Rehema Simbeye kutoka wilayani Mbozi katika Mkoa wa Songwe, alisema awali alikuwa anatumia mbegu za asili na alikuwa anapata kati ya gunia mbili mpaka nne kwenye ekari moja lakini alipopanda mbegu hiyo amevuna gunia 12.





## Kampuni yaeleza sababu kuchelewa ujenzi barabara

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Ujenzi ya MECCO imeeleza sababu za kuchelewa kwa ujenzi wa mradi wa barabara ya Chakechake hadi Wete Pemba kuwa ni kuongezeka kwa kazi kwa kiwango cha asilimia 1,015 baada ya kubainika barabara ya zamani inahitaji kuchimbwa udongo na kuondolewa na kuwekwa udongo mwingine.

Hayo yalisemwa jana na Mhandisi wa kampuni hiyo Nassor Ramadhan, wakati akitoa taarifa ya maendeleo ya ujenzi wa mradi huo kwa Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla baada ya kukagua maendeleo ya mradi huo kisiwani Pemba.

"Mshauri elekezi alielekeza barabara iliyokuwapo yote iondolewe kwa kuchimbwa kwa kina cha wastani wa mita 600 ya udongo wote na kuweka udongo mwengine ili barabara iwe na kiwango bora," alibainisha mhandisi huyo.

Aidha, alisema kazi hiyo imesababisha kuongezeka kwa kazi ya kukata na kutupa udongo kutoka mita za ujazo 26,600 hadi 270,000 ikiwa na wastani wa ongezeko la kazi asilimia 1,015.

Aidha, alisema mradi huo wenye urefu wa kilomita 22 ulianza utekelezaji wake Februari mwaka 2022 na ulitakiwa kukamilika ndani ya miezi 30 na ulitarajiwa kugharimu Sh. bilioni 23.

Waziri wa Mawasiliano, Uchukuzi na Usafirishaji, Dk. Khalid Salum Muhamed aliitaka kampuni hiyo kuongeza kasi ya ujenzi ili mradi huo ukikamilika Desemba na kuzinduliwa Januari mwakani.

Aidha, alisema Rais wa Zanzibar, Dk. Mwinyi ameweka kipaumbele kikubwa katika ujenzi wa miundombinu ambayo itarahisisha maendeleo kwa wananchi wa Zanzibar.

Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdullah, alisema barabara ya mkoani, Chakechake, Wete ndio nguzo ya uchumi ya kisiwa hicho kutokana na kutumika kwa shughuli za uchukuzi na usafirishaji.

"Pamoja na changamoto zilizojitokeza mategemeo yangu mtakamilisha kwa wakati ujenzi huu ili kuwaondolea changamoto wananchi wanaotumia barabara hii," alisema makamu huyo.

Hata hivyo, taarifa zaidi zinasema kuwa, kuchelewa kulipwa kwa wakati kampuni ya Mecco pia kumechangia matatizo ya mradi huo kuwa nyuma ya wakati, ikiwamo maombi ya malipo ya awamu ya nne yamechelewa kwa siku 177 ikiwa ni zaidi ya miezi sita, hivyo mkandarasi hajalipwa kiasi cha Sh. bilioni nne.

Aidha, mkandarasi wa ujenzi huo amelazimika kuchukua mkopo benki yenye thamani ya Sh. bilioni saba na kulazimika kulipa riba ya Sh. milioni 50 kwa kila mwezi.

# ACT-Wazalendo yamtaja Zitto fedha za UVIKO-19

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimesema kuwa, Kiongozi Mstaafu wa Chama hicho, Zitto Kabwe ndiye aliyefanikisha Tanzania kupata Sh. trilioni moja za kupunguza athari za kiuchumi baada ya kutokea kwa ugonjwa wa UVIKO-19 na Zanzibar kunufaika na Sh. bilioni 230.

Makamu Mwenyekiti wa ACT -Wazalendo, Ismail Jussa Ladhu, aliyasema hayo jana alipokuwa akihutubia mkutano wa hadhara wa chama hicho uliofanyika katika Uwanja wa Kata Tango Jimbo la mkoani, Mkoa wa Kusini Pemba.

Alisema, baada ya ugonjwa huo kusababisha hali ngumu ya kiuchumi, aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais Marehemu Maalim Seif Sharif Hamad, aliwaita vijana wake na kuwataka watafute vyanzo vya fedha vya kunusuru hali mbaya ya uchumi baada ya kuombwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi.

"Miongoni mwa vijana wa Maalim Seif waliojitokeza kufanya kazi hiyo alikuwa Zitto Kabwe na kufanikisha kupatikana kwa fedha hizo Sh. trilioni moja kupitia Benki ya Dunia (WB) na Shirika la Fedha Ulimwenguni (IMF)," alisema Jussa.

Aidha, Makamu Mwenyekiti huyo alisema kwa kuwa sekta ya utalii ndiyo nguzo ya uchumi wa Zanzibar ilitetereka ndipo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan kwa mapenzi yake na Zanzibar kati ya fedha hizo alitenga Sh. bilioni 230 kusaidia sekta mbalimbali visiwani humo.

"Huu ni mfano mdogo tu ambao tumeonesha tukiwa nje ya madaraka. Hivyo, tukiwa ndani ya madaraka, tutafanya mambo makubwa zaidi ya hayo," alisema.

Vilevile, alisema kwamba masoko yanayojengwa Zanzibar yanajengwa bila ya kuzingatia mipango na ndiyo maana kuna masoko yamejengwa, lakini hayatumiwi na wafanyabiashara kwa sababu hawakushirikishwa kabla ya masoko hayo kujengwa.

Mwenyekiti wa ACT -Wazalendo, Othman Masoud, alisema katika utumishi wake wa miaka 25 ndani ya serikali ya Zanzibar, anazifahamu vizuri kero za Muungano baada ya kushiriki kamati 25 na vikao zaidi ya 300 vinavyojadili mambo ya muungano, mbali ya kuwa mjumbe wa tume ya pamoja ya fedha.

Alisema utatuzi wa kero za Muungano unahitaji ujasiri kwa sababu mambo yanayolalamikiwa na Zanzibar ndiyo yenye uwezo wa kuifungua Zanzibar kiuchumi baada ya kuyaondoa katika mfumo wa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama hicho, Profesa Omar Fakihi, alisema maneno yaliyowahi kutolewa na aliyekuwa Rais wa Zanzibar marehemu Aboud Jumbe Mwinyi yana umuhimu mkubwa katika kujenga uchumi wa Zanzibar na misingi ya demokrasia.

"Jumbe alisema huwezi kuleta maendeleo ya nchi bila ya kuwa na ardhi, watu, siasa bora na uongozi bora lakini vyote hivyo vipo, ila tatizo lipo kwenye uongozi bora," alisema.

Aidha, alitoa mfano wa nchi ya Sengapol ni nchi yenye watu milioni sita, na kisiwa hicho kikiwa nusu ya kisiwa cha Pemba kwa ukubwa, lakini kimepiga hatua kubwa ya maendeleo baada ya kuwa na sifa ya mambo manne aliyoyasema Mzee Jumbe wakati wa uhai wake.



Kamishna wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Tanzania, Khatib Mwinyichande Khamis (katikati), akitoa maelezo kwa waandishi wa habari, mjini Zanzibar juzi, kuhusu ukusanyaji wa maoni kwa wadau mbalimbali wa mambo ya utalii, uchumi wa bluu na nishati. **PICHA: MAELEZO ZANZIBAR**

# Tamasha la Kizimkazi kufanyika Septemba, kuongeza idadi ya watalii

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

TAMASHA la Kizimkazi kwa mwaka huu linalotarajiwa kufanyika Septemba litaongeza kasi ya idadi ya watalii na kuzinduliwa kwa miradi mbalimbali ya maendeleo.

Hayo yalisemwa jana na Mwenyekiti wa Kamati ya Tamasha hilo, Mahfoudhi Said Omar wakati akizungumza na waandishi wa habari katika eneo la Kizimkazi Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema katika tamasha hilo litakaloanza Septemba 18, mwaka huu, kutakuwa na shughuli za kukuza uchumi, utamaduni na maendeleo ya jamii.

Pia mwenyekiti huyo alisema wageni mbalimbali wakiwamo watalii watakaofika katika tamasha hilo, watapata fursa ya kujionea shughuli za kimila, kijadi na kiutamaduni ili kufahamu mila na tamaduni za Tanzania.

Mkurugenzi wa Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), Ephrahim Mafuru, alisema tamasha hilo litashirikisha pande zote za Muungano yaani Tanzania Bara na Zanzibar na kwamba litachangia kuongeza pato la taifa na kipato cha mtu mmoja mmoja.

Aidha, alisema vijana watapata fursa ya kupata elimu ya kuwawezesha kupata kipato chao kwa ajili ya maendeleo licha ya sherehe zitakazo kuwapo.

Aidha, Katibu wa Tamasha hilo, Hamid Abdulhamid Khamis, alisema watatoa mafunzo kwa vijana 500 ambapo watakuwa katika makundi matano ikiwamo ujasiriamali, uvuvi, kilimo, sanaa na utalii.

Mwanzilishi wa tamasha hilo, Said Hamad Ramadhan, alisema walianzisha tamasha hilo miaka minane iliyopita kwa lengo la kuimarisha utamaduni na historia ya mkoa huo.

Alisema, tathmini ya tamasha hilo linaonesha kukua kwa kasi kutokana na maandalizi makubwa yaliofanyika na shughuli zilizoandaliwa.

Tamasha hilo litafunguliwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi Septemba 18 na kufungwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan Septemba 25 ambapo kauli mbiu ya tamasha hilo ni, 'Mitano kwa Mama, Neema kwa Watanzania."

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI NA TRANSCRIPT



**ANTONIA KASIO KAGUO** anatangaza kupotea kwa cheti cha chuo na transcript vya **BACHELOR OF EDUCATION IN ADULT EDUCATION AND COMMUNITY DEVELOPMENT** vyenye usajili namba **T/UDOM/2020/03567** vilivyotolewa na CHUO KIKUU CHA DODOMA mwaka 2023. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DOD/CHE/24508/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**MICHAEL REVOCATUS KIFYULA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye No. **NS0114/0032/2017** Kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia shule ya **ST JOSEPH KAENGESA SEMINARY mwaka 2017,** Cheti hiki kimepotea SUMBAWANGA. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya Polisi: **PHQ/RUK/SUM/1911/2024**

## KUPOTEA KWA PASSPORT YA KUSAFIRIA



**MOSES CHARLES MANUMBU** anatangaza kupotea kwa passport ya kusafiria yenye namba **TAE179018** iliyotolewa WASHINGTON, USA mwaka 2019 kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN/6829/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**LISSA JAMES JESSE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S3548/0005** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **MIDWAY SECONDARY SCHOOL** mwaka 2014. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/ILA/157877/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA SCANIA NA TRACTOR

**FRANK DISMAS KISWAGO** anatangaza kupotea kwa kadi za **SCANIA NA TRACTOR** zenye jina la umiliki **MGUYA COMPANY LIMITED** usajili namba **T 859 CFE na T522 AGZ .** Kwa yeyote atakaezіona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**PHQ.SAR/KIN/157843/2024**

---

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO. 16800 OF 2024**

**In the Matter of the Estate of the Late: GERALD MAHAMBA LUOGA**

**By 1: EPIFANIA AMBROS NJOVU**
**2: JOVINUS GERALD LUOGA**
**3: WINIFRIDA GERALD LUOGA**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above - named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 12 day of AUG.2024

Dated at MOROGORO this 25TH day of JULY.2024

RESIDENT MAGISTRATE

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE DISTRICT COURT P.O.Box 660, Morogoro

---

**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya wilaya ya Muheza Mkoa wa Tanga**

**Usimamizi wa mirathi Na 17579/2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU....AMINIEL NDENGERIO SWAI**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOTOLEWA NA LADDY AMINIEL SWAI**

**TANGAZO**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 25 mwezi 08 mwaka 2024

Kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Imetolewa leo tarehe 25 mwezi 07 mwaka 2024

RESIDENT MAGISTRATE MUHEZA
HAKIMU MKUU MAHAKAMA YA WILAYA MUHEZA

---

**SHASHINHALE AUCTION MART AND COURT BROKERS LTD**
**(Dealers in: Court Broker, Debt Collectors and commission agent)**
**TEL; 0757006076,P.O.BOX 288 – GEITA TANZANIA**

**TANGAZO LA MNADA WA BAJAJI**

**SHAURI LA MADAI NAMBA 86/2023**

**CHRISTINA LAZARO...............................................MDAI**
**DHIDI YA**
**MLANGO MAHENDE.........................................MDAIWA**

KWA MAMLAKA TULIYOPEWA NA MAHAKAMA YA MWANZO NYANKMBU WILAYA YA GEITA TUTAUZA BAJAJI MC 355 CHU YA MDAIWA MLANGO MAHENDE, ILIYOPO GEITA

**TAREHE YA MNADA: 31/07/2024**
**MUDA WA MNADA : SAA 3:30 ASUBUHI**
**SIKU YA MNADA : JUMATANO**
**ENEO LA MNADA : GEITA MJINI KATI**

**MASHARTI YA MNADA**
MNUNUZI ANATAKIWA KULIPA 25% YA PESA ITAKAYOFIKIWA MARA TU NYUNDO YA DALALI ITAKAPOMUANGUKIA, NA 75% ILIPWE NDANI YA SIKU KUM NA NNE (14) TOKA SIKU YA MNADA TOFAUTI NA HIVYO 25% HAITARUDISHWA ITAINGIA KWENYE GHARAMA ZA DALALI NA MNADA UTATANGAZWA UPYA. PIA UNARUHUSIWA KULIPA PESA YOTE ITAKAYOFIKIWA KWENYE MNADA.

**WOTE MNAKARIBISHWA**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**KELVIN ANORLD MURUSURI** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili namba **T 885 AZR.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**PHQ/KAG/BUK/10114/2024**

---

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**(DODOMA SUB REGISTRY)**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 16475 OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE NEBARTH DAIMON SILAU**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION**
**BY JENIPHA JOSEPH KIHANGA AND RHONE DAIMON SILAU**

**GENERAL CITATION**

**ALL PERSONS** Claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 9thDay of AUGUST, 2024.
Dated at Dodoma this 14th day of MAY, 2024

1st PETITIONER    2nd PETITIONER

Presented for filing this 11 Day of JULY 2024

RESIDENT MAGISTRATE

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA SHINYANGA**

Ofisi ya Mkurugenzi Manispaa ya Shinyanga kupitia idara ya ardhi na mipangomiji inatangaza kuendelea na utaratibu wa kufuta milki ya kiwanja namba 1 kitalu 34 mwanza road chenye hati namba **24188LR** Mwanza katika Manispaa ya Shinyanga baada ya mmiliki kushindwa kutekeleza masharti ya milki iliyotolewa kwake.

Mipaka ya ardhi **(i) 5492469594916 (ii) 5491749594956 (iii) 5491529594974 (iv) 5491959595021 (v )5492729594987** sababu za utelekezaji wa ardhi ni kudaiwa kodi ya pango la ardhi kwa zaidi ya miaka kumi na tatu.

Mtu yeyote mwenye maslahi na milki hii anatakiwa ndani ya siku sitini kutoa pingamizi au maelezo ni kwa nini ardhi hii isihesabike kama ardhi iliyotelekezwa chini ya sheria ya ardhi namba 4 ya mwaka 1999 kifungu cha 51(2)(a-d).
Imetolewa na idara ya ardhi manispaa ya Shinyanga na kusainiwa na

JACOB F. MWINUKA
AFISA MTEULE

LAND OFFICER
AUTHORISED OFFICER
SHINYANGA MUNICIPAL COUNCIL

---

**IN THE HIGH COURT OF UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**SONGEA SUB REGISTRY**
**AT SONGEA**

**LAND CASE NO 5545 OF 2024**

**KELVIN SHONGA ––––––– PLAINTIFF**

**VERSUS**

**LUKAS NGONYANI ............................................1st DEFENDANT**
**GERMAN SOKO.................................................2ND , DEFENDANT**
**SIFILIANO MKIMBIZI.........................................3RD DEFENDANT**
**JOSEPH BRUNO MAPUNDA ..............................4TH DEFENDANT**
**SAIDI MITI.........................................................5TH DEFENDANT**
**NESI NYONI .......................................................6TH, DEFENDANT**
**STEVEN NGONYANI..........................................7TH , DEFENDANT**
**ABDALLAH NJOVU...........................................8TH , DEFENDANT**
**REGINA MILANZI..............................................9TH DEFENDANT**
**BOSINESI.........................................................10TH DEFENDANT**
**YAKOBO MBEYU...............................................11TH DEFENDANT**
**KWANGUTI.......................................................12TH, DEFENDANT**
**MBINGA MHARULE VILLAGE COUNCIL............13TH, DEFENDANT**
**THE ATTORNEY GENERAL.............................14TH, DEFENDANT**

**TO: GERMAN SOKO, JOSEPH BRUNO, MAPUNDA,REGINA MILANZI, BOSINESI,AND KWANGUTI.**

**NOTICE OF DATE OF HEARING**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for Hearing on 05 th day of August 2024 At 09:00 am Before **Hon E.L. KAWISHE , JUDGE**
**YOU ARE ,** required to appear in this court on the fixed date without fail and you must produce on documents upon which you intend to reply in support your case
**GIVEN order my hand and the seal of the court this day 10th day of July 2024**

DEPUTY REGISTRAR

---

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA SONGEA LILILOKO SONGEA**

**MAOMBI NAMBA 74/2024**

**PETER MADUKA ––––– MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**AMUR HUMBARA}**
**HAMIMU NDAUKA } –WAJIBU MAOMBI**
**HAMISI MAPUNDA}**
**RASHIDI NINDI**

**WITO / KUITWA SHAURINI**

Hamisi Mapunda na Rashid Nindi mnataarifiwa kuwa Mleta Maombi amefungua shauri la mgogoro wa Ardhi dhidi yenu .Hivyo basi mnatakiwa kufika shaurini bila kukosa binafsi au Wakili,au wote kwa pamoja siku ya tarehe 15/08/2024 saa 4:00 asubuhi ,Kumbukeni pia nyaraka zote kuhusu mgogoro huu zipo hapa barazani kwa ajili ya kuleta hati zenu za utetezi.
Kumbuka pia kushindwa kwenu kufika shaurini kutapelekea Baraza hili kusikiliza shauri upande mmoja bila kujali uwepo wenu.
Imetolewa leo nami na muhuri wa Baraza hili leo tarehe 29/07/2024.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
SONGEA

---


**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie, 0677 020701***

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.
TUPIGIE: +255 - 0677 020701
AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.


Kwa

# Biteko ataka sera biashara ilete tija

**Na Joseph Mwendapole**

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, amezindua sera mpya ya taifa ya biashara huku akitaka itumike kuongeza thamani ya bidhaa za ndani na kuongeza ushindani wa mauzo ya bidhaa za Tanzania nje ya nchi.

Dk. Biteko aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati wa uzinduzi wa sera hiyo katika hafla iliyohudhuriwa na mabalozi wa nchi mbalimbali, mawaziri, naibu mawaziri na makatibu wakuu.

Alisema kuna umuhimu wa kutumia sera hiyo kuondoa vikwazo vya biashara na kuweka mfumo wa sheria unaolenga kuimarisha na kukuza biashara, huku akiwataka maofisa wa serikali kuachana na tabia ya kukwamisha mambo.

"Ofisa wa serikali lazima utambue kuwa heshima yako ya kukaa hapo ofisini ni kuhakikisha umewezesha watu kufanyabiashara na wakapata faida siyo kuwakwamisha maana kuna watu ambao kazi yao kubwa ni kukwamisha wengine," alisema.

Alisema mchanago wa sekta ya biashara kwenye pato la taifa bado ni mdogo hivyo kuna umuhimu wa kutumia sera hiyo kuhakikisha biashara inarahisishwa na inaongeza mchango wake kwenye pato la taifa.

"Watu walilalamikia sana kwamba sera yetu imepitwa na wakati sasa baada ya kuifanyia mabadiliko ni muda wa kuonyesha dunia kwamba tumefanya mabadiliko na tunakwenda na kasi ya dunia.

"Sera ni nyaraka sasa nyaraka ikiwepo wakakosekana watu wenye nia njema wa kuifanyia kazi itakuwa kama kitabu cha hadithi tu kwa hiyo tubadilishe mtazamo na fikra zetu tunaweza kuwa wazuri sana kwenye kuandika lakini kama haya tunayoandika hatuyafanyii kazi watu watatushangaa sana," alisema.

Alisema hakuna faida ya kuwa na sera nzuri lakini wakawepo maofisa ambao kazi yao ni kukwamisha wafanyabiashara na aliwataka kutumia sera kuwa kiunganishi baina ya wafanyabiashara na serikali.

"Rais wetu anakerwa sana na shida za wafanyabiashara, ameunda kamati kusikiliza kero zao sisi ni nani tushindwe kuwahudumia wafanyabiashara, aje mfanyabiashara umpe maisha magumu kwa sababu unamamlaka hatutakubali kabisa," alisema.



# UCHUMI COMMERCIAL BANK LTD

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

### WARAKA WA MIZANIA KWA TAREHE 30/06/2024
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo mwaka ya 30.06.2024 | Robo mwaka ya 31.03.2024 |
|---|---|---|---|
| A | **MALI** | | |
| 1 | Fedha tasilimu | 1,557 | 1,264 |
| 2 | Salio katika Benki Kuu ya Tanzania | 3,378 | 5,117 |
| 3 | Uwekezaji katika amana serekalini | 3,341 | 3,341 |
| 4 | Salio katika benki nyingine na taasisi za fedha | 7,211 | 6,833 |
| 5 | Hundi na miamala ya kushuhulikiwa | 88 | 197 |
| 6 | Miamala baina ya matawi | 0 | 0 |
| 7 | Bili zililizo afikiwa | 0 | 0 |
| 8 | Dhima za wateja zilizo kubalika | 0 | 0 |
| 9 | Mikopo iliyotolewa kwa benki nyingine | 898 | 511 |
| 10 | Uwekezaji katika amana nyingine | 0 | 0 |
| 11 | Mikopo halisi iliyopo | 37,771 | 36,775 |
| 12 | Mali nyingine | 2,493 | 3,000 |
| 13 | Uwekezaji wa hisa | 35 | 35 |
| 14 | Akauti za udhamini | 0 | 0 |
| 15 | Mali zisizohamishika , mitambo na vifaa | 2,350 | 1,594 |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | 59,122 | 58,667 |
| | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za benki nyingine na taasisi za fedha | 0 | 0 |
| 18 | Amana za wateja | 42,916 | 43,094 |
| 19 | Dhamana ya malipo kwa fedha tasilimu | 0 | 0 |
| 20 | Amana maalumu | 0 | 0 |
| 21 | Maagizo ya malipo/fedha za kuhamisha | 0 | 0 |
| 22 | Hundi na hawala za kibenki zilizotolewa | 0 | 0 |
| 23 | Limbiko za kodi na gharama zitakazolipwa | 271 | 198 |
| 24 | Dhima la tozo kwa ajili ya usuluhishi baina ya benki na mteja | 0 | 0 |
| 25 | Miamala isiyoshuhulikiwa baina ya matawi | 0 | 0 |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya kipindi kijacho na tozo nyingine zitakazolipwa baadae | 0 | 0 |
| 27 | Dhima nyingine | 751 | 439 |
| 28 | Madeni | 0 | 278 |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **43,938** | **44,009** |
| 30 | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 KUTOA 29)** | **15,184** | **14,658** |
| C | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa hisa uliolipwa | 13,421 | 13,155 |
| 32 | Akiba ya mtaji | 0 | 0 |
| 33 | Mapato yaliyobakizwa | 47 | 47 |
| 34 | Faida (hasara) ya kipindi husika | 465 | 205 |
| 35 | Akaunti nyingine za mtaji | 1,251 | 1,251 |
| 36 | Stahiki ya mwenye hisa chache | 0 | 0 |
| 37 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **15,184** | **14,658** |
| 38 | Dhima zisizo dhahiri | 4,729 | 3,837 |
| 39 | Mikopo chechefu | 2,444 | 3,219 |
| 40 | Tengo kwa ajili ya mikopo chechefu | 1,027 | 981 |
| 41 | Malinyingine chechefu | 0 | 0 |
| D | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| | Uwiano wa fedha za wanahisa na jumla ya mali | 25.68% | 24.99% |
| | Uwiano wa mikopo chechefu na jumla ya mikopo ghafi | 6.16% | 8.43% |
| | Uwiano wa mikopo ghafi na jumla ya amana | 90.40% | 87.05% |
| | Uwiano wa mikopo halisi na jumla ya mali halisi | 63.89% | 62.68% |
| | Uwiano wa mali zinazozalisha na jumla ya mali | 81.73% | 80.90% |
| | Ongezeko la amana | -0.41% | 7.86% |
| | Ongezeko la mali | 0.78% | 6.51% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO YA MWAKA UNAOISHIA 30/06/2024
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka wa sasa 30.06.2024 | Robo ya Mwaka Linganishi 30.06.2023 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30.06.2024 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 30.6.2023 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | **Mapato ya riba** | **1,846** | **1,552** | **3,583** | **3,107** |
| 2 | Gharama za riba | 510 | 426 | 968 | 783 |
| 3 | Madeni viza yaliyofutwa | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 4 | **Mapato halisi ya riba (1 kutoa 2)** | **1,291** | **1,067** | **2,524** | **2,240** |
| 5 | Punguzo/ongezeko la tengo katika mikopo | 45 | 59 | 91 | 84 |
| 6 | **Mapato yasiyo na riba** | **326** | **346** | **638** | **717** |
| | 6.1 Faida /hasara zitokanazo na miamala ya fedha za kigeni | 37 | 18 | 55 | 52 |
| | 6.2 Ada na kamisheni | 283 | 317 | 571 | 625 |
| | 6.3 Gawio | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | 6.4 Mapato mengine | 6 | 11 | 12 | 40 |
| 7 | **Gharama zisizo za riba** | **1,312** | **1,113** | **2,563** | **2,227** |
| | 7.1 Mishahara na mafao | 656 | 542 | 1,306 | 1087 |
| | 7.2 Ada na kamisheni | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | 7.3 Gharama nyingine za uendeshaji | 656 | 571 | 1,257 | 1140 |
| 8 | **Faida/(hasara) ya uendeshaji** | **305** | **300** | **599** | **730** |
| 9 | Tengo la kodi ya mapato | 72 | 114 | 165 | 168 |
| 10 | **Faida/(hasara) halisi baada ya kodi ya mapato** | **233** | **186** | **434** | **562** |
| 11 | Mapato mengine yaliojumuishwa (bainisha) | 26 | 202 | 30 | 203 |
| 12 | **Jumla ya faida /(hasara) iliojumuishwa kwa mwaka** | **259** | **388** | **464** | **765** |
| 13 | idadi ya waajiriwa | 52 | 49 | 52 | 49 |
| 14 | mapato kwa hisa | 1.93% | 3.79% | 3.46% | 7.48% |
| 15 | idadi ya matawi | 2 | 2 | 2 | 2 |
| | **BAHADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| | uwiano wa faida kabla ya kodi na watani wa mali | 0.44% | 0.38% | 0.79% | 1.55% |
| | uwiano wa faida kabla ya kodi na watani wa fedha za wanahisa | 1.74% | 1.51% | 3.11% | 4.57% |
| | uwiano wa matumizi yasiyo ya riba na mapato ghafi | 60.41% | 58.64% | 60.72% | 58.24% |
| | uwiano wa mapato halisi ya riba na wastani ya mali zinazozalishwa | 3.46% | 3.12% | 6.77% | 6.55% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA ULIOISHIA 30/06/2024
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| Mtiririko wa fedha kutokana na shuhuli za uendeshaji | Robo ya mwaka ya sasa 30.06.2024 | Robo ya Mwaka 31.03.2024 | Limbikizo la mwaka wa sasa 30.06.2024 | Limbikizo la mwaka Linganishi 30.06.2023 |
|---|---|---|---|---|
| **Mapato/(hasara) halisi** | **331** | **298** | **629** | **730** |
| **Marekebisho kwa ajili ya:-** | - | - | - | - |
| Uchakavu | 193 | 117 | 310 | 232 |
| **Badiliko halisi katika mikopo** | **(996)** | **(380)** | **(2,053)** | **(3,961)** |
| Faida / (hasara) kwenye mauzo ya mali | - | - | - | - |
| Mabadiliko halisi katika amana | (178) | 3,128 | 6,445 | 3,295 |
| Mabadiliko katika amana za muda mfupi zilizoafikiwa | - | (3,341) | (3,341) | - |
| Mabadiliko halisi katika dhima nyingine | 385 | (109) | 268 | (381) |
| Mabadiliko halisi katika mali nyingine | 507 | (429) | 245 | (757) |
| Kodi iliyopitwa | (72) | (93) | (165) | (168) |
| Mengineyo (bainisha) | (944) | (57) | (1,992) | 203 |
| **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shuhuli za uendeshaji** | **(774)** | **(866)** | **346** | **(807)** |
| **Mtiririko wa fedha kutokana na shuhuli za uwekezaji** | | | | |
| Gawio lililopokewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa mali za kudumu | (4) | (30) | (77) | (421) |
| Mapato kutokana na mauzo ya mali za kudumu | - | - | - | - |
| Ununuzi wa amana zisizoshuhulikiwa mawakala | - | - | - | - |
| Mapato kutokana na mauzo ya amana zisizoshuhulikiwa na mawakala | - | - | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shuhuli za uwekezaji** | **(4)** | **(30)** | **(77)** | **(421)** |
| **Mtiririko wa fedha kutokana na shuhuli za kifedha** | | | | |
| Ulipaji wa madeni ya muda mrefu | - | - | - | - |
| Mapato kutokana na utoaji wa madeni ya muda mrefu | - | - | - | - |
| Ongezeko la hisa | 266 | 372 | 3,194 | 68 |
| Gawio lililolipwa kwa fedha taslimu | - | - | - | - |
| Mabadiliko halisi katika madeni mengine | (278) | - | (555) | (112) |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shuhuli za kifedha** | **(12)** | **372** | **2,639** | **(44)** |
| **Fedha taslimu na mali zinazofanana na fedha taslimu** | | | | |
| Ongezeko /punguzo katika fedha taslimu na mali zinazofanana na fedha taslimu | **(790)** | **(524)** | **2,908** | **(425)** |
| Fedha na mali zinazofanana na fedha taslimu mwanzoni mwa robo mwaka/mwaka | 13,922 | 14,446 | 10,224 | 10,649 |
| **Fedha na mali zinazofanana na fedha taslimu mwishoni mwa robo mwaka/mwaka** | **13,132** | **13,922** | **13,132** | **10,224** |

### BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO YA MWAKA ULIOISHIA 30.06.2024

Katika kuandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8).

| *Jina na Cheo* | *Saini* | *Tarehe* |
|---|---|---|
| **Mr. Samwel A. Wado (Ofisa Mtendaji Mkuu)** | **S. Wado** | **29th July, 2024** |
| **Mrs. Anita Joseph Mnkeni ( Mkuu wa Idara ya Fedha)** | **A.MNKENI** | **29th July, 2024** |
| **Mr. Emmanuel Kessy (Mkuu wa Idara ya Ukaguzi )** | **E.Kessy** | **29th July, 2024** |

**Usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.**

| *Jina na Cheo* | *Saini* | *Tarehe* |
|---|---|---|
| **1. Dr. Heavenlight Kavishe (Mwenyekiti wa Bodi)** | **H.Kavishe** | **29th July, 2024** |
| **2.Mr. Munguatosha M. Makyao (Mkurugenzi)** | **M.Makyao** | **29th July, 2024** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 JUNI 2024
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizw | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya | Mengineyo (bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa robo ya kwanza inayoanza 01.01.2024** | **12,783** | **17** | **58** | **1,169** | **30** | **36** | **14,093** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato 30.06.2024 | 0 | 0 | 464 | 0 | 0 | 0 | **464** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Miamala na wanahisa | 638 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **638** |
| Gawio lililolipwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Mabadiliko katika tengo la mikopo chechefu | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Ziada ya Kisheria | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Mengineyo | 0 | 0 | (11) | 0 | 0 | 0 | **(11)** |
| **Salio la mwisho wa robo ya pili ya mwaka 30.06.2024** | **13,421** | **17** | **511** | **1,169** | **30** | **36** | **15,184** |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01 .2023** | **10,209** | **17** | **1,017** | **596** | **30** | **68** | **11,937** |
| Utoaji wa Mtaji wa Hisa | 2,574 | - | - | - | - | - | 2,574 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa(Gawio lililolipwa ) | - | - | (821) | - | - | - | (821) |
| Kodi iliyopita na mikopo iliyofutwa | - | - | (848) | - | - | - | (848) |
| Ziada Juu ya Hisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (573) | 573 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Kupungua kwa ruzuku za Mtaji | - | - | - | - | - | (32) | (32) |
| Hamisho kutoka faida au Hasara | - | - | 1,283 | - | - | - | 1,283 |
| **Salio la mwisho wa mwaka 31.12.2023** | **12,783** | **17** | **58** | **1,169** | **30** | **36** | **14,093** |

## UCB OFFERS THE FOLLOWING PRODUCTS:

- *Savings Accounts*
- *Current Account*
- *Elimu Juniour Account*
- *Mavuno Savings Account*
- *Uchumi Savings Account*
- *Fixed Deposit Accounts-(FDR) with attractive Rates*
- *Forex Accounts*
- *Bureau De Change*
- *ATMs Services,all over the Country-Umoja Switch*

CARING FOR FAMILY ECONOMY

# HOSPITALI YA MWANANYAMALA YAWAITA WAKAZI DAR WIKI YAO

**Na Enock Charles**

KATIKA kuhakikisha Watanzania wanajiepusha na magonjwa yasiyoambukiza ikiwamo kiharusi, kisukari, shinikizo la damu magonjwa ya figo, ini na uzito uliopitiliza, Hospitali ya Rufaa ya Mwananyamala sasa imekuja na Wiki ya Mwananyamala ikiwa na lengo la kuhamasisha ufanyaji mazoezi ili kuepukana na janga hilo.

Akizungumza katika uzinduzi wa Wiki ya Mwananyamala Jumapili iliyopita, yenye lengo la kuhamasisha ufanyaji mazoezi, Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mwananyamala, Zavery Benela, alisema wiki hiyo imeanza rasmi siku hiyo hiyo katika Uwanja wa Ustawi wa Jamii, Dar es Salaam na itamalizika Jumamosi ya juma hili.

**Alisema asilimia 40 ya wagonjwa wanaofika hospitalini hapo kwa mwaka ni wa magonjwa yasiyoambukiza na kushauri wananchi kuongeza kasi kufanya mazoezi.**

"Kwenye kitengo chetu cha dharura katika hospitali ya Mwananyamala, wagonjwa wengi tunaowapokea kwa miezi miwili iliyopita namba moja ni ajali, lakini namba mbili ni wale ambao wamepata kiharusi kutokana na tatizo la shinikizo la damu au kisukari.

"Ukiachilia mbali ajali, haya mengine ni kutokana na mtindo wa maisha na yanaweza kuepukika kwa njia ya kufanya mazoezi," alisema Dk. Benela.

Alisema katika Wiki ya Mwananyamala, watahamasisha michezo na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wake ambapo wafanyakazi wa hospitali hiyo wataonyesha kwa mfano michezo mbalimbali ikiwamo kucheza mpira wa miguu, mpira wa pete, kukimbiza kuku, kucheza muziki, kuvuta kamba na kukimbia kwenye magunia.

Mbali na kufanya mazoezi hospitali hiyo pia imesema katika Wiki ya Mwananyamala kwa kushirikiana na taasisi zingine zikiwamo Hospitali za Rufaa za Amana na Temeke, patakuwapo na huduma za upimaji wa afya na ushauri bure kwa wananchi, hivyo kutoa wito kwa watu kujitokeza kwa wingi.

Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Saad Mtambule, aliyekuwa mgeni rasmi katika uzinduzi huo, alisema serikali ipo tayari kutoa ushirikiano kwa taasisi za afya ikiwamo Hospitali ya Mwananyamala katika kuhamasisha michezo kwa wananchi ili kupunguza kiwango cha magonjwa yasiyoambukiza.

# *Mafunzo kucheza 10 za kirafiki*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Mafunzo SC imesema inatarajia kucheza michezo mingi ya kirafiki ili kujiandaa vema na Ligi Kuu Zanzibar, huku pia ikieleza inatarajia kusajili wachezaji wapya saba.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Abdallah Bakari 'Edo', alisema tayari timu hiyo ilishaanza mazoezi yake na kujifua vema kuelekea msimu huu mpya wa ligi ambao bado mpaka sasa haijatoka Kalenda ya Mashindano ya ZFF ikiwamo Ligi Kuu.

Alisema katika kuhakikisha anaisuka upya timu hiyo, wamepanga kucheza michezo 10 ya kirafiki ili kuangalia mwelekeo wa kikosi hicho.

Edo alisema katika michezo hiyo 10, sita anatarajia kucheza na timu kutoka Ligi Kuu na minne atachanganya timu kutoka madaraja tofauti.

Kocha huyo alisema lengo la kucheza michezo mingi katika maandalizi ya msimu mpya ni kuhakikisha anafanyia kazi suala la pumzi lakini pia kuangalia kama wachezaji wake wameshika mbinu zake.

Aidha, alisema timu hiyo imeanza mazoezi na miongoni mwa wachezaji wake wapya ambao wanania ya kuwasajili katika kikosi chao.

Alisema viwango vya wachezaji hao mazoezini vinaridhisha, hivyo huenda wakawa miongoni mwa wachezaji watakaowasajili kwa ajili ya kutumikia timu hiyo msimu huu.

Hata hivyo, alisema wanatarajia kusajili wachezaji wapya saba na kwamba wanne kati yao tayari wanaendelea na mazoezi na timu hiyo.

Mafunzo SC Katika msimu uliopita ilimaliza nafasi ya tano katika Ligi Kuu ya Zanzibar kwa kujikusanyia alama 48 katika michezo 30 waliyocheza.




Mchezaji wa Tennis, Mikidad Abdallah, akipiga mpira kurudisha kwa mpinzani wake wakati wakifanya mazoezi katika viwanja vya Gymkhana jijini Dar es Salaam wiki iliyopita. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# TBF yawapiga msasa makocha

**Na Shufaa Lyimo**

SHIRIKISHO la Mchezo wa Mpira wa Kikapu Tanzania (TBF), kwa kushirikiana na Kamisheni ya Makocha wa mchezo huo limeandaa mafunzo maalum kwa makocha ambayo yanaendelea kwenye viwanja vya JMK Park, jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa shirikisho hilo, Marry Arthur, alisema mafunzo hayo yameshirikisha makocha kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara.

Alisema yatawasaidia makocha hao kuongeza ujuzi wa kufundisha mchezo huo ikiwamo masuala ya lishe kwenye michezo na changamoto ya kutumia madawa ya kuongeza nguvu michezoni (Doping).

Alisema makocha ambao wamehudhuria mafunzo hayo ni wale wanayofundisha mchezo huo kwenye shule za msingi, sekondari pamoja na sekta binafsi za vijana wanaocheza kikapu.

"Ninaamini kila mwalimu ambaye amehudhuria mafunzo haya atafaidika kwani atapata vile alivyokuwa havifahamu ambavyo atakwenda kuwasaidia wale ambao hawajaweza kufika, alisema," alisema.

# Namungo yala tatu kwa Dodoma Jiji

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Dodoma Jiji imejaribu mitambo yake kwa mafanikio kabla ya Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao na ikakubali kwa kuichapa Namungo FC mabao 3-0, katika mechi ya kujipima nguvu iliyochezwa Uwanja wa Black Rhino, Karatu, Arusha.

Timu zote mbili zilicheza mechi zikiwa na lengo moja tu, kupima vikosi vyao kwa ajili ya Ligi Kuu 2024/25, pamoja na kuchezesha wachezaji wapya ili kuona wanaingia vipi kwenye vikosi vya kwa kwanza.

Wakati Namungo ikiendelea kunolewa na kocha aliyekuwapo msimu uliopita, Mwinyi Zahera, Dodoma Jiji inafundishwa na kocha mpya, Mecky Mexime, aliyetoka Ihefu FC ambayo kwa sasa inajulikana kama Singida Black Stars, akichukua mikoba ya Mkenya, Francis Baraza.

Mabao ya washindi yaliwekwa wavuni na Idd Kipagwile dakika ya 55 na 57, huku Mwana Kibuta akipachika bao la tatu dakika tano kabla ya mchezo kumalizika.

## ZISIKUPITE

### OSIMHEN ATAKIWA ARSENAL

ARSENAL bado inamtaka mshambuliaji wa Klabu ya Napoli na Timu ya Taifa ya Nigeria, Victor Osimhen, 25. ***(Corriere dello Sport)***

### LUKAKU AIVUTIA NAPOLI

NAPOLI inavutiwa na mshambuliaji wa Chelsea na Ubelgiji, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 31, na huenda wakamjumuisha katika mkataba wa kubadilishana na Victor Osimhen. ***(Guardian)***

### O'BRIEN SAFI EVERTON

MLINZI wa Jamhuri ya Ireland, Jake O'Brien mwenye umri wa miaka 23, amewasili Merseyside kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi wa kimatibabu kabla ya uhamisho wake wa pauni milioni 17 kutoka Lyon kwenda Everton. ***(Guardian)***

### DIARRA AWINDWA EVERTON

EVERTON huenda ikawasilisha ofa ya kumnunua kiungo wa kati wa Strasbourg na Senegal, Habib Diarra mwenye umri wa miaka 20. ***(L'Equipe)***

### CHONG AWANIWA EPL

KLABU kadhaa za Ligi Kuu England na nje ya nchi hiyo vinawania kumsajili winga wa Luton, Mholanzi Tahith Chong mwenye umri wa miaka 24, kwa takriban pauni milioni 10. ***(Sky Germany)***

### FOFANA NA WEST HAM

WEST Ham inataka kumnunua kiungo wa kati wa Ufaransa na Monaco, Youssouf Fofana, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, anavutiwa na Klabu ya AC Milan. ***(Givemesport)***

### DE GEA BASI TENA GENOA

GOLIKIPA wa zamani wa Manchester United, David de Gea mwenye umri wa miaka 33, hatajiunga na Genoa, na Mhispania huyo hakuwahi kukaribia kujiunga na klabu hiyo ya Italia. ***(Fabrizio Romano)***

### ATAJWA WEST HAM

KLABU ya West Ham imeelekeza darubini yao kwa mshambuliaji wa Borussia Dortmund na Ujerumani, Niclas Fullkrug mwenye umri wa miaka 31, wanapomtafuta mshambuliaji mpya. ***(Sky Sports)***


### SANE ATAKIWA ARSENAL

ARSENAL inavutiwa na winga wa Bayern Munich na Ujerumani, Leroy Sane, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, hana nafasi ya kuhama msimu huu wa majira ya joto. ***(Sky Germany)***

### BRUCE ANUKIA JAMAICA

KOCHA wa zamani wa Newcastle United, Steve Bruce mwenye umri wa miaka 63, yuko kwenye mazungumzo ya kuwa mkufunzi wa Timu ya Taifa ya Jamaica. Mwingereza huyo hajafanya kazi tangu alipofutwa kazi na West Brom Oktoba 2022. ***(Mail)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# ALVAREZ KUAMUA HATIMA YAKE CITY

**MANCHESTER,** England

JULIAN Alvarez amekiri kuwa hapendi kuachwa benchi kwenye mechi kubwa kule Manchester City huku uvumi kuhusu uhamisho wake ukiendelea kutanda.

**Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Argentina, ambaye alicheza kwenye Copa America 2024 kabla ya kutimkia Ufaransa kushiriki katika Michezo ya Olimpiki ya Paris, alikuwa akitumika kama mchezaji wa akiba katika kikosi cha Man City msimu uliopita na alichangia mabao 11 na asisti tisa waliposhinda taji la Ligi Kuu.**

City wanasemekana kumthaminisha Alvarez na pauni milioni 75, ambazo zinaweza kuwafanya wanunuzi watarajiwa kuondoka msimu huu wa majira ya joto, lakini amefichua kuwa kuachwa kwenye orodha ya wachezaji wa hali ya juu imekuwa ngumu kwake.

### ●●● Sijaacha kufikiria, baada ya kampeni hii ya Argentina kwenye Olimpiki nita...

Aliiambia DIRECTV Sports: "Sijaacha kufikiria nitakachofanya. Wakati kampeni hii ya ya soka ya wanaume ya Argentina kwenye Olimpiki itakapokamilika nitaanza kufikiria ninachotaka mimi mwenyewe. Tutaweza tazama mambo yanavyokwenda.

"Msimu uliopita nilikuwa mmoja wa wachezaji waliocheza dakika nyingi kwenye timu. Lakini ni kweli: mwishowe, katika michezo muhimu, hupendi kuachwa na unataka kuchangia."

Alvarez mara nyingi alionekana kwenye safu ya kiungo ya ushambuliaji kama mlinzi wa Kevin De Bruyne aliyejeruhiwa, huku pia akiwa naibu mkuu wa mbele wakati mashine ya mabao ya Norway, Erling Haaland ilipokosekana.

Tangu ajiunge na City mwaka 2022, Alvarez amekuwa mmoja wa wachezaji waliopambwa sana katika soka la dunia katika ngazi ya klabu na kimataifa.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, ameshinda mataji mawili ya Ligi Kuu England, Ligi ya Mabingwa Ulaya, Kombe la FA, UEFA Super Cup na Kombe la Klabu Bingwa Dunia na pia alishinda tuzo ya timu ya taifa akiwa na Argentina wakati wa Kombe la Dunia la 2022 na ushindi mara mbili wa Copa America.

# ARSENAL HAITASAJILI TENA KWA BEI KUBWA KAMA RICE



**PHILADELPHIA,** Marekani

MIKEL Arteta amesema Arsenal haitarajii kufanya usajili mwingine wa fedha nyingi kama Declan Rice msimu huu wa majira ya joto.

'Washikabunduki' hao walivunja rekodi yao ya uhamisho Julai mwaka jana kwa dili la pauni milioni 105 kumnasa Mwingereza huyo.

Arsenal wamefanya uhamisho wa kwanza muhimu katika dirisha la usajili la sasa, Jumatatu baada ya Riccardo Calafiori kukamilisha uhamisho wa pauni milioni 42 kutoka Bologna.

Nyota huyo sasa anaungana na wachezaji wenzake wapya huko Philadelphia kabla ya mechi ya mwisho ya ziara yao ya kujiandaa na msimu mpya nchini Marekani dhidi ya Liverpool.

Alipoulizwa kama Washikabunduki hao walikuwa na uwezo wa kufuatilia hilo na ununuzi mwingine wa aina ya Rice, Arteta alisema: "Hatutarajii kufanya kitu kama hicho. Huo ndio ukweli. Tunapaswa kusubiri na kuona mienendo sokoni, tayari tumebainisha mambo ambayo tunaweza kuboresha.

"Tulikuwa na mikutano Februari, Machi, Aprili. Kwa hiyo ikiwa tunaweza, tutaimarisha timu. Hadi sasa nina furaha sana na tulichonacho."

Arteta pia alisema wachezaji ambao bado wako likizoni kutokana na kuhusika kwao katika fainali ya Euro 2024 - Bukayo Saka, Aaron Ramsdale, Rice na David Raya - wataungana na kikosi mwishoni mwa wiki wakati Arsenal watakapokuwa wanarejea England.

# FIFA yapokea zabuni Kombe la Dunia 2030, 2034

**NYON,** Uswisi

UKIACHA Michezo ya Olimpiki ya Paris, Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA), limekuwa ikifanya biashara na waandaji wake wajao wa Kombe la Dunia la Wanaume ikiwa ni pamoja na Saudi Arabia.

FIFA ilisema Jumatatu ilipokea huko Paris zabuni rasmi kutoka kwa viongozi wa mashirikisho saba wanachama ambao ndio wazabuni wa kipekee wa Kombe la Dunia la 2030 na 2034.



Kombe la Dunia la 2030 linaandaliwa kwa pamoja Hispania, Ureno na Morocco pamoja na majirani watatu wa Amerika Kusini - Argentina na Paraguay.

Saudi Arabia ndiye mgombea pekee wa Kombe la Dunia la 2034.

Zabuni hizo mbili zimepangwa kuthibitishwa katika mkutano wa mtandaoni wa Desemba 11 wa mashirikisho 211 wanachama wa FIFA.

Kwanza, mipango ya mradi inayopendekezwa ya Kombe la Dunia lazima ifafanuliwe katika mamia ya kurasa ambazo FIFA inalenga kuchapisha baadaye wiki hii. Lazima zijumuishe mipango ya viwanja, hoteli, viwanja vya mazoezi, usafiri na usalama wa taifa.

"FIFA itatathmini kwa kina vitabu vya zabuni na kuchapisha ripoti yake ya tathmini inayotarajiwa katika robo ya mwisho ya mwaka," shirikisho hilo lilisema katika taarifa yake.

Wazabuni wa Kombe la Dunia pia lazima sasa wawasilishe kwa tathmini ya wajibu wao wa haki za binadamu kuandaa mashindano hayo. FIFA ilialikwa Mei kufanya kazi na wataalamu huru kutathmini wagombeaji.

Sera ya FIFA ya haki za binadamu ilianzishwa miaka nane iliyopita baada ya kutoa matoleo ya 2018 na 2022 kwa Urusi na Qatar.

# Man United kujenga uwanja mpya

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United inatarajia kujenga uwanja wenye uwezo wa kuchukua watu 100,000 ndani ya miaka sita ijayo, kwa mujibu wa ESPN.

Klabu hiyo inatarajia kufanya uamuzi wa mwisho iwapo itajenga uwanja mpya au kuendeleza upya Old Trafford kabla ya mwishoni mwa mwaka huu.

Mradi huo unatarajiwa kugharimu zaidi ya pauni bilioni 2 huku United ikitarajia kutoa uwanja wenye uwezo wa kuchukua kati ya 90,000 na 100,000 ifikapo 2030.

Mmiliki mwenza Sir Jim Ratcliffe hapo awali alisema angependelea kujenga uwanja mpya katika eneo la uwanja wao wa sasa kwa kutumia ardhi nyuma ya Stretford End.

Mipango bado haijakamilishwa, lakini maafisa wa klabu wamepata msukumo kutoka kwa miradi kadhaa kama hii kote duniai, haswa kutoka kwa Uwanja wa SoFi na mradi wa uundaji upya karibu na Los Angeles.

United walicheza na Arsenal kwenye Uwanja wa SoFi huko Inglewood Jumamosi kama sehemu ya ziara yao ya kabla ya msimu mpya huko Merika na vyanzo vimeiambia ESPN kwamba wakubwa wa klabu wametembelea LA mara kadhaa katika miaka michache iliyopita.

Mshambuliaji wa zamani wa United, Andy Cole, ambaye alikuwa sehemu ya kikosi cha L.A. kwa ajili ya mchezo dhidi ya Arsenal, alisema: "Mashabiki wa Manchester United na kila mtu Kaskazini mwa Uingereza anastahili uwanja wa kiwango cha kimataifa, na SoFi iliweka kiwango hicho.

"Lakini unaweza kuona ulinganifu na fursa ya kurudi nyumbani huko Manchester. Uwanja mpya au uliotengenezwa upya Old Trafford unaweza kuwa kitovu cha ufufuaji wa eneo jirani."



# HABARI MICHEZO

## Gamondi ashikilia namba za mastaa

INATOKA UK. 24

wachezaji wapya kuonyesha kile ambacho kitamshawishi kuwapa nafasi kwenye kikosi cha kwanza au wataingia vipi kwenye mfumo wa timu.

"Niwaambie tu mechi ya kwanza dhidi ya FC Augsburg ya Ujerumani ambayo tulifungwa mabao 2-1, hatukuwa vizuri kabisa, ilikuwa ya kwanza na wachezaji hawakuwa na utimamu wa mwili, mechi ya pili tulishinda bao 1-0 dhidi ya TS Galaxy, ilikuwa ngumu sana kwa sababu walichezesha wachezaji wao wote tegemeo, lakini hii ya Kaizer Chiefs, ingawa haikuwa mechi rahisi, ila tulimiki mpira kwa kiasi kikubwa," alisema.

Yanga inatarajiwa kuendelea na kambi yake Kigamboni, Dar es Salaam, tayari kwa kilele cha Wiki ya Mwananchi, Agosti 4 na Ngao ya Jamii, Agosti 8 dhidi ya Simba.

## Fadlu ataka sasa ushindi kila mechi

INATOKA UK. 24

ishinda mabao 2-1, yaliyowekwa wavuni na Steve Mukwala na Joshua Mutale, ambao wote ni wachezaji wapya katika kikosi hicho.

"Kocha huyo alisema kambi ya nchini Misri imemsaidia vitu vingi, kukaa na kufahamiana na wachezaji, pamoja na kufanya mazoezi kwa uhuru na utulivu.

"Kuna vitu vingi tumevifanya na tumevimaliza katika kambi hii, tunajua wiki ijayo ni wiki ambayo tutakwenda kwenye Simba Day ambayo ni siku ya kwenda kuwatambulisha wachezaji mbele ya mashabiki wao," alisema.

Kwa upande wa Balozi Makanzo, ambaye alikuwa mgeni rasmi katika mechi zote tatu ilizocheza, aliwataka wachezaji kwenda kucheza soka kama walilolionyesha nchini humo.

"Nawashukuru Simba kwa kuweka kambi nchini Misri na nimefarijika kwa ujio wenu, niwatakie safari njema, nimeona maandalizi ni mazuri, vijana wanacheza vizuri sana, na timu mlizocheza nazo nimeziona ni ngumu na nzuri, lakini vijana hawa wanacheza soka safi mtu hadi unapenda kukaa kuwaangalia, ni burudani kwa kweli, nawatakia msimu bora," alisema.

Simba imecheza mechi tatu ikiwa huko, ya kwanza ni dhidi ya Canal FC, ikishinda mabao 3-0 yaliyofungwa na Jean Charles Ajoua (mawili) na Augustine Okejepha, wachezaji wapya wa timu hiyo, huku ya pili ikicheza dhidi ya Telecom Egypt na kushinda mabao 2-0, yakifungwa na Mashaka Valentino na Ladack Chasambi.



# KOCHA WYDAD AMPA MAUA YAKE FEI TOTO

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Wydad Casablanca ya Morocco, Rhulani Mokwena, ameonekana kuvutiwa zaidi na uchezaji wa kiungo mshambuliaji wa Azam FC, Feisal Salum 'Fei Toto', huku akisema amegundua kitu kingine kwake, ambacho ni utu na upole tofauti na wachezaji wengi wenye uwezo mkubwa kama wake.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa mechi ya kimataifa ya kirafiki kati ya timu hizo mbili uliochezwa juzi, Benslimane nchini Morocco ambako Azam imeweka kambi ya kujiandaa na msimu mpya wa mashindano, kocha huyo mpya wa Wydad, alisema amekuwa akimfuatilia mchezaji huyo mara kwa mara, na amemvutia, na siku hiyo amemwona mwenyewe mubashara uwanjani.

"Kwangu katika bara hili, Feisal ni mchezaji wa kipekee sana si tu kama mwanasoka, pia napenda utu wake, kiubinadamu ni mtu mzuri sana, mpole ni wachezaji mastaa wachache sana Afrika unaoweza kuwakuta wana tabia kama yake, wengi ni watata sana," alisema Mokwena ambaye msimu uliopita alikuwa akiifundisha Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini.

**Katika mechi ya juzi, Azam ilikubali kipigo cha mabao 4-1, mchezo ambao hadi mapumziko timu hizo zilikuwa sare ya bao 1-1.**

Akizungumzia mchezo huo, alisema ulikuwa mzuri na mgumu, ambapo Azam wamempa mechi nzuri ambayo imemfanya kuona mazuri na mapungufu ya kikosi chake.

"Naishukuru Klabu ya Azam, imenipa mechi nzuri, ilikuwa mechi kali na yenye kasi kubwa, nimeona uwezo wao na wachezaji wao, wanapambana sana, kwa hili walilolionesha hata wao wanaweza kufanya vema kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika," alisema.

Tayari Azam imeshacheza mechi tatu za kirafiki ikiwa kwenye kambi ya maandalizi nchini humo, awali ilikipiga dhidi ya US Yacoub Al Mansour ya Ligi Daraja la Tatu nchini Morocco, ikishinda mabao 3-0, kabla ya kucheza na timu ya Ligi Kuu, Union Touarga Sport na kutoka sare ya bao 1-1.

HAMNIWEZI...



Winga wa Simba, Joshua Mutale, akiwatoka wachezaji wa timu ya Al-Adalah FC ya Saudi Arabia kwenye mechi ya kimataifa ya kirafiki iliyopigwa juzi katika Uwanja wa New Suez Canal nchini Misri na kumalizika kwa 'Wekundu wa Msimbazi' kushinda mabao 2-1. **PICHA: SIMBA**

# *Singida BS kuivaa Aigle Noir siku ya tamasha lao*

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya Singida Black Stars inatarajia kucheza mchezo wa kirafiki wa kimataifa dhidi ya Aigle Noir ya Burundi kwenye Tamasha la Big Day, litakalofanyika Agosti 10, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Liti mkoani Singida, imeelezwa.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa Timu hiyo, Patrick Aussems, alisema kabla ya mchezo huo atakuwa na kibarua kingine na Namungo FC hapo kesho.

"Kabla ya mchezo huo nitakuwa na mchezo mwingine dhidi ya Namungo tutakaoucheza Agosti Mosi (kesho), ambao utanisaidia kuangalia safu yangu ya umaliziaji ambayo bado haijakaa vizuri," alisema Aussems.

Alisema michezo hiyo ya kirafiki watakayocheza anaamini itaimarisha kwa kiasi kikubwa wachezaji wake kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaoanza Agosti 16, mwaka huu.

Aussems alisema mchezo wa kesho utawasaidia kufanya vizuri katika mechi ya 'Big Day' ambayo watacheza siku ya tamasha hilo litakalopambwa na burudani mbalimbali.

Alisema msimu ujao utakuwa na upinzani mkubwa kwani kila timu imejipanga vizuri kuhakikisha inashika nafasi ya juu kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Michezo

Jumatano Julai 31, 2024

Nipashe



Man U kujenga uwanja mpya

UKURASA 22

UZI UMEMFIKIA...



Waziri Mkuu wa Tanzania, Kassim Majaliwa, akikabidhiwa jezi ya msimu mpya ya Simba na wasambazaji wa jezi hizo, Sandaland, baada ya mbio za NBC Dodoma Marathon zilizofanyika jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. **MPIGAPICHA WETU**

# GAMONDI ASHIKILIA NAMBA ZA MASTAA

**Adam Fungamwango na Shufaa Lyimo**

●●● Awaonya pia waliokuwa wakianza msimu uliopita, mashabiki Yanga nao watakiwa...

BAADA ya kutwaa taji lake la kwanza nchini Afrika Kusini kwa kuichapa Kaizer Chiefs mabao 4-0, Jumapili iliyopita katika Uwanja wa Bloemfontein, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi amesema kwenye kikosi chake hakutakuwa na mchezaji mwenye namba ya kudumu, hivyo kuwataka wachezaji wote hata wale waliotengeneza majina wakiwa kwenye timu yake msimu uliopita kujituma na kupambana zaidi ili kumshawishi.

Kocha huyo alizungumza hayo kwenye Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere, Dar es Salaam, juzi alfajiri wakati kikosi cha timu hiyo kilipowasili nchini kikitokea Afrika Kusini, ilikoalikwa kwa michezo kadhaa ya kirafiki ya kimataifa, ikitwaa Kombe la Toyota lililoandaliwa na wenyeji wao, Kaizer Chiefs.

Gamondi alisema wakati Ligi Kuu na michezo ya kimataifa inaanza, atapanga kikosi chake kutokana na mchezaji atakayejituma mazoezini na si kwa mihemko ya mashabiki, akiwataka wasubiri soka safi, burudani na ushindi, huku mambo ya kupanga kikosi wamwachie yeye kwani pia wapo wachezaji wapya ambao wameonyesha uwezo mkubwa.

"Tayari nimeshaona kuna watu wanahoji kwa nini wachezaji fulani wamekaa benchi, kwa nini wameingia kipindi cha pili, na kwa nini wachezaji fulani wameanza wengine hawajaanza, huu ni mpira wa miguu, unahitaji wachezaji 11 tu, kwenye kikosi na nina wachezaji 27, natakiwa kuchagua 11 tu wa kuanza kutokana na mpinzani ninayecheza naye, jinsi mchezo unavyoendelea na vitu vingi vya kuangalia, kikubwa ni kwamba timu inacheza vizuri," alisema kocha huyo.

Gamondi alisema hayo baada ya kuulizwa sababu za kutowaanzisha wachezaji, Clatous Chama, Pacome Zouzoua na Mudathir Yahya katika mechi dhidi ya Kaizer Chiefs ambao waliingia kipindi cha pili.

**Alisema kitu anachotaka wachezaji wamfanyie uwanjani ni kazi na kujituma na ameshawaeleza hivyo.**

"Kazi na kujituma, ndiyo msemo wangu, ukicheza soka zuri matokeo mazuri yanakuja yenyewe," alisema.

Akizungumzia michezo waliyocheza Sauzi, alisema hakuangalia zaidi matokeo, bali timu inachezaje, pia kuwapa nafasi

INAENDELEA UKURASA 23

## Fadlu ataka sasa ushindi kila mechi

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI kikosi cha wachezaji wa Simba kikitarajiwa kutua nchini leo kikitokea Misri ambako kiliweka kambi ya kujiandaa na msimu mpya wa mashindano, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Fadlu Davids, amesema kikosi chake kimeiva na lengo sasa ni kupata ushindi kila mechi watakayocheza.

Hata hivyo, wakati kocha huyo raia wa Afrika Kusini akisema hayo, Balozi wa Tanzania nchini Misri, Meja Jenerali Richard Mutayoba Makanzo, amesema katika mechi zote tatu alizoangalia, wachezaji wa Simba wamekuwa wakisakata kandanda la hali ya juu na la burudani kwa mpenda soka yoyote angependa kuwaangalia.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa mchezo uliochezwa juzi usiku Uwanja wa New Suez Canal, dhidi Al-Adalah FC inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza nchini Saudi Arabia, kocha huyo alisema ingawa bado hajafika mwisho wa kukinoa kikosi hicho, lakini mwanga unaonekana na vitu vingine vimekwenda kama vilivyopangwa na kuahidi kumalizia mambo machache tu ya kiufundi yaliyobaki.

"Tumemaliza 'pre season' vizuri, bila kuzalisha majeruhi wengi, isipokuwa Kagoma (Yusuph), nadhani wiki ijayo atarejea ni yeye pekee ndiyo nilimkosa kwa wiki mbili, kila kitu hivi sasa kipo vizuri kwa maana ya dakika za kucheza, kila mchezaji amepata dakika kadhaa za kuwa uwanjani, tumepata matokeo leo (juzi) na mechi zote zilizochezwa, ila siyo muhimu sana kwetu, zaidi ilikuwa ni kuangalia namna gani ya kuzuia, kulinda na kushambulia.

"Tayari huko tumeshamaliza, hii wiki ya tatu iliyobaki ni ya kutazama mbinu na ufundi uwanjani, hapa napaswa kuingiza vitu hatua kwa hatua ndani ya kikosi hiki wachezaji waelewe zaidi, lengo mama ni kushinda kila mechi iliyo mbele yetu," alisema kocha huyo.

Katika mechi hiyo, Simba il-

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >